**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

## BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 3 Juni, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

## DUA

Mhe. Naibu Spika. *(Ali Abdalla Ali)* alisoma Dua

## MASWALI NA MAJIBU

**Nam. 72**

### Kurudi Nyuma kwa Huduma za Ushushaji na Upakuzi wa Makontena Bandarini

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza :

Kutokana na mabadiliko ya Sera za Biashara na Uchumi, Zanzibar ina Shirika lake la Bandari lakini huduma za ushushaji Makontena na upakizi unaendelea kurudi nyuma kutokana na uhaba wa nyenzo.

(a) Kwa nini Serikali isibinafsishe shughuli hizo kama ilivyofanya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa kuipa Kampuni ya *TICKS* kushusha mizigo katika bandari ya Dar-es-Salaam badala ya Mamlaka ya Bandari Tanzania.

(b) Kwa kuwa Bandari ndio nguzo ya uchumi wa nchi kwa nini tunashindwa kuandaa mipango mizuri ya kuwa na Bandari ya Huduma bora na kuwa mfano Afrika Mashariki.

(c) Kwa kuwa kumekuwepo na hadithi ya muda mrefu ya kujenga Bandari Huru bila ya utekelezaji wake kuonekana, kwa nini Serikali isitafute mwekezaji wa kushirikiana naye katika eneo hilo chini ya Mpango wa *P.P.P* hasa kwa kuzingatia tunao wafanyabiashara wakubwa na wenye uchungu wa nchi Tanzania Bara na Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano) -** Alijibu :-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 72 lenye vifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

Kutokana na mabadiliko ya sera ya biashara na uchumi Zanzibar ina Shirika lake la Bandari lakini huduma za ushushaji wa Makontena na upakizi unaendelea kurudi nyuma kutokana na uhaba wa nyenzo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumfahamisha Mheshimiwa kuwa Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imekuwa ikijitahidi kuimarisha huduma za Bandari ya Malindi kwa kuipatia vifaa vya kazi kila hali inaporuhusu, kwa mfano mwaka jana (2014) Shirika lilifanikiwa kununua Tagi mpya yenye uwezo mkubwa wa kuhudumia meli.

Mwaka huu (2014/2015) Shirika lina mpango wa kununua vifaa vipya vya kunyanyulia mizigo bandarini ambapo zabuni za vifaa hivyo tayari imeshatangazwa katika vyombo vya habari. Ni mategemeo ya Wizara yangu kuwa baada ya Shirika kupata vifaa hivyo huduma za ushushaji na upakizi wa mizigo zitaimarika zaidi.

a) Serikali haiwezi kubinafsisha huduma za ushushaji wa makontena katika Bandari ya Malindi kwa sasa kwa sababu Bandari ya Malindi ni bandari inayotoa huduma za aina mbali mbali *(Multipurpose Terminal)* ikiwemo kuhudumia meli za aina tafauti (Meli za mizigo mchanganyiko, Makontena, Meli za Abiria, Meli za Kitalii, Meli za Kijeshi n.k.). Aidha, bandari hiyo inatoa huduma kwa abiria wa ndani na Watalii wanaokuja na Meli za Kitalii.

    Kwa maana hiyo, Bandari ya Malindi ni tafauti na sehemu iliyobinafsishwa katika Bandari ya Dar-es-Salaam kwani sehemu hiyo inatoa huduma za makontena pekee. *(Container Terminal).*

    Mipango ya Serikali hivi sasa ni kujenga Bandari mpya katika eneo la Mpiga Duri kwani Bandari ya Malindi haiwezi tena kuendelezwa zaidi kutokana na ukosefu wa eneo katika bandari hiyo.

Serikali inaendelea kuwasiliana na Benki ya *Exim* ya China ili kukamilisha taratibu za kupata mkopo kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo ambapo matayarisho ya awali

yameshakamilika ikiwemo kuwasilisha Ripoti ya Upembuzi Yakinifu, Uchunguzi wa Kimazingira, Michoro ya Awali tayari imeshawasilishwa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa Naibu Waziri nafikiri *birthday* yake ya jana imemsababisha mpaka kusahau.

**Mhe. Naibu Spika**: Swali la nyongeza.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Nibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Kaimu Waziri alitumia uzoefu wake kwa vile yeye alikuwa mjumbe wa bandari kwa muda mrefu kujibu swali hili, lakini nitakuwa na maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

a) Bandari ya Dar es Salaam inategemea eneo la mizigo ya abiria kama ilivyo Zanzibar, je ni lini abiria wa Zanzibar wamewahi kushushwa katika eneo la mizigo, hadi kufikia Serikali isibinafsishe huduma ile.

b) Kwa kuwa huduma za Bandari ni muhimu kwa uchumi wa nchi, kwa nini Serikali iendelee na uzito wa kubinafsisha wakati Tanzania Bara faida yake inaonekana ikiwemo kuongezeka kwa mapato, Tanzania bara wamebinafsisha na mapato yamekuwa yanaongezeka, huu wimbo imekuwa muda mrefu Shirika la Bandari wananunua vifaa, sijui Tanzania havifiki sijui vinatengenezwa au viko njiani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, samahani namuomba Mhe. Mjumbe aulize taratibu ili nimuelewe anachokusudia kitu gani, swali lake la kwanza sikumsikia, anavuma, azungumze taratibu mimi nimsikie.

**Mhe. Naibu Spika:** Maswali hakuyasikia hata moja Mhe. Naibu Waziri, Mheshimiwa anza tena.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, bandari ya Dar es Salaam inategemea eneo la mizigo na abiria kama ilivyo Zanzibar, bandari ya Dar es Salaam ni kama bandari ya Zanzibar ilivyo. Lini abiria wameshushwa katika eneo la mizigo hadi ikafika Serikali hadi hii leo isibinafsishwe nafikiri Mhe. Naibu umesikia hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa huduma za bandari ni muhimu kwa uchumi wa nchi, na ukizingatia ni kioo cha mapato yetu, kwa nini Serikali iendelee na uzito wa kukalia

suala hili la kutokubinafsisha, wakaiga kwa mfano kwa ndugu zetu wa damu wa Tanzania Bara walivyobinafsisha ukizingatia faida yake au matunda yake hivi sasa tunayaona uchumi umekua kwa kiasi kikubwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Naomba nimkumbushe tu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba anaujua vizuri sana ukuta wa bandari yetu, kwa maana kwamba ile *wharf* upande wa magharibi una mita zisizozidi 120 mpaka 130, kati ya urefu huo kuna kipande ambacho kinatumiwa kwa ajili ya *passenger terminal,* kuna kipande ambacho tunatumia kwa ajili ya meli, lakini upande wa Kaskazini ambao una mita takriban 90 anajua fika Mhe. Spika, kwamba tunatumia kwa abiria tunatumia kwa mizigo.

Sasa tunaposema kwamba tubinafsishe tunabinafsisha kipande kipi, maana katika kipande ambacho hakizidi mita 200 tayari tumeshafanya eneo moja ndio tumewapa *terminal passenger* lakini eneo dogo lililopo tunatumia kwa ajili ya meli.

Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba dhana na dhamira ya kutaka kubinafsisha ni nzuri, lakini anapochukua mfano wa Dar es Salaam atakuwa hachukui mfano mzuri, Dar es Salaam bandari yao ina *terminal* 14 ziko za mafuta, ziko za mizigo, ziko za majahazi, zipo za abiria. Kwa hivyo eneo la *TICS* analochukulia yeye mfano ni miongoni mwa maeneo ambayo yametengwa maalum kwa ajili ya *container terminal.* Kw hivyo nimuombe Mhe. Jaku kwamba kwa kipindi hiki Serikali yetu hatuwezi kuwa na nafasi ya kukidhi kwa ajili ya kubinafsisha kwa shughuli za makontena.

**Nam. 79**

**Kukosekana Daktari wa Mifupa Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza :-

Serikali hivi karibuni imetoa ushauri mzuri kwa Wabunge na Wawakilishi kutafuta Magari ya Kubebea Wagonjwa katika Majimbo yao kutokana na kauli ya Mkuu wa Huduma za Jamii tarehe 14/4/2015 kupitia Vyombo vya Habari. Lakini cha kusikitisha na cha kutia huruma kutokuwepo Daktari wa Mifupa masaa 24 hapo Mnazi Mmoja Hospitali kwa kuzingatia ajali zimekuwa nyingi.

(a) Je, ni lini Serikali itaweka Daktari Mnazi Mmoja wa Mifupa masaa 24 ili kuwaokoa wananchi katika maradhi.

(b) Tumeshuhudia nikiwemo mimi ninayeuliza swali hili usumbufu mkubwa wa kutafuta Daktari hapo Mnazi Mmoja na mgonjwa kusubiri hadi siku ya pili kupata matibabu. Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuharakisha hatua za kumpata daktari huyo kwa masaa 24.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya – ** Alijibu :-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 79 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwanza kabla sijamjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake namba 79 nilikuwa naomba kidogo Mheshimiwa atusaidie hapa maana tumelijibu a na b lakini katika maelezo yake ya juu ameeleza kuna kauli imetolewa na Serikali na Mkuu wa huduma za jamii na kauli hii sisi tumeangalia. Kwanza (a) hakuna mtu mwenye cheo anayeitwa Mkuu wa Huduma za Jamii ndani ya Wizara yetu.

Lakini la pili taarifa iliyotoka katika vyombo vya habari ilikuwa ni taarifa ya kijamii, yaani Wabunge wenyewe wamefanya shughuli yao na Mbunge mmoja alikuwa akitoa kifaa cha aina ya Ambulance, kwa hiyo yule Afisa wa Wilaya ile akashauri Wabunge wote au Wawakilishi wote waige mfano huo, kwa hivyo hiyo sisi hatukuichukulia kama taarifa rasmi ya Wizara ya Afya.

Taarifa rasmi ya Serikali ya Wizara ya Afya ni kuwashajihisha Wabunge na Wawakilishi kujenga zaidi nyumba za makaazi za wafanyakazi vijijini ili wananchi waendelee kupata huduma masaa 24. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa aweke sawa swali lake kwanza kwa kutueleza amekusudia nini huyu Mkuu wa Huduma za jamii, na kauli ipi ya Serikali aliyokusudia Mheshimiwa.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

**Mhe. Naibu Spika:** Kaambiwa Mhe. Jaku atoe maelezo alivyokusudia maana Naibu Waziri kidogo hakufahamu swali lake, naona unasimama wewe. Mhe. Jaku umemfahamu Mhe. Waziri.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana nimemsikia Mhe. Naibu Waziri, nilichokusudia hapa Mhe. Naibu Spika, Serikali hivi karibuni imetoa ushauri mzuri kwa Wabunge na Wawakilishi kutafuta magari ya kubebea wagonjwa katika Majimbo yao kutokana na kauli hii iliyotoka hapa kwa Afisa mmoja aliyekuwa anapokea msaada au vipi kutoka Wizara ya Afya na jina lake nimeli- *quote* lakini halikupendekezwa kutajwa hapa sijui nafikiri ameshafahamu Naibu Waziri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kupata ufasaha zaidi lakini nimshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Muyuni kwa kuliweka wazi, maana ameweka wazi kwamba ni Afisa mmojawapo aliyetoa kauli hiyo na sio Mkuu wa Huduma, kwa hivyo amelirekebisha swali lake. Sasa naomba nimjibu swali lake lenye vifungu a na b nambari 79 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali pekee ya Rufaa kwa Zanzibar ambayo inafanya kazi ya kutoa huduma bora za afya kwa masaa 24. Kiutaratibu wagonjwa wote wanaofika Hospitali wakiwemo wagonjwa wa ajali kwanza kabisa wanatakiwa wapitie kitengo cha huduma za dharura *(Emergency department)* kwa kupatiwa matibabu ya haraka zaidi katika kitengo hicho ambacho madaktari wake pia wanatakiwa wawepo masaa 24, na hivi sasa kwa bahati nzuri tuna wale madaktari ambao wamemaliza masomo yao wanaitwa *Intern* wanafanya kazi pale wanapatikana kwa saa 24.

Baada ya kupatiwa matibabu ya haraka mgonjwa anapelekwa Idara husika kwa kupata matibabu zaidi, ikibidi kama kulazwa anapelekwa kwenye *admission* ili alazwe kwenye wodi na kama suala ma *medical* anashughuliwa kwa upande wa *medical,* kama suala la *surgeon* anahitaji upasuaji anashughulikiwa huko.

Kwa sasa Hospitali ya Mnazi Mmoja ina utaratibu maalum wa madaktari wa zamu kwa kila Idara kuwepo Hospitali kwa masaa 24 *(Doctor on Call).* Lakini si idara zote zilizokuwa na madaktari saa 24 kwa siku. Tatizo moja lililopo ambalo tunakiri eneo linalotoa huduma ya *Emergency service* kwa saa 24 ni dogo, pana uchache wa nafasi na hivi sasa mategemeo yetu makubwa sote tumeelekeza kwenye jengo jipya linalojengwa na *Orio* tukishirikiana na SMZ na Serikali ya Uholanzi kupata *emergency room* ya kisasa na ya uhakika. Maana wenzetu pia juzi waliofungua Hospitali yao ya *Private* tumeona *emergency room* yao ni kubwa zaidi, na ina vifaa zaidi kuliko ya kwetu. Kwa hivyo ile sasa hivi inatoa tu huduma za *emergency* za hapa na pale lakini bado haijafikia kile kiwango kinachotakiwa cha *emergency room* ya masaa 24.

Kitengo cha mifupa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kinafanya kazi zake za kutoa matibabu kwa masaa 24 kwa kufuata utaratibu maalum uliowekwa na Hospitali. Kwa sasa kitengo cha Mifupa kina jumla ya Madaktari bingwa wa mifupa 2 *(Orthopeadic surgeons),* na hapa tuna uhaba mkubwa wa madaktari wa mifupa, mmoja daktari huyo ni daktari mzalendo wa hapa hapa na wa pili ni Daktari kutoka Cuba ambaye tumempokea katika mashrikiano ya msaada tunaopata na Serikali ya Cuba.

Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeweka usimamizi maalum wa kufuatilia kazi za kila siku za Hospitali, na tatizo lolote linapotokea linalohusu utendaji wa kazi kwa ujumla au kuhusiana na daktari baina ya saa moja na nusu mpaka saa tisa na nusu malalamiko yanatakiwa yapelekwe Ofisi ya Daktari Mkuu katika jengo la Utawala kwa kupatiwa ufafanuzi yaani *Chief Medical Superitendent* Dkt. Nofal Kassim.

Na baada ya kumalizika muda huo huduma za Hospitali kwa ujumla zinaendelea kama kawaida katika Idara zake zote kwa mujibu wa utaratibu maalum uliopangwa, ambapo Msimamizi wa zamu *(Supervisor)* anachukua dhamana ya Hospitali ya kufuatilia utendaji wa kazi na uwajibikaji kwa ujumla.

Na iwapo kutatokea malalamiko yoyote kwa wakati huo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanatakiwa wasisubiri mpaka wakati wa bajeti au wakati wa kipindi cha maswali na majibu, pia huduma hizo zinashughulikiwa kwa saa 24 hapo hapo na leo nitaweka wazi na nitalieleza.

Iwapo kutatokezea malalamiko yoyote kwa wakati huo baada ya saa za kazi yanatakiwa yapelekwe kwa msimamizi mkuu yaani *Chief Nursing Supervisor au Chief Nursing Officer* ambaye yupo hapa leo katika ukumbi huu amekuja, nitaomba asimame ili aonekane naomba Bi. Magreth asimame yupo hapa amekuja na namba yake ya simu kwa ruhusa zote na ridhaa zote amepata 0779 951525 na imeandikwa humu katika waraka ambao umewasilishwa ndani ya Baraza la Wawakilishi ambao unaingia kwenye *Hansard*.

Kwa hivyo nawaomba Wajumbe na wananchi, lalamiko lolote; mtu kazuiliwa mlangoni, askari kamzuia hajaweza kufanya hichi, hajaweza kupeleka chakula kwa mgonjwa huyu ndio mpokeaji wa malalamiko. Msimsubiri Mhe. Rashid Seif Suleiman wakati wa bajeti, kwa sababu lile tatizo litakuwa limeshapitwa na muda na halijashughulikiwa, na kama ni dogo basi litaendelea kuwa kubwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri lakini ningelimuomba afute usemi wake Hospitali ya Mnazi Mmoja haijafika hospitali ya Rufaa mpaka hivi sasa tunavyozungumza, nazungumza Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tukienda mguu kwa mguu Kitengo cha dharura *oxygen* hakuna haipatikani. *Oxygen* ni kitu muhimu kuokoa maisha ya mwanadamu, *oxygen* haipo, sizungumzi kwa kubahatisha. Kwa hiyo huduma masaa 24 daktari yupo lakini huduma hazipo.

Mhe. Naibu Waziri kwa mujibu wa Kanuni za Baraza letu linakataza Mjumbe au kiongozi kujibu au maelezo yasiyo na ukweli. Katika majibu ya msingi Mhe.

Naibu Waziri madaktari wanapatikana masaa 24 lakini daktari wa mifupa hapatikani. Hii kesi mimi imeshanikuta, inafika siku ya pili kutafutwa daktari ndio nampata, itokee nitafute njia nyengine ya kumtafuta Dokta Shaibu. Nimshukuru sana Dokta Shaibu, lakini kitengo hichi kimetajwa kinakaa masaa 24 hakipo kitiba. Ukizingatia ajali zimekuwa nyingi, kwa hivyo nimekunasihi sana mtafute njia mbadala ya kuweka daktari masaa 24 awe wa kudumu, hilo la kwanza.

Suala la pili, kwa kuwa ubora wa hospitali unazingatia upatikanaji wa huduma ikiwemo vifaa na dawa. Je. Mhe. Naibu Waziri unaposema Mnazi Mmoja kuna huduma bora kati ya mambo matatu, lipi linalopatikana; dawa, huduma au vifaa ili wananchi waweze kufahamu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, juzi bahati nzuri nilikuwa katika jimbo langu nimekaa nyakati za usiku na kuna sehemu katika jimbo letu hili la Kiembesamaki kunaitwa Entebbe, kwa wale wenyeji watakuwa wameshafika Entebbe. Kuna vijana ambao nyakati za usiku wanaendesha hivi vyombo vya moto vya matairi mawili na huwa wanapakiana watu wanne mpaka watano, wanaita wenyewe mshikaki.

Sasa kuna vijana ambao nawafahamu niliwasimamisha nikawaambia jamani mnapakiana kama hivi sisi tuna madaktari wawili tu wa mifupa, bahati nzuri wakanifahamu.

Mhe. Naibu Spika, na leo nalirejea tena, hapa tuna madaktari wawili tu hivi sasa wa mifupa. Katika kitabu cha bajeti kwenye kiambatanisho kimoja wapo kimeandikwa taaluma mbali mbali. Tunaendelea na jitihada ya kuwatafuta wengine, tunaendelea na jitihada ya kuwasomesha wengine lakini madaktari wawili hawatoshi kwa *population* ya watu milioni moja takriban na laki nne, haitoshelezi na hawa ndio mabingwa. Kwa hivyo hata *referrals* za Pemba zikitokea kubwa za mifupa zinaletwa Mnazi Mmoja.

Mimi bado nataka kusema kwamba huduma za Mnazi Mmoja hapa zilipo kwa bajeti yetu tunayoipata ni bora zinatusaidia. Akianguka Mwakilishi yeyote humu ndani pahali pa mwanzo atakapopelekwa itakuwa ni Mnazi Mmoja, kwa sababu wataalamu wapo. Na wameshawahi kuanguka Wawakilishi wengine wamepelekwa Mnazi Mmoja. Kwa hivyo ninachotaka kusema huduma zinatolewa saa 24. Hivi sasa tumechukua *interns* wale madaktari waliokuwa wamemaliza masomo ambao wanafanya kazi pale zaidi ya 70 na ni kada mbali mbali. Tunachokosa kidogo sasa hivi ni *specialization,* na ndio maana katika kauli ya Rais na hotuba zake kadhaa kila mara amekuwa akisisitiza kwamba vijana waliomaliza masomo yao, wazalendo tunatakiwa tuwapeleke kwenda kusoma masomo ya juu zaidi ili waweze ku- *specialize*.

Katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya jana ameeleza kwamba wapo madaktari 9 kutoka pale pale ambapo wamekwenda kufanya *specialization*. Kwa hivyo *specialization* hizo zikishakupatikana naamini huduma zetu zitakuwa bora zaidi. Lakini naomba pia nikubaliane naye lakini kwa kumrekebisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Hospitali kitu cha mwanzo kabisa sio dawa, sio chochote chengine ni vipimo, kwa sababu vipimo ndiyo vinam -*guide* daktari kujua tatizo la mgonjwa. Laa sivyo anakuwa yule daktari anakisia.

Zamani kama mtachunguza daktari yeyote anakuwa ana *status copper* anaivaa pale hata hakupeleki kupima damu, moja kwa moja wewe unatizama *temperature*, malaria. Kwa sababu malaria ilikuwa ipo kwa wingi sana hapa Zanzibar. Lakini sasa hivi kwa maradhi yaliyoendelea haya zaidi na yaliyoibuka mapya vipimo ndio kitu cha mwanzo. Ndio maana wenzetu Dar-es-Salaam kule, Muhimbili, Ocean Road, wana-*concentrate* kwenye vipimo yaani (*diagnosis*). Kwa sababu daktari baada ya kumuona kitu cha mwanzo anachokuandikia madaktari wetu *professional* waliokuwepo sasa, kitu cha mwanzo wanachokuandikia ni kipimo aidha cha damu au cha *image* yaani picha au vipimo vyengine vyovyote. Sasa inapokuwa vipimo hivyo hakuna inakuwa tatizo, kwa upande wa vipimo tunajitahidi.

La pili kuwa na human *resources* yaani kuwa wale madaktari wenyewe ambao wanatoa zile huduma hata kama vipimo havipo pale Mnazi Mmoja unaweza kwenda kupata vyengine.

Tatu baada ya kujulikana yote hayo ni dawa. Sasa Mhe. Jaku Hashim, alikuwa ameweka dawa mwanzo, dawa inakuja mwisho baada ya kugundulika matatizo uliyokuwa nayo. Kwa hivyo kwa *standard* zetu kwa bejeti yetu jamani. Bajeti yetu ni bilioni chache hazitoshelezi kabisa katika sekta ya afya. Sisi *target* yetu tunatakiwa ili tufanye kazi vizuri ni bilioni mia moja na ishirini ndio tunatakiwa tuzipate. Na nyinyi wenyewe mnajua Mhe. Waziri alichokisoma jana kama bilioni 84, kwa hivyo bado kuna *deficit* katika sekta nzima ya afya, kuna *deficit*. Tuwashukuru madaktari wetu, tuwashukuru wauguzi wetu. Wanachelewa kupata *call allowances* zao wanafanya kazi kizalendo.

Humu ndani naamini tukichelewa kupata *allowance* yetu hapa patakuwa na zogo. Lakini madaktari wanakubali kufanya kazi katika hali ngumu ya kuchelewa pia kupata *call allowances* zao, hasa wale wanaokwenda kwa saa 24 au wanakwenda baada ya saa za kazi. Kuna wauguzi, kuna ma-*orderly* wote wanafanya kazi kwa moyo wa kizalendo.

Sitaki niseme zaidi lakini tuwapongeze madaktari wetu, naomba tuwapongeze wauguzi wetu, naomba tuwapongeze wale wasaidizi wao wote, tuwapongeze

wafanyakazi wa sekta ya afya kwa kufanya kazi katika bajeti yenye *deficit* zaidi ya asilimia 40. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Waziri, kifungu cha 37 nafikiri hana haja ya kuki- *quote* swali langu namba 2 Mhe. Naibu Waziri nafikiri hakulisikia naomba nirudie tena.

Kwa kuwa ubora wa hospitali unazingatia upatikanaji wa huduma ikiwemo vifaa. Mhe. Naibu Waziri unaposema Mnazi Mmoja kuna huduma bora kati ya mambo matatu, huduma, vifaa na dawa, hivi sasa ninachozungumza ni kwamba *oxygen* katika kitengo cha dharura haipo. Unatoa kauli gani kwa wananchi ukizingatia *oxygen* ni kitu muhimu. Hivi sasa una bajeti kipindi hichi na hivi sasa *oxygen* haipo. Inatia huzuni inatia uchungu, inafika wakati kulia, *oxygen* ni kitu gani inafika mpaka inakwisha hospitali, hebu toa kauli Mhe. Naibu Waziri tukusikie wakati leo hii una bajeti yako.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, swali lake hakuuliza habari ya *oxygen*, aliuliza habari ya vifaa dawa na vipimo na ndio nililolijibu mimi. Hii *oxygen* imekuwa ni swali jipya, lakini naomba nilijibu Mheshimiwa, *oxygen* ni swali jipya. Sasa utaratibu huu tutakwenda nao.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa *oxygen* juzi nimekaa mimi mwenyewe na bahati nzuri kuna ushahidi uliorikodiwa kwa TV tume-*record under camera*, nimekaa na kitengo cha *engineering*, nimekaa na wauguzi wanaoshughulikia suala hili wamesema kweli ilikwisha *oxygen*, kulikuwa na *shortage* ya siku mbili tatu kutokana na kwamba hivi sasa tunaagizia matenki kutoka Tanzania Bara, *Tanzania Oxygen Limited* na tunaagizishia chupa 240, ni nyingi sana hizo kila mwezi. Lakini zinakuwa hazitoshelezi na wale inabidi walipwe kwa wakati kule, kama hatujalipa kwa wakati hatupati.

*Solution* ya kutatua tatizo hili pekee ingewezekana kama kuna fedha sehemu nyengine tungesema zichomolewe kwengine tupewe sisi. Lakini *solution* pekee kwa Mnazi Mmoja ni kujenga *tank* la *oxygen* pale pale. Hospitali zote zenye uwezo kama Mnazi Mmoja zina uwezo wa kulaza wagonjwa mpaka 440 kwa siku zilizokuwa zinapokea zaidi ya wagonjwa 2000 kwa siku, pale wanapokewa mpaka 2800 wagonjwa na watu wanaoingia katika kijiji kile kinahitaji *oxygen tank.*

Tenki kubwa tulijenge pale iwe *oxygen* ina *supply* moja kwa moja, hizi paipu na laini tumeshatia, lakini zile paipu ukitia lile *tank* moja tu basi kufika kwenye paipu zote kwa sababu lile *tank* limekwisha hata haijaanza kutumika ile *oxygen* bado. Ile *supply* ya kuingia mle kujaa mle katika paipu inakuwa imekwisha kabla hata ya lile tenki halijatumika. Kwa hiyo *solution* ni kupata *tank* na gharama zake ni kubwa.

Kwa hivyo hilo tatizo tunalifahamu, lakini naendelea kusisitiza kwa hali tuliyonayo *oxygen* sasa hivi imeshafika ipo, tunaagizia kila mwezi chupa 240 ndio uwezo wetu na ndio kwa fedha tunazozipata zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi hapa, na kila zikipungua huwa tunaomba wakati mwengine mkopo kwa wenzetu wanatusaidia na baada ya fedha kupatikana huwa tunawalipa.

Kwa hiyo kwa suala la *oxygen* kwa hii leo akianguka humu mtu hiyo *oxygen* ipo na kama itatakiwa baadaye tutaileta humu tenki ionekane hapa na Mhe. Jaku Hashim.

**Mhe. Naibu Spika:** Maswali yote matatu kamaliza mwenyewe Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Tunaendelea Katibu.

**Nam. 19**

**Kufanyika kwa Tathmini ya Kimazingira**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Aliuliza:-

Kwa kuwa uwekezaji wowote mkubwa hufanyika baada ya serikali kufanya *Evironmental Impact Assessment (EIA).* Baada ya serikali kufanya tathmini ya kimazingira na kuridhika, hutoa masharti kwa mwekezaji.

a) Je, serikali iliwahi kufanya tathmini ya kimazingira kwenye hoteli ya *Muyuni Hotel & Spa*.

b) Kama ilifanya Je, serikali iliwahi kutoa maelekezo ya kimazingira kwa mwekezaji huyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 19 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kama ilivyo utaratibu wa uwekezaji wa miradi mikubwa ya sekta yoyote inapaswa mwekezaji kufanya uchambuzi wa athari za mazingira (*EIA*). Wawekezaji wa *Muyuni Hotel & Spa* waliagizwa kuifanya kazi hiyo na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar. Kwa bahati nzuri, kazi hiyo imefanyika kama walivyoelekezwa na baadaye kupatiwa cheti (*certificate*) yenye nambari IM/EIA/13 ya mwaka 2011 yenye masharti 17.

b) Mhe. Naibu Spika, serikali ilitoa maelekezo ya kimazingira kwa mwekezaji huyo yaliyoainishwa katika kibali hicho nilichokitaja. Kwa kawaida baada ya kazi hiyo, Idara ya mazingira hufanya kazi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa masharti hayo. Masharti (17) aliyopewa na Idara ya Mazingira ameyatekeleza. Hata hivyo, mradi huo umezuiwa kutokana na kushindwa kufuata masharti ya ujenzi ambapo mwekezaji alitakiwa asijenge ndani ya mita 30 (aziache) kutoka ufukweni mwa bahari.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa mwekezaji wa hii hoteli niliyoitaja hapa tayari ameshajenga mpaka kwenye ufukwe. Na kwa kuwa mnasema kwamba amezuiliwa lakini yale makuta yake bado yapo pale kiasi ambacho kasa wanakosa raha kwenda kutaga kule katika sehemu za ufukwe kutokana na ule ukuta.

a) Je, ni lini serikali itatoa amri ya kwenda kuvunja ule ukutas, kusudi viumbe kasa wapate raha ya kwenda kutaga kwenye ule ufukwe.

b) Kwa kuwa pale jirani kuna hoteli iliyojengwa chumba cha chini ya bahari, na kwa kuwa inasadikiwa chumba kile hakikufanyiwa hii (*EIA*) yaani *Evironmental Impact Assessment*. Je, kama ni kweli Mhe. Naibu Waziri ni lini serikali itakwenda kufanya *environmental auditing* hasa ukitilia maanani kwamba ile ofisi ya yule mama anayehusika na mambo ya Mdhibiti wa Hesabu za Serikali anao wataalamu sasa wa kuweza kufanya *environmental assessment*. Je, ni lini serikali itapeleka wataalamu wale kwenda kufanya *environmental auditing* ili ikiwa kuna tatizo katika mradi ule ambao utaharibu mazingira uweze kuzuiliwa, ukitilia maanani kwamba kila muwekezaji sasa anataka kujenga chumba cha chini ya bahari.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Saleh Nassor, Mwakilishi wa Jimbo la Wawi nataka uamini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kweli imeleta muongozo wa kutosha kwenye serikali na kwa wawekezaji.

a) Pia kama swali hili ulililoliuliza Mhe. Saleh ni kuwa wizara yangu kwa kushirikiana na *ZIPA* ndiyo iliyokaa pamoja kuweza kutoa maamuzi ya kumzuia mwekezaji huyu. Kwa sababu wananchi pale wanatakiwa maeneo yale ya fukwe waweze kuyatumia na waweze kupata maslahi yao ya kujiendeshea maisha yao.

b) Mhe. Mwakilishi swali lako la pili umezungumzia kuhusu swali la chumba cha chini kilichopo kwenye hoteli ya Manta Reef. Mheshimiwa serikali kwa kushirikiana na mwekezaji huyu wameshirikiana pamoja kuweza kufanya utafiti ili kujua ni kitu gani ambacho hakitoleta athari kwa chumba kile na wananchi na wawekezaji wanaokuja.

**UTARATIBU**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Katika swali langu niliuliza je, ile hoteli ya kile chumba cha chini ya bahari kimefanyiwa *evironmental assessment*, na kama hakikufanyiwa, je, serikali ni lini itapeleka wataalamu kwenda kufanya *environmental auditing* kama kuna athari za kimazingira zinazotokea chini ya bahari, basi tuweze kujikinga nazo, hasa ukitilia maanani kwamba kila mwekezaji sasa hivi anataka kujenga chini ya bahari. Sasa ikiwa kina madhara kile tujue vya kujikinga. Ikiwa haikufanyiwa *evironmental assessment*, ni lini serikali itafanya *environmental auditing*.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, narudia tena jibu la pili Mhe. Saleh Nassor. Wawekezaji wote huwa wanashirikiana na watu wa mazingira kufanya utafiti na wanashirikiana na *ZIPA* ndipo anaruhusiwa mwekezaji yeyote kuwekeza kwenye maeneo yetu ya Unguja na Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongeza kama ifuatavyo.

Kwa sababu viumbe vya bahari na utafiti wa bahari ni endelevu, basi niseme tu nimwambie Mhe. Mwakilishi kuwa serikali inafanya utafiti kila baada ya kipindi na tukibaini kama jambo lile liko vyengine basi serikali inaweza kuchukua hatua. Lakini kwa sasa serikali imefanya utafiti ule na hakuna tatizo lolote lililotokea katika tafiti zilizoripotiwa.

**UTARATIBU**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Jibu ninalotaka nijibiwe na serikali, ule mradi ulifanyiwa *Evironmental Impact Assessment.*

**Mhe. Naibu Spika:** Ndio wamejibu mara mbili umefanyiwa au hupo Sheikh Saleh, mara mbili umejibiwa! (*Makofi*)

**Mhe. Mwanaid Kassim Mussa:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikamuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu yake mazuri aliyotoa namuuliza mna mashirikiano gani na watu wa Mazingira na Utalii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, nimeeleza kwenye jibu langu mama kuwa lazima tushirikiane na *ZIPA*, Wizara, halafu tushirikiane na Mazingira, halafu na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana kwa pamoja ndio tunatoa maamuzi ya mwekezaji kuweka mradi wake.

**Nam. 68**

**Hatua ya Kuutunza Mji Mkongwe**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza :-

Mji Mkongwe ni kivutio kikubwa cha watalii, lakini unakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa taa katika mitaa ya mji huo.

(a) Je, ni nani mwenye jukumu la kuweka taa hizo kati ya Mamlaka ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa.

(b) Je, Mamlaka ya Mji Mkongwe inazingatia vipi umuhimu wa taa kwa maendeleo ya Zanzibar na usalama kwa wageni na wananchi wanaotumia mji huo.

(c) Pamoja na Mji Mkongwe kupata sifa za dunia lakini majengo ya historia yapo katika hatari ya kutoweka kutokana na kukabiliwa na uchakavu. Je, Mamlaka hii ina mpango gani wa kulinda taswira ya Mji huu wa kihistoria usitoweke.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu :-**
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 68 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kiutaratibu mwenye jukumu la kuweka taa ndani ya Mji ni Baraza la Manispaa, lakini Mamlaka inashirikiana nao.

b) Mamlaka ya Mji Mkongwe inazingatia kwa umuhimu mkubwa wa kuung'anisha Mji huu kwa taa ili wageni wetu waweze kutembea bila ya wasiwasi wowote na watumiaji wengine pia wafaidike na huduma hiyo.

c) Mhe. Naibu Spika, mamlaka ya Mji Mkongwe inaendelea kushauriana na Serikali namna ya kuyakabili majengo yetu pamoja na taasisi nyengine nchini pamoja na jumuiya za Kimataifa ili kuweza kuyahifadhi majengo

yetu. Ili mji huu uwe ni mji wa faida kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa tatizo la taa ni la muda mrefu katika mji huu wa Mji Mkongwe na ndio sura ya mji wetu tunatangaza vipi kwa wageni wanaotembelea Zanzibar. Hilo la kwanza.
Kwa kuwa tatizo la taa linaendelea kuongezeka na wageni kukutwa na vitendo vya kihalifu, ni lini tatizo hilo litaondoka pamoja na barabara ya *Airport* ambayo inatumiwa na viongozi wetu wakuu.

Na vile vile katika jibu lako ukajibu Mhe. Naibu Waziri unasema tatizo la taa ni Mamlaka ya Manispaa ndio inayoshughulikia tatizo hilo. Lakini cha kushangaza Forodhani pale wanasimamia Manispaa lakini mapato yote mnachukua nyinyi, sijui utaweza kuwaeleza vipi wananchi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali suala la taa ni suala ambalo linahusiana na Manispaa lakini kama nilivyoeleza kwamba Mamlaka ya Mji Mkongwe inashirikiana na Manispaa kwa ajili ya kuyashughulikia matatizo hayo ya taa. Kwa hivyo nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu itakaa na Manispaa tuangalie kila pale ambapo pana tatizo la taa ili tuweze kulirekebisha.

Na niseme kwamba tuwahakikishie wale wawekezaji na wageni wote ambao wanaingia nchini, kwamba matatizo hayo tutayarekebisha na si muda mrefu tutakaa pamoja na tutajitahidi kuyarekebisha. Lengo ni kuun'garisha mji wetu kama vile ambavyo inavyostahiki kwa ajili ya usalama wa raia pamoja na wageni wetu kama nilivyoeleza hapo awali.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea nimepata wageni kidogo, lakini kabla ya wageni nina tangazo, tangazo hili nimepewa na Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Zainab kwamba jana alipokwenda kusali msikitini alisahau saa yake, sasa aliyeiona basi amkabidhi Katibu wa Baraza ama ampe mwenyewe.

Baada ya tangazo hilo tuna wageni wa aina mbili. Kwanza tuna wageni wa Mhe. Mohammed Said ambao yeye kaleta timu iliyopanda daraja kwenda daraja la kanda hivi sasa na ina jumla ya watu 28 lakini wakiongozwa na Ndugu Abrahman Mohammed Abdi asimame, huyo ndio *captain* wa timu, akifuatiwa na Ndugu Salmin Ridhwan Khamis yeye Rais wa Timu, akifuatiwa na ndugu Salum Ali Salum Mwenyekiti, akifuatiwa na Ndugu Othman yeye ni kocha wa timu ambaye ndio kaleta matunda hayo, tunakupongeza sana na wale waliobakia wachezaji wote

wasimame kwa jumla mnyanyue na kombe Waheshimiwa walione. Waheshimiwa kombe hilo limeletwa kutoka Jimbo la Mpendae, vijana wamefanya kazi kubwa, kwa hivyo tunawapongeza, ahsanteni kaeni kitako.

Wageni wengine ni wanafunzi waliokuja kujifunza juu ya Baraza letu linavyoendesha na hawa wanatoka Skuli ya Sekondari Mikindani Dole kwa Mhe. Shawana. Jumla ya wanafunzi ni 35 simameni, ahsante kaeni kitako, wakiongozwa na walimu wao wawili. Wa kwanza Mwalim Maulid Ramadhan Khamis asimame na wa pili Mwalim Ali Mohammed Shamis. Kwa hivyo tumeona walimu na wanafunzi wao, karibuni sana kaeni kitako.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tuna wajumbe 10 ambao wanataka kuchangia na tunategemea jioni tumalize bajeti yetu hii, kwa hivyo naomba tusirejee, tujali muda twende kwenye *point* moja kwa moja.
Kwa hivyo tunaanza na mchangiaji wa mwanzo kabisa Mhe. Saleh Nassor Juma, akifuatiwa na Mhe. Mohammed Haji Khalid na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad ajiandae.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, uzima na uwezo wa kuja hapa katika jengo hili.

Pili Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu mtu wa mwanzo kabisa leo hii. Kwa hivyo kwa niaba ya watu wa Wawi na mimi mwenyewe nasema ahsante sana.
Mheshimiwa vile vile nadhani kabla sijaenda kwenye *point* kwanza niipongeze Wizara ya Afya kwa ujumla pamoja na matatizo na mashaka waliyonayo, kwa kweli bidii yao inaonekana, kwa hivyo ninachukua fursa hii nimpongeze Waziri wa Afya Mhe. Rashid Seif Suleiman, vile vile pamoja na matatizo ya fedha na mambo mengine.

Napenda nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na *technical team* yake pale kwa kuweza kutusaidia sana katika kututibu, hususan huyu mkuu wa hapa Mnazi Mmoja na yeye anastahili sifa sana, kwa hivyo ninampongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye *point*. Nchi mbali mbali za magharibi Mhe. Spika, zinatoa kipaumbele sana kwa zile wizara zinazohami uchumi wake kwa mfano wizara zinazoshughulika na sekta za viwanda kule nchi za Ulaya hutengewa bajeti kubwa sana.

Kwa upande wa nchi hizi za ghuba Wizara zinazohusika na mambo ya mafuta na madini huwa zinapewa umuhimu sana katika bajeti ya nchi.
Mhe. Naibu Spika, Zanzibar sisi hatuna mafuta wala hatuna viwanda, *asset* pekee tuliyonayo katika nchi hii Mhe. Naibu Spika, ni sisi walipa kodi wa nchi. Nilidhani Mhe. Spika, kwamba Serikali kama ingekuwa na kipaumbele basi ingekuwa na kipaumbele kwa Wizara hii ya Afya.

Wizara ya Afya nailinganisha na *garage* kwamba ndio inayofanya *service* magari ili yaweze kutembea na kuzalisha mali. Lakini *garage* ya mlipa kodi ni hospitali, sasa ningedhani serikali ya nchi hii Mhe. Naibu Spika, ingetenga karibu asilimia 40 ya bajeti yake katika Wizara hii ya Afya ili kuweza kufanyiwa *service* sisi viumbe tukazalisha mali, hatimaye tukaweza kulipa kodi vizuri kwa Serikali.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba *the whole budget* ya Zanzibar ni bilioni 807, bilioni 807 ndio *the whole budget of islands*, ningelidhani Mheshimiwa angalau asilimia 30 zingetengwa kwa Wizara ya Afya ili ikaweza kututibu vizuri sisi walipa kodi wa nchi hii tukaenda tukalima, tukaenda tukavua, tukaenda kupanda mikarafuu tukafanya ujasiri amali hatimaye tukaweza kulipa ili Serikali ikapata maendeleo na muamala mzuri katika nchi.

Inasikitisha sana, katika hii *the whole budget* bilioni 807 Wizara ya Afya imepewa bilioni 84 *only 10% of the total budget*. Wakati *recommendations* za UN kwa Wizara ya Afya inatakiwa angalau iwe asilimia 20, inasikitisha sana hata katika nchi za Afrika Mashariki Zanzibar ni ya mwisho, yaani wenzetu wana asilimia 15, Kenya asilimia 16 sisi tuna asilimia 10, huku tukiwategemea hawa hawa kulipa kodi, je wananchi wabovu wanalipa kodi vizuri.

Aibu, mtu akiumwa hawezi kufanya kazi, akienda hospitali japo wataalamu tunao kina Dkt. Jamala pale lakini wakiwa hawana vifaa hawawezi kututibu hao. Hatuwezi kwenda India sisi wakulima wa nchi hii na wavuvi.
Sasa mimi nilikuwa naiomba tu Serikali kwamba bajeti iangalie umuhimu wa Wizara, na Wizara muhimu katika nchi hii wakati hakuna viwanda wakati hatuna mafuta *asset* yetu ni binadamu. Binadamu afanye kazi alipe kodi, kwa hivyo kuna haja ya kupanua hii bajeti ya Wizara ya Afya.

Baada ya utangulizi huo Mhe. Naibu Spika, niende katika mafao sasa ya hawa watumishi wa Wizara ya Afya.

Mhe. watumishi wa Wizara ya Afya Mheshimiwa wanahitaji wapate motisha katika kufanya kazi zao na kumuhudumia binadamu. Inasikitisha sana kuwa watu wanaoshughulika na makompyuta, wanaoshughulika na mambo ya *internet* wao wanalipwa vizuri sana lakini watu wanaochezea uchafu, wanaochezea taka taka za binadamu, wanaochezea madamu ya binadamu wanao-*risk* maisha yao mafao yao hayaridhishi; kuanzia madaktari bingwa hadi ma-*orderly* ninazungumzia taasisi nzima ya afya.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitembelea siku moja katika hospitali moja hapo Dar es Salaam nikakutana na mama mmoja huyu mama yeye ni *Gynecologist* anapewa *2 million* lakini hapa huyo Mkurugenzi wa Mnazi Mmoja basi haikaribii *2 million* achilia mbali daktari wa kawaida.

Sasa hawa tunawavunja moyo wanatafuta nchi nyengine wanakwenda Afrika Kusini, wengine wanakwenda wapi wanatukimbia wana taaluma. Mimi ninawasifu sana kina Dkt. Jidawi na *technical* timu nzima ya Wizara ya Afya wale mabingwa hukaa pale kututibu kwa kiwango hicho hicho kidogo.

Mimi ninawapongeza, *keep it up!* Ndio uzalendo wenyewe lakini mafao yao ni madogo sana. Nilisahau kumsifu Naibu Waziri kwa kutujibu vizuri, kama kuna kijana anayejibu vizuri maswali humu ndani basi Naibu Waziri wa Afya, mimi ninamsifu sana Mheshimiwa. Huyu kijana ni mtoto wetu tumemzaa sisi na anajibu maswali vizuri sana, na aendelee huyu kijana vizuri na aendelee kutujibu hivi hivi, hongera sana Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, sasa narudi kwenye mafao hayatoshi, kuanzia madaktari bingwa mpaka ma-*orderly* hayatoshi. Daktari bingwa anapokwenda kumtibu mgonjwa tuseme *surgical operation* ana-*risk* maisha yake maradhi ni mengi, pengine mgonjwa yule ana maradhi yanayoambukiza kwa mfano ukimwi na kadhalika anafanyiwa *surgical operation* na daktari bingwa, ikimchuna kidogo kile kimkasi wakati yuko ndani ya *operation* huyo na yeye basi ameshaambukizwa maradhi daktari wetu bingwa. Je, aniambie Waziri wangu wa Afya, ni kwa kiasi gani anatoa mafao haya ya *risk allowances* mbali na mishahara ninazungumzia *risk allowance* kwa hawa madaktari wetu mabingwa walioko katika *surgical operations*, anatoa mafao kiasi gani watu wanao-*risk* maisha yao.

Na si huyu tu akishatibiwa *orderly* anazoa madude yale yaliyofanyiwa *operation* anakamata uchafu uchafu, japo hana elimu naye *orderly* lakini anachezea chezea haya mambo yanaweza yakahatarisha maisha. Leo *orderly* unamlipa shilingi 150,000/= anachezea takataka za mgonjwa wa ukimwi, anachezea takataka za mgonjwa wa kifua kikuu, anachezea takataka za wagonjwa maradhi kibao, kwa sababu hana elimu ndio umlipe laki moja unusu laki mbili, *risk allowance at least*

wapatiwe *risk allowance* na hawa ma-*orderly* hawana elimu lakini jamani wanahitaji msaada hawa, wana-*risk* maisha yao na wao. Wagonjwa wengine wanakuja pale wala hawana watu, wamuoshe, wamsugue wamfanyie kila kitu, leo unamlipa laki moja na nusu *orderly* jamani si kumdhalilisha huko?

Mimi naomba Serikali inieleze ni lini Serikali itawainua mafao hawa ma-*orderly* na wafanyakazi wa chini ya Wizara ya Afya, wana shida ya maisha saa 24 wako pale maharufu. Unapokwenda kumuona anayemshughulikia mgonjwa wa sukari kule kwenye chumba wewe huthubutu kufika, yeye anakwenda anawashughulikia anawaosha anawafanya nini, wewe una mgonjwa wako huthubutu, analipwa kiasi gani *orderly* yule tuelezee laki moja na nusu nini, wanaumwa na kichwa kwa zile harufu tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda umenambia niende haraka haraka nije katika Idara ya Tiba ambayo iko katika ukurasa 15 ambayo inakusanya hospitali ya Chake Chake, Abdalla Mzee, Wete, Micheweni, Vitongoji na Kivunge.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna Idara muhimu inayotakiwa uangalifu wa hali ya juu tena si kwa kuiangalia kwa macho tu mpaka *finacial* ni hii Idara ya Tiba. Hawa kuna haja ya ku-*up* hii ni bajeti yao iinuliwe sana. Kwa sababu umaskini wa nchi ni tatizo nchi yetu maskini, miundombinu ya nchi hii ni tatizo, huu umaskini wa nchi unatoa kazi kubwa kwa Idara ya Tiba ya Wizara hii. Kwa mfano hivi karibuni tunatoka kwenye mvua hizi, mvua hizi mafuriko yalikuwa makubwa mpaka maji yakaingia katika nyumba zetu za makaazi na maji machafu yakaingia, musije mkafiria ni maji ya mvua ni maji machafu.

Sasa kuna tatizo la maradhi yanaitwa *waterbone diseases*, maradhi yanayozaliwa na maji ikiunganisha mambo kama *cholera*, *typhoid*, *schistosomiasis*, *diarrhea, dysentery* hizi ni *waterborne diseases* zinazozaliwa na maji machafu ambayo kwa wingi yameingia katika majumba ya watu mara hii.

Sasa bajeti ya Idara hii ya tiba inatakiwa ipanuliwe sana na iwekwe karibu asilimia kumi *other expenses* kwa ajili ya miripuko ya maradhi. Inasikitisha bajeti yao ni ndogo halafu haina 10% ya *other expenses*, ni tatizo, tutawapa shida sana Katibu Mkuu wetu wa Wizara hii katika kuhudumia miripuko ya maradhi pale yanapokuja hususan katika kipindi hiki cha mambo ya mvua mvua na mafuriko.

Mhe. Naibu Spika, mbali na hilo hospitali zetu kwa mfano naanza na hospitali ya Chake Chake. Hospitali ya Chake Chake Mheshimiwa ni miongoni mwa hospitali muhimu sana katika nchi hii, kwa sababu iko katikati ya Kisiwa cha Pemba ile ni *centre* ya nchi, hospitali iko katika *centre* ya nchi, wagonjwa kutoka Bogoa, wagonjwa kutoka Nanguji, wagonjwa kutoka Kiwani, wagonjwa kutoka Kuukuu,

wagonjwa kutoka sehemu za Kaskazini huku sehemu za Makangale, wagonjwa kutoka Konde wote wale wanaletwa kwanza katika Hospitali ya Chake Chake, inasikitisha sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, hospitali ya Chake Chake ni miongoni mwa hospitali pamoja na kuwa iko katikati hapana benki ya damu pale. Benki ya damu hapana, kwa hiyo ikitakikana damu lazima ikimbiliwe Wete ndio ije pale damu aje atiwe mgonjwa, wakati mgonjwa huyo pengine anatoka huko huko pande za Wete.

Sasa nataka Mhe. Waziri aniambie ni sababu gani za msingi hata pale Chake Chake pakawa hapana benki ya damu, au ni kutokana na kwamba pale Chake Chake ni katikati tu haina umuhimu hii damu. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, hili naomba jibu wakati wagonjwa walioko sehemu mbali mbali wanakuja Chake Chake kwa nini kama benki ya damu iwepo Wete pale Chake Chake isiwepo?

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kwamba Kisiwa cha Pemba na Zanzibar kwa ujumla tunategemea sana, sana uchumi wa karafuu, na lazima mtu apande mikarafuu. Na katika kupanda mikarafuu mara nyengine huwa tunaanguka sana mikarafuu, kiasi ambacho huwa tunapata matatizo makubwa makubwa ya kiafya.

Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine huu utaratibu wa lishe zetu za siku hizi ni wa umasikini, zinatusababisha kufanya mishipa, mishipa zikiwemo ngiri na busha. Sasa inasikitisha sana Mheshimiwa kwamba hospitali ya Chake Chake haina *surgeon;* daktari wa upasuaji huyu Dkt. Shaaban ameshamaliza muda wake kwa taarifa niliyonayo. Kwa hivyo, hakuna daktari wa upasuaji pale Chake Chake huku ukitilia maanani kwamba nimeambiwa mambo ya mishipa yamezidi siku hizi.

Sasa waziri aniambie ni lini hospitali ile tutapatiwa *surgeon,* na kama hakuna daktari wa upasuaji basi yule yule Dkt. Shaabani muongezeeni mkataba aendelee kutupasua mishipa kinyume na hivyo ni tatizo. Mishipa imetuzidi Mheshimiwa ngiri, buhuweti, nini sijui zimetuzidi sana, Dkt. Shaaban alikuwa akijitahidi sana kuicherenga pale, lakini sasa ndio ameshamaliza muda wake, tusaidieni sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nije katika Baraza la Tiba Asili katika ukurasa wa 27. Mheshimiwa kama kuna tiba muhimu sana ambazo nazo zinasaidia saidia kidogo ni hizi tiba za asili, lakini hili Baraza la Tiba Asilia naona haliko makini sana katika ku-*assess* baadhi ya wataalamu hawa wa mambo haya ya kienyeji kiasi ambacho huwa inasababisha wakati mwengine kuhatarisha afya ya mtu badala ya kumtibu.

Napenda niwapongeze wataalamu wengine waliosajiliwa wanajitahidi sana katika suala zima la kututibu katika madawa hayo asilia, wengine wale wamama wajawazito wanawasaidia wake zetu wakati wanapata uchungu. Lakini wengine hawawi *assessed*, hawasajiliwi kiasi ambacho ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, siku za nyuma alikuwepo mganga mmoja wa kienyeji hapa Wawi kwetu huyo lazima akisha kuna kitu kinaitwa nyungu yashi, unawekwa katika *temperature* kubwa sana huku umefunikwa mikeka, wengine siku nyengine walikuwa wanakufa pale pale. Sasa naomba sana wizara katika kuokoa maisha iweze kuwa-*assess* vizuri hawa ili waendelee kututibu katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika Mradi wa Ukimwi katika ukurasa wa 32. Mheshimiwa Mradi wa Ukimwi ni mradi muhimu sana katika kupambana na ukimwi, inajitahidi sana lakini sasa Mheshimiwa kufikia lengo la serikali ambalo siku zote tunaambiwa 03 hazifikiwi katika nchi hii, kwa sababu serikali yenyewe haiko *serious* kutaka kuuondosha huu ukimwi 03 hatufikii.

Mheshimiwa juzi ilikuwa mimi nakuja zangu huku Unguja natoka zangu nyumbani pale Vitongoji kwa bahati hapa Matrekta palilala mwenge, sherehe za mwenge zilifanywa pale Matrekta pale Kilimo. Mheshimiwa kuanzia tangu Msikiti Kibegi hapa niliona mambo ya ajabu sana ambayo hayahitajiki kuonekana kwa macho ya hivi hivi watu kuyaona, basi mimi niliyaona.

Mhe. Naibu Spika, nikajiuliza kuna nini huko mbele kila ninapopita naona mambo ya ajabu, kila ninapopita naona mambo ya ajabu, nikawaambia watoto wanaweza kuchezea kwa bahati yule kijana aliyekuwa ananiendesha akawa ana pauro mle ndani, akawa anaondosha ondosha akitupa pembeni mpaka akachoka yule kijana. Kwa hiyo, ni tatizo Mheshimiwa kuna wale waliotumia hayo mambo lakini kuna wengine hawakutumia katika sherehe ile, basi mimi naona kwamba tupunguzeni baadhi ya sherehe kama unataka tufikie zero, zero ukimwi, zero VVU na zero maambukizi mapya yaani zero tatu basi sherehe kama hizi za kukusanya watu usiku usiku wakicheza ngoma tu pale na wakinywa soda ni tatizo, sherehe za mkesha wa mwenge hizi achilia mbali 03 Mheshimiwa 01 basi hatuifikii, hilo ni tatizo moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tatizo la pili mambo ya mavazi haya nayo ni tatizo. Kweli sisi ni nchi ya demokrasia Mhe. Waziri nashukuru Naibu Waziri yuko makini katika kusikiliza mchango wangu. Mheshimiwa mambo ya mavazi ni tatizo nayo yanaweza yakasaidia mambo ya Ukimwi kuongezeka.

Siku moja nilijibiwa humu na serikali lakini ni Waziri wa Sheria nikajua mambo ya sayansi hayajui, yeye anajua sheria tu na Katiba na nini ama kwa hapo hatari,

lakini ukija mambo ya sayansi hayajui hayo atuachie sisi, sisi hatwendi hata siku moja kukaa uwakili kwa sababu hatujui sheria, hatwendi kumtetea mtu Mahakamani, lakini mambo ya sayansi ndio yetu.

Mhe. Naibu Spika, mavazi ni tatizo na hii Tume ya Ukimwi itapata tatizo sana kwa sababu mavazi ni tatizo, kwa sababu *sexual intercourse* Mhe. Naibu Spika, ni *hormonal controlled, sexual intercourse is a hormonal controlled process,* na *hormones* wanaweza wakafanya kazi kwa kuona tu hivi unamuona mama kavaa kimini pale kwa jicho, basi *sensory nerves ending* za jicho zinapeleka hiyo mpaka kwenye *hypothalamus of the brain,* ukipeleka kwenye *hypothalamus of the brain* zinatoa kitu *releasing factors* ambazo zinakwenda moja kwa moja katika *testosterone,* ambazo zinakwenda moja kwa moja kwenye *reproductive organs* ambapo anasababisha *erection*.

Sasa kama patakuwa na madaktari bingwa mimi sijakaa darasani miaka mingi kusomesha, lakini madaktari bingwa kina Dkt. Jamala wapo hapo haya yakishatokea *testosterone* akishatokea, wewe utataka tu hata kwa kubaka, ikiwa hakukuridhia unaweza ukaenda jela Mheshimiwa kama akili yako haikufanya kazi.

Sasa tatizo hili la mavazi sisi Afro Shirazi enzi ya Mzee Karume ilikuwa hatukubali, ukivaa nguo fupi unapigwa bakora pale pale, lakini sasa ndio kuna utawala bora na demokrasia hamuwezi kuchapa, kwa hiyo tutungieni sheria ya mavazi ili wasiende uchi wanawake hawa.

Mheshimiwa sisi wazee tumeshamalizika lakini kuna vijana sasa, hili ni tatizo. Mimi naishauri serikali Mhe. Naibu Spika, nashukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali ananisikia tuleteeni sheria ya mavazi, japo hatutawapiga bakora kwa sababu utaambiwa mnakiuka haki za binadamu. Lakini tutungieni sheria ya mavazi, mavazi lazima yawe mazuri haya mbona kule Saudi Arabia wazungu wanavaa *mahegals,* kwa nini washindwe hapa kuvaa matenge mpaka humu watuendee vichupi vitupu huko barabarani. Mimi napata tatizo sana katika hii zero ukimwi kufikia ikiwa Mwanasheria Mkuu hujatutungia sheria ya mavazi, hapa ni tatizo sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa niiombe serikali…

**Mhe. Naibu Spika:** Ujali muda bado dakika tano.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika suala la Idara ya Tiba. Mheshimiwa Idara ya Tiba mara nyingi mimi huwa napata shida sana kwamba serikali inatumia pesa nyingi kutibu, hapa tumeondosha *malaria* kwa pesa nyingi sana.

Mimi nilikuwa na wazo Mhe. Naibu Spika, watusikilize wataalamu halafu walifanyie kazi. Hapa kuna tatizo la kichocho, tatizo la kichocho nalo ni *waterborne diseases* ambayo husababisha na hayo hayo maji, *causative agents* wa kichocho *schistosoma jobanicam*, kuna ya tatu ni *schistosoma haematobium* hawa wote hawawezi ku-*exist* kama hawajampata koa ndio wakamuingia binadamu. *Intermediate host* wa *schistosoma* Mhe. Naibu Spika ni koa, *snail*. Sasa mimi nashangaa serikali inafanya kazi kubwa kutumia *chemotherapy treatment* mapesa mengi, kututibu kichocho ambacho hakiondoki na kichocho Mheshimiwa ni tatizo kwa sababu kinaua nguvu kazi ya nchi. Kuna hii *muscular cancer* tunaambiwa kinasababisha zaidi na *Schistosoma haematobium*, ni tatizo sana.

Huyu anaingia vile vile katika mishipa nakusudia misuli anaingia mdudu huyu anaweza akasababisha hata kensa inayosababishwa na kichocho. Kichocho kikishakuwa sugu sana hata kensa inasababisha mbali ya kensa ya kwenye mapitio ya mikojo lakini hata kwenye misuli.

Kwa hivyo, kama hatukuwa makini Mheshimiwa, mimi sijui sana mambo haya lakini najua kwamba kichocho kikiwa sugu sana kinasababisha ugonjwa mkubwa buhuweti na kinaweza kikasababisha hata kensa ya misuli mwilini.
Sasa kuna haja ya kudhibiti mmeshatumia pesa nyingi sana katika kupambana na kichocho serikali haijafanikiwa. Mimi naomba nitoe ushauri kidogo Mheshimiwa katika kutibu.

Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali itumie kitu kinaitwa *predator-prey relationship* kwa kutibu kichocho watu wa *ecology* wanafahamu hata Mhe. Naibu Waziri anajua mambo haya, mwanafunzi wangu huyu. Ni kwamba Mheshimiwa tukitumia *predatora- prey relationship* tunatafuta *natural enemy* wa koa, adui mkubwa wa koa maana tukishamuondosha koa hakuna kichocho. Adui mkubwa wa koa katika nchi hii ni chonjwe ni mnyama mmoja anaitwa chonjwe.

Mhe. Naibu Spika, chonjwe ni adui mkubwa wa koa. Chonjwe mmoja anaweza akateketeza koa 400 kwa saa kwa uchache, sasa tukishamu-*handle* chonjwe na kumpa kazi ya kutuulia koa basi kichocho itakuwa hakuna tena katika nchi hii, tena wala itakuwa hatutumii *chemotherapy* kwamba tutatumia mapesa mengi.

Sasa mimi nashauri serikali itusikilize sisi wataalamu katika mambo ya *ecology* kusudi waweze kutumia *predator-prey relationship for the treatment of*

*schistosomiasis, then chemotherapy treatment* ambayo ni *too expensive* hata Mhe. Waziri anajua.

Kwa hivyo, Mheshimiwa nashukuru sana katika hili, na kwa mnasaba huo basi, ikiwa Mhe. Waziri atutupelekea daktari wa mishipa kule hospitali ya Chake Chake tukaweza kupasuliwa na kutilia maanani huu mradi wangu wa chonjwe katika kudhibiti kichocho, basi nitaunga mkono hoja. Ahsante sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kutoa yangu machache sana kuhusu Wizara hii ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo kufika hapa kuendelea na kazi zetu za kawaida, na nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote wa wizara hii ya afya kwa jinsi wanavyojitahidi katika kufanya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya pamoja na mengi waliyonayo kazi zao kubwa ni mbili ninavyozihisi mimi, ni kutoa elimu ya kinga na hatimaye kutibu. Kwa hivyo, mambo mawili haya ni ya msingi kabisa katika Wizara ya Afya na hili la kinga lingelipewa kipaumbele kwa sababu tunasema kwamba kukinga ni bora kuliko kutibu.

Mhe. Naibu Spika, miaka ya nyuma sana ilikuwa madaktari wa fani mbali mbali. Watu juzi walikuwa wanapita maskuli kutoa elimu mbali mbali za kinga dhidi ya maradhi mbali mbali yaliyokuwepo kwa wakati huo.

Madaktari wa meno ilikuwa wanapita maskuli kuchunguza meno ya wanafunzi, mimi binafsi nilipokuwa mwanafunzi niling'olewa meno mawili. Kwanza si hospitali pale pale skulini pangu nilipokuwa nikisoma niling'olewa meno, kwa sababu madaktari walikuwa na mtindo wakati huo wa kupita na kutoa huduma kwa wanafunzi maskuli mbali mbali. Lakini jinsi maendeleo yanavyokua pia maendeleo yanaongeza matatizo, kwa sababu wakati huo madaktari walikuwa wanapita wanafanya huduma hizi bila ya kutumia umeme, leo huduma zote hizi kama hakuna umeme hazifanyiki.

Sisi hapa kama utazima umeme shughuli zetu zinakatika, hospitali kama hakuna umeme hata sindano hutochomwa, hospitali kama hakuna umeme *operation* haitofanyika kwa sababu haya maendeleo pia baadhi ya wakati yanaleta matatizo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, elimu ya kinga ina umuhimu wake katika Wizara hii ya Afya, kwa sababu unampa elimu mtu ya kujikinga dhidi ya maradhi mbali mbali

hata yale ya kuambukiza namna ya kukaa na mgonjwa mwenye maradhi ya kuambukiza, anapewa elimu ili mwengine maradhi hayo yasimfikie.

Mhe. Naibu Spika, niangalie kidogo mimi katika hii wenyewe waliyoita huduma za afya Wilayani. Mhe. Naibu Spika, hii inaonesha kuwa wana *team* watu wa afya ambazo zinatoa elimu katika Wilaya, zinasaidia matatizo madogo madogo, ujenzi wa uchimbaji wa visima, matengenezo ya nyumba za madaktari na kadhalika, kwa sababu kazi hizi ambazo wanazifanya ni kazi za msingi kabisa, kwa hivyo zinastahiki kupongezwa na waongeze juhudi kutoa elimu hizo.

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna kifungu kilichoelezea kuwa uchunguzi wa maradhi mbali mbali ulifanyika katika siku za maadhimisho ya Siku ya Afya vijijini. Katika maadhimisho hayo jumla ya watu 1,232 walichunguzwa maradhi ya sukari na sindikizo la damu na waliobainika walipatiwa matibabu.

Sasa kati ya watu 1,232 wako waliobainika na hayo magonjwa ambayo walichunguzwa na walisema hao waliobainika walifanyiwa matibabu. Lakini hajatwambia ni wangapi waliobainika. Katika uchunguzi wao huo katika hao watu 1,232 ni wangapi walibainika na hayo matatizo ili tujue asilimia gani ya watu wameathirika na haya magonjwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu magonjwa haya ya kisukari na sindikizo la damu siku hizi yanakua kwa kasi sana, yanaongezeka kweli kweli, nini sababu yake, nini kinachosababisha kwa kweli mimi sijui. Lakini wasiwasi wangu ni huu ustaarabu na utaalamu wetu wa vyakula tunavyotumia.

Mhe. Naibu Spika, tunatia vyakula moto katika *package* za vyakula sijui kuwa karatasi zile zilizotengenezwa haziyayuki zikatoa madini fulani ambayo yanaathiri viwiliwili vyetu. Vyombo vyetu tunavyopikia vyengine vimetengenezwa kwa *aluminium***.** Je, katika *high temperature* vyombo vile haviyayuki kidogo vikasababisha chakula kuchanganyika na madini ambayo hatimaye yanaathiri?

Sisi zamani tulikuwa tunatumia vyombo vya udongo(vyungu) na maradhi haya ilikuwa hayapo kwa wingi, wasiwasi wangu ni kuwa vyombo tunavyotumia pengine vinasababisha baadhi ya maradhi kujitokeza kutokana na vyombo hivyo tunavyotumia katika kutayarisha vyakula vyetu, sio kitaalamu ni wasiwasi wangu. Kwa hivyo, kama ni hivyo tungefanya utafiti na hatimaye tukaona kama ni hivyo tukatafuta vyombo mbadala vya kutumia ili kulinda afya za watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, nitazame Idara ya Tiba. Baada ya mwananchi kuathirika na magonjwa mbali mbali anakimbilia hospitali kupata tiba juu ya yale yaliyomsibu.

Hapa kuna jedwali lililoonesha mahudhurio ya wagonjwa waliolazwa na wagonjwa waliofariki katika hospitali zetu.

Mhe Naibu Spika, katika Hospitali ya Mkoani wagonjwa wa nje waliohudhuria katika kipindi hiki kinachomalizika yaani hadi Machi ya mwaka huu walikuwa ni wanaume 10,795 na wanawake 15,094. Hawa walikuwa ni wagonjwa wa nje yaani waliokwenda kupata matibabu na kurudi nyumbani. Waliolazwa wanaume walikuwa 712 na wanawake 2,384 na waliofariki walikuwa wanaume 49 na wanawake 32.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla hawa watu waliofariki hospitali peke yake kwa Hospitali ya Abdalla Mzee ni karibu watu 81, si watu kidogo sana katika miezi tisa iliyomalizika, si watu kidogo, lakini pia watu hao watakuwa wamefariki kutokana na matatizo ya magonjwa mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunatembea katika miaka karibu 52 ya Mapinduzi yetu na bado tunaagizia madaktari bingwa kutoka nchi mbalimbali duniani, kama katika miaka hii ingekuwa kila mwaka tunafundisha angalau madaktari bingwa wawili wa fani zote; wawili pengine madaktari bingwa wa mambo ya koo, wawili mara 50 tungelipata madaktari bingwa karibu 100. Lakini leo kama tunao madaktari bingwa wazalendo ndio itakuwa ni wachache sana. Je, serikali bado haijaona umuhimu wa kufundisha wazalendo wetu wenyewe na tukaacha huu mtindo wa kusaidiwa au kuagizia madaktari kutoka nje kwa ajili ya kuja kutusaidia kazi za matibabu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kazi hii ya tiba ni ngumu inahitaji uzalendo, inahitaji uvumilivu, inahitaji mtu awe kafaulu vizuri mafunzo ya uuguzi ya mwanzo *nightingale*, ili aweze kutoa huduma bora lazima awe kafaulu vizuri mafunzo ya muuguzi wa mwanzo duniani, *tolerance nightingale* vyenginevyo kama hakufaulu vizuri mgonjwa baada ya kupata lugha nzuri ya kumfanya aone maneno ni sehemu ya tiba, baadhi ya wahudumu wakatoa lugha ya kumvunja moyo ugonjwa wake unaongezeka. Kwa hivyo, ni vyema baadhi ya wale wahudumu ambao huduma zao si nzuri wakapewa elimu ya namna gani kuhudumia wagonjwa,

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na *staff nurse* mmoja alikuwa na *psychology* nzuri sana ya kutibu. Unapoingia pale katika kijiji chetu huko kwetu shamba Kengeja anakuuliza, anakwambia toa macho, toa ulimi, fanya hivi, anaandika, hakwambii nenda dirishani anajua kufungua mtoto wa meza yake pale anakwambia kidonge hiki kitakutibu lakini kula hapa hapa, kwa sababu dirishani dawa hii haipo wewe unafarijika kuwa umepata upendeleo, kumbe ni ile ile ambayo unakwenda kuchukua dirishani. Lakini yale maneno mazuri anayokupa yanakufanya upate imani kwa huyu daktari ni mzuri.

Kwa hivyo, lugha nzuri ya anayetibu ni sehemu ya tiba. Kwa hivyo wale ambao maelezo yao sio mazuri kwa wagonjwa waelimishwe wawe na lugha nzuri, ni wachache wako walio na lugha mbaya, wengi wao wenye lugha nzuri.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze kijana ambaye simjui jina wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Nilikwenda na mgonjwa wangu katika hali ya dharura nikamuona anatoka nikamwambia kijana samahani nina haja na wewe. Bahati nzuri yule kijana mimi hanijui na yeye simjui, akanambia Mzee samahani kidogo nazungumza na huyu kijana hapa. Wakazungumza walipomaliza nikamwambia mimi naomba tuingie katika ofisi yako, tukaingia nikamueleza nimekuja na mgonjwa wangu lakini hali yake ni mbaya naomba msaada wako. Tukazungumza halafu nikamwambia mimi ni Mwakilishi, akanambia ah, basi Mheshimiwa unaniacha nazungumza na yule kijana ningezungumza na wewe mwanzo, nikamwambia aa na yule ana haki ya kumsikiliza kama ningekwambia mwanzo kuwa mimi ni fulani huyu ungelimuacha.

Kwa hivyo, yule kijana nilimwambia maneno hayo baada ya kwisha kunipa huduma ya yule mgonjwa wangu. Kwa hivyo, namsifu sana kuwa aliweza kutoa huduma bila ya upendeleo, kwa sababu ningemtambulisha pengine angeona anamtumikia Mheshimiwa, lakini kama sikumwambia kamwe asingenijua lakini huduma aliyotoa ni nzuri, kwa hivyo nampongeza sana huyo kijana. Ni miongoni mwa watu waliohitimu vizuri mafunzo yao na yeye ni kiongozi, kwa hivyo awafundishe na wale wengine ambao tunawasema sema kuwa lugha zao, huduma zao sio nzuri.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya wagonjwa wanaposhindwa kupata matibabu sawia hapa nchini wanalazimika kupelekwa nje ya nchi na fedha nyingi hutumika. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014 serikali ilitenga shilingi 500 milioni kwa ajili ya kupeleka matibabu nje, lakini fedha iliyotumika ni shilingi 2 bilioni na milioni fulani hivi, lakini iliyotengwa ni shilingi 500 milioni.

Bajeti ya mwaka 2014/2015 tulitenga shilingi 800 milioni kwa matibabu ya nje, lakini zilizotumika ni shilingi 3 bilioni *point something*. Sasa ningeona hawa wataalamu kwa nini hawana mlinganisho, tulitenga 500 milioni tukatumia bilioni mbili, halafu tukatenga 800 tumetumia bilioni tatu, kwa nini wasione kwamba zile 500 milioni zilikuwa kidogo tukatumia bilioni mbili. Halafu kwa nini baada ya kupandisha ikafika kwenye ile bilioni wao wakapandisha kwenye milioni tu, kwa nini ile *raise* yao ikawa ndogo wakijua kwamba wanachotumia ni kingi kuliko kile wanachokipanga? Je hiki kitakachozidi watakivumbua wapi na kilichozidi ni kingi zaidi kuliko kile ambacho walikiandaa, hiki cha ziada ambacho ni kingi kweli kweli Mhe. Waziri wanazipata wapi.

Napongeza kwamba wanapeleka watu kwa kugharamia pesa nyingi lakini wanazivumbua wapi na walichopanga ni kidogo na wanatumia kingi. Ningeomba pale wanapozipata hizi pesa nyingi za kupeleka watu nje nijue zinapotoka. Kwa sababu ni zaidi sana ya kile ambacho wamekiomba kutumia.

Mhe. Naibu Spika, hapa kunaoneshwa habari ya huduma za mama na mtoto kwenye uzazi, pametajwa wanawake wanaokwenda hospitali wanaolazwa, wanaojifungua, wanaokufa na vyenginevyo. Kwa bahati nzuri au bahati mbaya jedwali hili linaonesha kwamba wale ma mama tu katika kipindi hicho ndio waliokufa hakuna mtoto aliyekufa wakati huo kule hospitali? Sisemi kwa nini watoto hawakufa lakini je ni kweli kuwa katika kipindi hicho wazazi walipojifungua waliopata maafa ya kufa ni wale wazazi tu hakuna mtoto na yeye ambaye alipoteza maisha?

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya wakati kuna watoto ambao wanazaliwa hospitali kabla ya ule wakati wake wa miezi tisa, pengine anazaliwa mtoto wa miezi sita au saba ambapo kwa Kiswahili akizaliwa miezi minane haponi, kwa Kiswahili lakini sio kitaalamu, lakini wa miezi sita na saba anaweza akaishi. Lakini kwa sababu hajafikia ule muda halisi wa kuzaliwa je, hospitali zetu wanayo *incubator* ya kumuweka yule mtoto kumlea kumaliza ule muda wake ili halafu ndio atolewe aendelee kuishi kama kawaida?

Kwa sababu anapozaliwa kabla ya wakati pengine kinakuwa ni kitoto kidogo hakijakamilika vizuri, sijui kuwa ile *incubator* ya kumuweka na kumlea kitaalamu na hatimaye kwa vipimo vyao ikifika muda huu tayari miezi imemalizika kama kazaliwa kwa miezi saba akatolewa, ili wakakabidhiwa wazazi wake aendelee katika hali ya kawaida, sijui chombo hiki tunacho. Kama hatuna ningeomba kuwa kitafutwe, ingawaje sisi tuna malalamiko ya fedha, uchumi unakua lakini matumizi yanapungua sijui hizo fedha zinazoongezeka zinakwenda wapi.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mkoani kwa Pemba ni karibu ya kuwa kama Hospitali ya Rufaa. Kwa sababu mara nyengine wagonjwa kutoka Vitongoji wanaletwa Mkoani, kutoka Micheweni wanaletwa Mkoani, takriban Pemba nzima mtu kapata ajali anapelekwa Wete hakuwezekana Chake Chake *final* Mkoani, hakuwezekana kwa Pemba ndio imeshindikana. Lakini pamoja na hali hiyo ya Hospitali ya Mkoani bado inakabiliwa na uchache wa vifaa, ingawaje hivi sasa ile hospitali imevunjwa kwa sababu inajengwa upya, mategemeo yetu pengine ikimalizika inaweza ikawa kweli ni hospitali ya rufaa kwa kule Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wagonjwa kila siku wanaongezeka, ule mrundikano wa wagonjwa katika wodi zetu umekuwa ni mkubwa mno na unatishia amani. Kwa sababu vitanda vinajaa zaidi kwa watoto wanalazwa wawili wawili, wengine

wanapangiwa magodoro chini wanalala wawili wawili, pale kila mmoja kenda na tatizo lake lakini unawarundika watoto wenye matatizo mbali mbali kwenye kitanda kimoja wawili au watatu, hatuoni hapa kama wenye magonjwa ya kuambukiza watarushiana yale magonjwa? Badala ya kwenda pale kutibiwa itakuwa tunawapeleka kwenda kuongeza magonjwa.

Sasa mtindo ule ambao umezoeleka, na kwa kuwa juu ya umasikini wetu tunaridhika kuwa mtoto wangu mimi na mwengine na mwengine, wangu mimi anaharisha mwengine ana pumu wote wanawekwa katika kitanda kimoja, hatuoni kuwa badala ya kutibu tutaongeza magonjwa tutibu jengine ambalo sababu yake ni pale ambapo tumempeleka kutafuta tiba ya huyo mtoto?
Kwa hivyo, ili kukabiliana na hili lazima tatafute njia mbadala lakini kuwarundika wagonjwa wawili katika kitanda kimoja kwa mtazamo wangu mimi si njia bora ya kutibu, si njia bora hata kidogo, lakini ni jambo ambalo ni kawaida kwa sasa na tunalifanya.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kazi hii ya kuhudumia wangonjwa wenye matatizo mbali mbali ni kazi ngumu na kazi ya kijasiri, hawa wanaofanya kazi hii lazima ikiwezekana *allowance* fulani ya kazi yao ngumu wanayofanya.

Zamani sisi ulivyokuwa wafanyakazi wa kawaida ile kupewa uhamisho basi unapewa *allowance* ya ile kuhamishwa, unapewa *allowance* ya mazingira magumu huko unakokwenda kutoka nyumbani. Leo hawa wauguzi wetu madaktari wetu sina hakika kama wana *allowance* yoyote wanayopatiwa.

Kwa hivyo, kama haipo ningeomba wizara au serikali kwa ujumla ibuni *allowance* angalau ya kuwafanya waridhike kidogo, uzalendo upo kwa sababu kama si uzalendo wangeliondoka, lakini na nyinyi kama serikali muweze kuwafanya waridhike kwa kima fulani. Kwanza nilitumia na sisi mimi si serikali nikarudia kuwa na nyinyi kama serikali.

**Mhe. Naibu Spika:** Bado dakika tano.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya kama nilivyoanza huku mwanzo jukumu lake ni kubwa, na sijui kwa nini ikawa wizara hii bajeti yake haitononoki, kwa nini wizara hii ambayo inashughulikia na afya ya wananchi wetu ikawa inabanwa banwa katika bajeti zake ili madaktari, *staff* wake, *nurse* na wengine wafanye kazi kazi zao vizuri na wajisikie wapatiwe huduma za kutosha katika mafao yao.

Mhe. Naibu Spika, serikali kwa ujumla nikitaka ione kuwa wanawake, kwanza wanawake wote kwa ujumla wazazi na wao ni sehemu ya madaktari. Kwa sababu

mama mtoto wake mchanga ambaye hata kusema hawezi anaweza akagundua huyu mtoto anaumwa na nini kutokana na mlio wake tu. Mtoto mlio anaolia mama anabaini kuwa kwa mlio huu hichi kitoto changu kinaumwa na tumbo, kwa mlio huu anataka kunyonya, kwa mlio huu sasa hivi hataki nimchukue mimi anamwita dada yake anampa na mtoto ananyamaza! (*Makofi*)

Kwa hivyo, hawa wanahitaji kutizamwa kwa jicho la huruma, kwa sababu mama ni daktari, mama ni mwalimu, mama ni jaji. Kwa hivyo, hawa nikisema hawa nawasema wanawake na wao wanahitaji waingizwe katika fungu la huruma la kuonekana na wao ni *staff nurse.*

Mhe. Naibu Spika, Mzanzibari yeyote ukiacha wanawake naye ni daktari, huyu ni daktari kwa sababu unaweza ukamwambia kuwa unaumwa na tumbo akakwambia katafute dawa fulani. Mimi ni daktari unaweza kunambia naumwa na kichwa nikakwambia kachimbe mzizi wa mtunguja unywe. Kwa hivyo, kila mmoja katika sisi ana fani fulani ya udaktari , lakini fani zetu nyengine si za kitaalamu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya ni wizara muhimu, ni wizara inayohusika na maisha yetu ni wizara ambayo lazima ipatiwe vifaa, madawa na malipo au ile michango ipungue. Kwa sababu bado tangazo la Mzee Karume kama matibabu bure halijafutika. Lakini ukienda hospitali vile vipimo tu mnyonge anaweza akarudi bila ya kutibiwa, unaweza ukaambiwa kuwa ukipima hichi na hichi utatoa shilingi hamsini elfu, huyo anaaga anakwenda zake.

Sasa ile dhana ya matibabu bure  katika awamu hizi zinazoendelea mumeifumbata, mmeificha. Hizi huduma za kuchangia ningeomba zipungue. Kwa mfano *CT Scan* ni laki moja na hamsini elfu, wako watu wanaoweza wala msinambie kwetu ni rahisi ukienda kwa wenzetu ni laki mbili, tusilinganishe wenzetu na sisi, kila mtu na hali yake.

**Mhe. Naibu Spika:** Malizia.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ukilinganisha kuwa laki moja na hamsini bado rahisi na ukienda Bara ni laki mbili au tatu aah tusilinganishe sisi na wengine, sisi na hali zetu kuna watu wengi kile kipimo wana haja nacho lakini hawamiliki kipimo hicho.

Kwa hivyo, ikiwezekana kuchangia iwepo lakini kima cha kuchangia kipunguzwe ili wanyonge waweze kumudu. Naona taa nyekundu inawaka.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:**Mhe. Naibu Spika, na mimi awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa na afya njema

na kutupa uwezo wa kuwepo katika Baraza hili kwa ajili ya kuzungumza mawili matatu kwa maslahi ya wananchi wetu.

La pili nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia angalau kwa muhtasari hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Aidha nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kukitayarisha kitabu hichi kwa malengo ya kuifikishia ufanisi mzuri Wizara ya Afya katika kipindi hichi cha mwaka 2015/16. Pia nimpongeze kwa uwasilishaji wake mzuri.
Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo niseme kwamba Wizara ya Afya kama lilivyo jina lake Wizara ya Afya lengo kubwa ni kuwafanya wananchi wahusika kuwa na afya nzuri katika viwiliwili vyao ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kitaifa. Kwa hivyo, ni wajibu wa wizara hii kuyatekeleza majukumu yao kwa uhakika kabisa, kwa uwazi na kwa ufanisi wa hali ya juu.

Ni vyema serikali kuhakikisha kwamba inawapatia yale mahitaji yao kwa ukamilifu wake, ili kuweza kukidhi haja ile waliyoikusudia kuwasimamia wananchi kiafya.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 4 wa kitabu hiki *paragraph* ya 3.

Mafanikio ya Sekta ya afya kwa mwaka 2014/15. Mimi mizingumzie mafanikio namba mbili naomba kunukuu:-

> "Kuongeza kwa asilimia ya mama wajawazito wanaojifungua katika vituo vya afya kutoka asilimia 56.1 mwaka 2013 kufikia asilimia 68.3 mwaka 2014".

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo zuri la kufikia mafanikio haya na ndio wito wa serikali kwamba wazazi wanatakiwa wajifungulie katika vituo vya afya na hospitali zetu.
Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa asilimia ya wanaojifungua hospitali imeongezeka kutoka 2013/14 ni kuonesha dhahiri kwamba wananchi wameitikia wito huu kwa asilimia kubwa.

Mhe. Naibu Spika, suala la uzazi ni suala muhimu sana lakini ni suala gumu sana. Tunapotaja uzazi tusiutaje tu katika hali ya kawaida tuuangalie mazingira yake, wazazi wamo humu, wanawake ndio wanaozaa na ndio maana wanawake mara nyingi hukwambia kwamba wewe mwanamme umeumia wapi. Lakini mimi katika

kujifungua najua tabu ambayo naipata, wewe mwanamme kazi yako ni kunipa halafu na mimi ndio naenda mimi kutoa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi kwa masikitiko makubwa nataka nizungumze hapa kwa wale madaktari au wakunga wanaowahudumikia wazazi katika vituo vya afya au hospitali.

Mhe. Naibu Spika, wazazi wetu miongoni mwao wanapata usumbufu mkubwa miongoni mwa wahudumu wa vituo vya afya au hospitali. Mhe. Naibu Spika, wahudumu wetu au madaktari wetu baadhi yao hawana lugha nzuri juu ya wazazi, jamani uzazi ni jambo kubwa na upokeaji wa uzazi ni jambo jengine.
Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe kisa kimoja kilichotokea juzi tarehe 24/5/2015 katika Hospitali ya Muembeladu Waheshimiwa naomba mnisikilize kwa makini sana.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Muembeladu juzi tarehe 24/05/2015 kama kipindi cha saa sita mpaka sita na nusu kuna mzazi fulani alikwenda pale kwa ajili ya kujifungua, hapa huyu mzazi alipata tabu kwa wakunga waliokuwepo zamu wakati ule. Mzazi keshapanda kwenye dungu, mzazi huyu umefika muda wa kujifungua daktari hayupo yupo kwenye meza kando akamwita dokta njoo nataka kujifungua, daktari hata hashughuliki.

Lakini jambo la kusikitisha au jambo la kushangaza zaidi mzazi unafika wakati wa kusukuma anawambia njoo msalie Mtume, basi daktari anasema *Salallahu alayhi wasallam.* Ndio kawaida ya waislamu unapoambiwa salia mtume unasema *Salallahu alayhi wasallam.* Mzazi huyu Mheshimiwa kwa masikitiko makubwa, na kwa uzembe wa daktari aliyekuwepo wakati ule alijifungua peke yake daktari anamuona yuko kwenye meza mtoto kaanguka, kizaliwa kitoto kichanga. *Innaa lillaahi wainnaa ilayhi raajiun!*

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo, na baada ya kuanguka mtoto ndio daktari akakurupuka akaenda kumuokota aah hata huyu mtoto wako hajaumia, unamwambia mzazi mtoto wake hajaumia ambaye kaanguka kwenye kitanda ambacho sio kidogo na hata kiwe kidogo, Mwenyezi Mungu kajaalia viumbe wake kawagawa katika uzazi, sisi kama wanaadamu lazima tupokeane katika uzazi, ng'ombe, punda, mbuzi hakuna wapokeaji wa ngombe, punda na mbuzi, lakini wapokeaji wa wanadamu ndivyo ilivyo, heshima kubwa ya wapokeaji wanapewa na Mungu.

Kwa hivyo, kazi ya udaktari na kazi ya ualimu ni kazi ya wito malipo yake analipa Mungu. Mkunga yeyote au mtu yeyote anayetoa huduma za kiafya kwa ajili ya kuwahudumia watu anapaswa aelewe kwamba kazi hii ni kazi muhimu, na anapata

thawabu katika kazi yake anayoifanya mbali ya malipo anayolipwa na mshahara anaolipwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hili alitolee ufafanuzi wa kina, kwa sababu mzazi wa mtoto huyu kazungumza na dokta dhamana wa Hospitali ya Muembeladu lakini kufika jioni ya saa 12 mtoto huyu kabadilika rangi Hospitali pale, akapelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja akafariki.

Mhe. Naibu Spika, ni tatizo, na wakunga wengi katika hospitali zetu na vituo vya afya kwa kweli miongoni mwao wanawatesa kwa lugha chafu na kutokuwahudumia wazazi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba daktari wa zamu wa tarehe hii, sitaki kumtaja jina waziri mwenyewe atafanya hiyo kazi, dokta dhamana wa hospitali hii daktari Waziri anajua ni nani anahusika, tunataka tupate maelezo na hili niseme kwamba liwe ni funzo kwa ajili ya wakunga na wauguzi wetu kuwahudumia wazazi katika hospitali.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe faida ya upokezi wakati alipozaliwa Mtume Muhammad (*S.A.W*) waliompokea ni watu wema hata katika vipindi vya kasida wanasema Asia na Mariama ndio waliompokea; ni mama Asia ambaye ana historia kubwa ya Uislamu na Mariam ni mama yake Issa ambaye pia ana historia kubwa ya Uislamu. Ina maana kwamba hawa Mwenyezi Mungu aliwandaa makusudi kwenda kumpokea Mtume. Kwa hivyo, wale wakunga wanaowapokea watu wana heshima kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Wakunga wa kiasili wa zamani wana mabembelezo makubwa sana kwa wanaozaa. Mtu anapoumwa akienda kwa mkunga wa zamani wa asili ambao leo tunataka kwamba wazazi wote waende hospitali. Wakunga wa asili wala lugha nzuri, wana mabembelezo dakika chake tu kuumwa basi hutumwa mtu hebu nenda kwa fulani akakuandikie kombe, pale yule mzazi anapata matumaini, hebu katafute dawa fulani ulete hapa, anapata matumaini. Lakini leo anakwenda mzazi hospitali ni matusi, lugha zisizopendeza, hii si kazi nzuri katika kazi yetu ya udaktari.

Mhe. Mtumwa Kheri wakati alipokuwepo ***backbencher*** hapa katika siku za nyuma alikuwa na lugha anaizungumza mara nyingi nataka niinukuu alikuwa anasema:

> *"Innalmuallima wattwabiiba kilaa humaa layanswahaan idhaa humaa lam yukrama"*

Anazungumza kuhusiana na umuhimu mkubwa wa kazi ya mwalimu pamoja na daktari. Mwalimu kazi yake analea roho ya mwanadamu na daktari kazi yake

analea kiwiliwili cha mwanaadamu. Kwa hivyo, watu wawili hawa ni muhimu sana katika mazingira yetu ya kijamii.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atueleze hatua gani ambazo amezichukua juu ya wakunga hawa waliokuwepo siku ya tarehe 24 wakati wa mchana kwa mzazi huyu ambaye kapoteza mtoto wake na lugha ambazo zinatolewa na baadhi ya wakunga katika mitaa mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika mafanikio hivyo hivyo kwenye nukta ya nne. Inasema;

> "Kukamilika kwa ujenzi wa kazi kwa jengo jipya la utoaji huduma za upasuaji wa maradhi ya mgongo na ubongo katika hospitali yetu hiyo hapo Mnazi Mmoja".

Hapa nilikuwa na swali tu. Je, Mhe. Naibu Spika, upasuaji wa uti wa mgongo na ubongo tunao wataalamu wazalendo, kama tunao wataalamu wazalendo au hatuna wataalamu wazalendo naomba jawabu na kama hatuna Serikali kupitia Wizara ya Afya inajipanga vipi kuliendeleza jengo letu hili kwa mintarafu ya kuwa na wataalamu wazalendo katika hospitali yetu hii.

Mhe. Naibu Spika, nikenda na mafanikio nambari sita, naomba ninukuu linasema, "Kukamilika ujenzi wa majengo mapya ya maabara katika Hospitali za Wete, Chake-Chake na Micheweni". Ni jambo zuri kukamilika kwa ujenzi wa maabara haya, lakini kuna tatizo kubwa la Ofisi ya Wizara ya Afya Pemba. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba tumetengeneza na kukamilika maabara lakini Wizara ya Afya Pemba bado haijakuwa na Ofisi ya kufanyia kazi. Hawa wanapata taabu na wanapata usumbufu mkubwa wa wafanyakazi, kwa sababu Ofisi yao ipo katika Hospitali ya Wete.

Mwaka jana tulikwenda pale Hospitali ya Wete kuzungumza na viongozi wa Wizara ya Afya Pemba, lakini walisema kwamba wao wameiomba Serikali wapewe lile jengo la Hoteli ya zamani ili lifanyiwe ukarabati iwe Ofisi yao. Sijui Wizara wamelipokea vipi hili na imefikia hatua gani ili na wao hawa wajisikie, yaani pamoja na mafanikio haya lakini changamoto hizi bado zipo.

Mhe. Naibu Spik, nikiendelea na mchango wangu niende katika fanikio la saba ambalo linasema kuanza kwa ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee. Haya ni mafanikio miongoni mwa mafanikio mazuri na kwa kweli kumalizika Hospitali ile ya Abdalla Mzee itakuwa ni hospitali mkombozi kwa watu wa Kisiwa cha Pemba. Lakini jengo mbali na utaalamu na huduma ni kitu chengine.

Je, Mhe. Waziri umejipangaje katika wahudumu na wataalamu baada ya kumalizika kwa jengo lile. Kwa sababu kwa mujibu wa jengo lilivyo na tulivyoliona katika picha ya bajeti yako ya mwaka uliopita, kwa kweli lile jengo litakuwa zuri, kubwa la kisasa lakini linahitaji wataalamu wa kutosha wenye ujuzi na wenye fani mbali mbali. Je, umejipangaje Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika kuhakikisha kwamba jengo lile baada ya kumalizika kwake litafanyiwa kazi kwa ukamilifu na siyo tu kwamba litafanyiwa kazi katika hali ambayo ya kusuasua.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 18, "Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu. Mhe. Naibu Spika, hospitali ile ni muhimu sana kwa Wazanzibari ikiwa kuna sehemu ambayo ni muhimu katika kuwatibu Wazanzibari, basi na Hospitali ile ya Kidongo Chekundu ni miongoni mwa sehemu ambayo muhimu sana. Kwa sababu kama tunavyojua kwamba maradhi tofauti yanakuwepo lakini kukiwepo na maradhi haya ya ugonjwa wa akili. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini pale panahitaji utaalamu, panahitaji wataalamu wa kutosha kwa sababu wagonjwa wa akili tunajua mazingira yao. Mtu anakuwa na mgonjwa wake wa akili nyumbani, ni kumtia pingu na kumfunga kwenye kiguzo kutokana na hasira, uchungu na ukali anaweza hata kuhatarisha maisha. Mwaka juzi mimi nimo katika Kamati ya Ustawi wa Jamii, tumepita pale tukenda katika eneo ambalo wanakaa wale wagonjwa wa akili, tulimkutia daktari mmoja pale mwanamama amechubuka sehemu yake ya shavu karibu na jicho hapa. Mimi binafsi nikamuuliza vipi mama naona hapa umechubuka chubuka vipi. Akaniambia aah! ni miongoni mwa kazi kwa sababu katika kuwaweka sawa hawa vijana kuna mmoja kaniparuzaparuza hapa.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, pale pahali panataka pawezeshwe sana. Kwanza madaktari waliopo pale pamoja na mshahara wao ambao wanapewa lakini waonekana wale kwamba wanafanya kazi katika mazingira makubwa, katika mazingira hatarishi. Je, munawawezesha vipi kwa *allowance* angalau ya kuweza kuwapumzisha na ile kazi na adha wanayoipata pale kwa ajili ya kuwahudumia Wazanzibari wenzetu ambao wanakuwa katika matatizo ya akili. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 33 Kifungu cha 13.34 na ninaomba ninukuu,

"Mhe. Spika, katika kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wanaoishi na *VVU* na Ukimwi jumla ya kliniki 11 zinatoa huduma hii, saba Unguja na nne Pemba. Kuanzia Julai, 2014 hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya wagonjwa 7,820 walikuwa tayari wameshasajiliwa kwenye kliniki hizo. Miongoni mwao wagonjwa

5,375 sawa na asilimia 68.7 walianzishwa dawa za *ARVs* waliobakia kwenye dawa kufikia Machi, 2015 ni wagonjwa 3,585 na wagonjwa 1,788 sawa na asilimia 33 wamekimbia kuchukua dawa".

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme kwamba janga la Ukimwi kwa mtindo huu, kwa kweli ni tatizo hapa Zanzibar. Inaonekana kwamba wagonjwa wa Ukimwi badala ya kupungua wanaongezeka siku hadi siku. Kwa hivyo ipo haja ya Serikali kuwa na miundombinu madhubuti na mikakati madhubuti katika kudhibiti wagonjwa wa Ukimwi pamoja na wale ambao wanaathirika na virusi vya Ukimwi.
Lakini kwa sababu kuna wagonjwa zaidi ya elfu moja, hawa wamekimbia kuchukua dawa. Je, Wizara yako Mhe. Waziri kupitia Kitengo cha Ushauri Nasaha cha Wizara imefanya utaratibu gani wa kutoa ushauri nasaha endelevu ya kutosha juu ya wagonjwa hawa kuchukua dawa hizi ili kuwarefushia maisha.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika Kituo cha Afya Ukutini. Mhe. Naibu Spika, kituo hichi ni kituo ambacho kimejengwa muda mrefu kidogo, ni kituo kikubwa, kizuri na kipo kati kati ya Shehia ya Chambani, Shehia ya Mtangani, Shehia ya Ngwachani. Hichi kituo kipo kati kati kwenye Shehia ya Ukutini.

Mhe. Naibu Spika, kituo hichi matarajio makubwa ilikuwa ni kuzalisha lakini kituo hichi ni muda mrefu imefungwa huduma ya kuzalisha. Je, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ni lini kituo hichi kitafunguliwa kwa ajili ya huduma ya kuzalisha ili kuwapunguzi masafa makubwa wananchi hawa ambao wamekizunguka kituo hichi.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa kuna kituo ambacho kingekuwa na huduma endelevu ni kituo hichi, kwa sababu hata Naibu Waziri katika majibu yake ya ujengaji wa vituo vya afya, amesema kwamba jamani vituo vya afya *alhamdulillahi* Wabunge na Wawakilishi hivi sasa waelekeze nguvu zao katika ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na madaktari.

Kituo cha Afya Ukutini kimejengewa nyumba mbili. Nyumba hizi zipo kwa ajili ya kuchukua wafanyakazi mbali mbali ambao watafanya kazi kituo hichi. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe.Waziri pamoja na yote, lakini kituo hichi kifanye ile kazi hasa ambayo ilikusudiwa ya kuwapunguzi mwendo wa mbali, kuwapunguzia gharama watu wetu ili wazalishwe pale pale Kituo cha Ukutini. Kituo hichi kipo *centre* kabisa, kimezungumzwa na Shehia karibu nne. Ni sababu gani za msingi ambazo zinapelekea kwamba kituo hichi kisifanyiwe utaratibu huu wa kuzalishia watu pale.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika Kituo cha Afya Kojani. Mhe. Naibu Spika, Kojani ni kisiwa, kwa sababu ni kisiwa vile vile kinahitaji kipate huduma maalum. Mhe. Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Kojani ni kizuri lakini masikitiko makubwa ya Kituo cha Afya cha Kojani, kuna nyumba ya madaktari pale, pamoja na maelezo ya Waziri katika kitabu chake kwamba wamefanya matengenezo madogo madogo kwenye baadhi ya vituo vya afya. Amezungumza na hili suala la jengo la Kojani lakini jengo hili bado halifikii kiwango kizuri cha kuweza kuishi madaktari wetu.

Hili jengo linavuja, kuna dari imetoboka kwa sababu ya mvua. Jengo hili kuna mlango Mhe. Waziri kule nyuma umetoka, munakaa watu, madaktari wanawake ni tatizo na mlango ule mpaka tunapita mwaka jana haujaingizwa. Labda nikuombe katika matengenezo haya madogo madogo muliyofanya, kituo kile kimekamilika kwa ajili ya kuweka ule mlango na kuyaziba madirisha yale yaliyo wazi au ukarabati huu ulifanyika miaka mitatu iliyopita. Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, tunawapa taabu sana madaktari wetu ambao wanafanya kazi pale Kituo cha Afya cha Kojani.

Mhe. Naibu Spika, ...

**Mhe. Naibu Spika:** Bado dakika tatu.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** ...ninakushukuru zitanitosha. Kutokana na suala hili naomba tu niseme kwamba Kojani madaktari wetu wanastahiki sana kupongezwa. Kwa nini, wanatoka mbali. Tumekwenda mwaka jana kukiangalia kituo kile, tumesafiri sisi kutoka ng'ambu kuja kisiwa huku, wakati tunatoka kisiwani kuja ng'ambu tulipata misukosuko ya bahari na chombo chetu kwa kweli tulitoka pale sote tumeroa. Ina maana sisi tuliokwenda siku moja tu tumeiona adhabu ile ya bahari. Madaktari hawa wanakuwepo siku zote na wengi wao ni wanawake.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niombe sana Wizara iwaangalie madaktari kuwawekea mazingira mazuri lakini pia wapewe posho maalum kwa ajili ya mazingira magumu wanayofanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, dakika zangu tatu ninafikiri zimemaliza, nishukuru na niunge mkono hoja hii baada tu ya kupewa majibu yangu hasa kuhusiana na wakunga ambao wanawadhalilisha wazazi.

Mwisho, nitoe pole kwa yule mama ambaye mtoto alianguka kwenye dungu na kufariki. Mwenyezi Mungu ampe subra na inshaallah awape subra familia nzima. Assalam Aleykum. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mheshimiwa tunakushukuru. Sasa nafasi ni ya Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi baadae Mhe. Fatma Mbarouk Said na baadae ajiandae Mhe. Hamad Hassan Omar.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kidogo katika hotuba hii.

Kabla ya kuchangia kwanza niseme *Inna Lillahi Wainna Ilih-rajiun*. Kutokana na hotuba ya Mheshimiwa aliyekuwa akichangia hapa kuhusu mtoto aliyefariki katika Hospitali ya Mwembeladu. Niseme nimpe pole mama huyu na pia nimwambie huyu daktari na yeye hakuja tu mzima, lakini na yeye kazaliwa, kapokewa vizuri na ndiyo hatimaye na yeye akafikia hatua hii. Kwa hivyo, na yeye afanye kama alivyofanyia yeye kuwahudumikia wazazi wengine wanaokuja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuingia katika kitabu chako cha Mhe. Waziri hiki. Niseme kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Wake wakiwemo na watendaji wake wote na hususan Katibu Mkuu wa Wizara hii. Katibu ambaye ni mpole, ni mstahamilivu na mnyenyekevu na mtu anayefanya kazi zake kwa bidii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, vile vile kabla ya kuingia kwenye kitabu hichi, naomba wenzangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kitabu nje kinachosema,

> "Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein akijaribu darubini ya kufundishia *(Teaching Microscopy)* wakati alipotembelea kitengo cha maabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja".

Mhe. Naibu Spika, niseme Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ninaamini kwamba hawezi kusahau kazi zake. Huyu ni daktari, bado anazikumbuka kazi zake alizotokea. Kwa hivyo, niwaombe na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na sisi tusidharau kazi zetu. Tunapofanya kazi hii ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaamini kwamba na hatimaye tunaweza tukarudi kwenye ukulima, uvuvi pamoja na ualimu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika kitabu hichi, nije katika Wizara hii ya Afya. Mhe. Naibu Spika, kwenye Wizara hii ina jukumu kubwa sana la kuweza kuhudumikia wananchi wake na wageni wanaoingia katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, hapana budi tumshukuru Mwenyezi Mungu na hatimaye kuishukuru Wizara hii, kwa sababu bila ya afya ya mwilini huwezi kufanya kazi na bila ya afya huwezi kufanya kitu chochote. Kwa hivyo niiombe Serikali iangalie

Wizara hii kwa makini sana na moja kuiongezea fungu bajeti hii kwenye Wizara hii ya Afya. Lakini vile vile kuiongezea fungu maalum au kuitengea fungu maalum ambalo litasaidia Wizara hii hasa ukiangalia ina Vitengo vingi na hivi vyote vinahitaji kuhudumikia watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika ukurasa huu wa 12 unaosema Kitengo cha Kupambana na maradhi ya Kichocho, Minyoo na Matende. Mhe. Naibu Spika, kitengo hichi kinaendelea kutoa huduma na uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa wote wanaosumbuliwa na maradhi ya kichocho na minyoo. Lakini niseme niiombe kwanza nikipongeze hichi kitengo kwa juhudi zake kubwa walizochukua kwa kuwapima wananchi wetu Unguja na Pemba na kutoa idadi ya watu waliochunguzwa na kugunduliwa na maradhi haya Unguja na Pemba, wakiwemo jumla ya watu 3,952 waliochunguzwa na kati yao 1,646 sawa na asilimia 41 waligunduliwa na maradhi ya kichocho Unguja 1,292 na Pemba 354.

Kwanza na mimi niwapongeze zaidi wachunguzi hawa zaidi Kisiwani Pemba kwa kuweza kufanya kazi hii mpaka kufikia hatua ya watu 354. Lakini pia niseme wajitahidi kufanya kazi zao katika Kisiwa cha Unguja na wao ili wapungukiwe hadi asilimia ndogo kama ilivyofikia Pemba.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na uchunguzi huo pia kunahitajika elimu, kwa sababu zipo dawa hizi ambazo zinatolewa kwa watu wetu lakini elimu ni ndogo. Kwa hivyo, niseme kwamba kunahitajika elimu na ufahamu na kuna umuhimu wa zile dawa kutumia, hasa ukiangalia serikali inatumia gharama kubwa ili kuhakisha raia wake wanaepukana na tatizo hili la kichocho. Lakini kutokana na ufahamu mdogo wa wananchi wetu Mhe. Naibu Spika, ndipo wanaposema kwamba dawa hizi tunazokula zinatuharibia uzazi, dawa hizi tunazokula pengine sijui madhara yake ni nini. Sasa kutokana na ile elimu kuwa ni ndogo ya wale watu wetu ndio wanapozungumza maneno hayo.

Kwa hivyo, niiombe serikali kabla ya kutoa zile dawa iwashirikishe Masheha pamoja na Madiwani na kamati zao ziwape elimu kwanza hawa, ili na wao zinapoletwa dawa hizi waweze kuwalimisha wananchi wao.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 13 kifungu cha 4. 8.3 kinasema kwamba;

Kifungu cha 4.8.3

"Katika kuhakikisha kwamba maradhi ya Kichocho yanatoweka ifikapo 2016 kupunguza maambuzo ya maradhi ya minyoo, ulishaji wa dawa kwa lengo la kutibu na kupunguza maambukizo mapya ya maradhi ulifanyika, na jumla ya

walengwa milioni 1,093,004 walitarajiwa kula dawa, kati hao 915,954 walipatiwa dawa hizo"

Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Waziri kwa nini hawa wagonjwa 1,750, kwa nini hawakupatiwa dawa hizo, na kusudio letu ni kuondoa haya maradhi waliyopata, ili na hawa wapate kutibiwa. Kwa nini hawa hawakutibiwa.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi. Kitengo hiki Mhe. Naibu Spika, kinasema kwamba;

"Katika mwaka wa fedha 2014/15 jumla ya watu 6,499 walifanyiwa uchunguzi wa afya za. Wafanyakazi hawa walijumuishwa wafanyakazi wa hoteli, mikahawa, wageni, wafanyakazi wa viwanda, wauza nyama, wauza vyakula na Mashirika ya Umma 1,039 pia walifanyiwa uchunguzi huo".

Niseme tu kwa ufupi Mhe. Naibu Spika.

Je, nimuulize Mhe. Waziri, baada ya kufanyiwa uchunguzi huo wangapi walibainika na maradhi.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 14 kwenye kampeni ya Surua Rubela, kifungu 4.9.5. Mhe. Nabu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje anifafanulie namna ya Surua Rubela siifahamu. Sijui kama kuna wenzangu hawafahamu, ikiwa atatufahamisha nadhani na wenzangu watapata kufahamu.

Pia Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 16 katika kifungu cha 5.1.4 kinachosema;

Kifungu cha 5.1.4

"Damu salama ni muhimu katika kuhuisha afya za wananchi"

Niseme hili ni kweli Mhe. Naibu Spika, kwamba tatizo hili lakini kubwa liko pale katika Hospitali yangu ya Mkoani. Mhe. Naibu Spika, katika Hospitali ya Mkoani kuna tatizo kubwa la uwekaji wa damu salama na hii mgonjwa anapokuja pale ni lazima mpaka damu ifatiliwe Wete na hili ni tatizo kubwa ingawaje tukiangalia hospitali ile ni *temporary*, lakini iko haja ya kuweka damu salama na tatizo la kutokuweka damu pale ni ukosefu wa umeme kuwa ni mdogo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili nilimuuliza katika swali langu, lakini mpaka leo sijahakikisha kwamba pahala pale tayari umeme umeshakuwepo wa kuweka damu hii au ni vipi. Naomba Mhe. Naibu Spika, atakapokuja Mhe. Waziri

aje anieleze vipi tayari umeme uko tayari na damu tayari inawekwa pale. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kuhusu damu salama katika kituo hiki.

Yote hayo Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba ukosefu huu wa kuweka damu salama, kwa bahati watu wetu pale wanaotoa damu, kuna vikundi vinavyotoa damu, kuna watu maalum wanaotoa damu. Hii mimi nafikiria kutokana na kukosekana kutimia ile asilimia inayotakiwa ya damu na hii pia inachangia kutokana na huu uwekaji wa damu, kwa sababu haupo salama pale watu wanashindwa kutoa damu zao.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 19 kifungu cha 7.3, naomba ninukuu kidogo;

Kifungu cha 7.3

"kwa upande wa serikali kuna jumla ya shilingi 800,000,000 zilitengwa hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya shilingi bilioni 1,367,325,561/- sawa na asilimia 49 ndio zilizopatikana".

Mhe. Naibu Spika, niseme je, hii kweli serikali inaisaidia wizara au inazidi kuiporomoa wizara, ikiwa hali ndio kama hii kile kiwango ambacho kimekusudiwa kutimizwa hakikutimia. Je, kweli wizara hii itaweza kufanyakazi zake. Naomba Mhe. Waziri aje anieleze.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nikija katika ukurasa wa 25 unaosema kwamba bodi ya chakula na vipodozi. Mhe. Naibu Spika, ukurasa huu unaeleza kwamba katika utekelezaji wa sheria namba 2 ya chakula, dawa na vipodozi, bodi iligundua jumla ya maeneo 1,304 ya biashara ya chakula, dawa, vipodozi na vifaa vya tiba.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme kitengo hiki kiwaangalie sana hawa wauzaji wa hizi dawa, kwa sababu siku hizi akina mama tumeingiwa na kujipamba, kujipodoa na kujichubua. Sasa kuna wengine wapokwenda pale inakuwa ile dawa au ile *cream* yenyewe haijui kwamba hii inafaa na yule anayeuza hajui kwamba hii ni aina yake ya kuweza kujipodoa mwanamke, yeye anamwambia hii ni nzuri tu, lakini kutokana na elimu hawana basi ni lazima serikali iangalie, hawa wanaouza madawa haya wawe na elimu ya kuwafahamisha mtu anapokwenda kununua dawa zile. Kwa sababu wengine wanakuwa hawajui na dawa nyengine zinaandikwa Kiingereza, wengine hawajui ni lazima wafahamishwe, na yule muuzaji aelewe nauza nini kwa maslahi ya watu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 24, kifungu 11.5 kinasema kwamba;

Kifungu 11.5

"Napenda kuliarifu Baraza hili kwamba wizara kwa kushirikiana na asasi isiyo ya kiserikali ya *Milele Zanzibar Foundation* wizara imeanza ujenzi kwenye vituo vinne ambavyo ni Kinuni, Kiongwe, Bumbwisudi na Ukongoroni".

Mhe. Naibu Spika, kwanza hapa nipongeze. Lakini pamoja na kupongeza, kuna Kituo cha Afya, ambapo kituo hiki nakifahamu tangu sijazaliwa na kuna kituo hiki kuna watu zaidi ya 2,000 karibu 3,000 na wote hutumia kituo hicho. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akakifikiria Kituo kile cha Kangani kujengwa upya, kwa sababu kituo ni kidogo ambacho hakina uwezo wa kuwachukua watu wote hawa. Anakwenda mtu pale kujifungua anashindwa, mpaka mtu yule aingizwe kwenye gari mpaka Hospitali ya Mkoani. Kwa hivyo, namuomba akiangalie kituo kile kwa kujengwa upya.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa katika Kitengo cha Afya Bandarini. Mhe. Naibu Spka, kitengo kinaendelea na kazi ya utoaji wa njanjo kwa wasafiri wa kimataifa. Jumla ya wasafiri 1,052 wamepatiwa chanjo hiyo. Lakini niseme kwamba pamoja na hayo kwanza niwapongeze kwa kufanya kazi zao vizuri, kuweza kuwafanyia chanjo wageni wetu wanaoingia ili kuepukana na maradhi.

Vile vile niseme kwamba pamoja na juhudi zao kubwa wanazochukua kuzuwia hali hiyo, lakini ipo haja hiki kitengo kuwa na maabara ya kisasa ili kuwapimia wagonjwa wetu wanaoingia pale. Kwa mfano, zaidi kwa kwetu sisi kinachotuathiri ni homa ya malaria. Kwa hivyo, naomba kitengo hiki kipatiwe maabara ya kuangalia maradhi haya ya maleria sugu ambayo hapa Zanzibar ni tatizo kubwa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie  na baada ya hapo naomba Mhe. Naibu Spika, uniruhusu ahsante sana nashukuru. *(Makofi)*

Ahsante Mhe. Mwanajuma tunakushukuru umejali muda. Sasa tunampa nafasi Mhe. Fatma Mbarouk Said ujali muda na wewe, baadae Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Mwanaid Kassim Mussa ajitayarishe na Mhe. Salma Mohammed Ali. Dakika kumi.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii nikazungumza machache katika hotuba hii ya waziri Mhe. Rashid Seif Suleiman. Kwanza awali ya yote nimshukuru yeye pamoja na watendaji wake wote, kwa kutuletea bajeti yake hii nzuri na ni bajeti ambayo kama walivyosema wenzangu ni wizara ambayo ina majukumu mazito yanayohusu jamii moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, tunaposimama hapa mara nyingi nia na madhumuni ni kuzisaidia wizara zetu kwa mambo mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, tunaposimama hapa hatuna nia labda ya kuzichagua wizara hizi kwa utendaji wake, lakini ni

jukumu letu kama wawakilishi basi tusimame hapa kuchangia na kutoa changamoto mbali mbali. Aidha, tunasema jambo tunalolileta hapa litakuwani zuri la kufurahisha au litakuwa pengine ni changamoto. Lakini nia na madhumuni ni kukaa pamoja na baadae tukalipatia ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana kwa nia ile ile ya kutengeneza nilisimama mbele ya Baraza lako tukufu, kuchangia bajeti hii hii ya Wizara ya Afya. Nilielezea machache kuhusu mambo ambayo ni mitihani yake Mwenyezi Mungu. Niliondokewa na mtoto wangu wa mwanzo na kwa kweli nilitoa ile historia ya maradhi yake mpaka kufikia kufa kwake. Nimuombe Mwenyezi Mungu aniwezeshe kusema bila ya kutoa chozi, kwa sababu mpaka leo suala hili kwa kweli silisahau.

Lakini nilisema hapa kwa msaada niloupata, lakini labda nilikuwa sikufahamika na baadae nilikuja kupatwa na kadhia nyengine ya kule kule na nilitoa taarifa, sitaki kusema nilimpa nani. Lakini baadae nikaambiwa, "hivyo unataka tena tuje tuuwe". Baada ya hapo kwa kweli nilisikitika sana. Haikuwa nia yangu nililaumu kwamba yule mtoto ameuliwa, nilitoa historia kuwa yule mtoto alitoka mwenyewe kwa miguu yake mpaka hospitali. Siku ya Jumanne alishuka mpaka chini, akazungumza kwamba tunasema kesho atarudi nyumbani, lakini baadae usiku wake alizidiwa yule mtoto, akawa anasema sema maneno ambayo hayatambulikani na kutoa shahada na kila kitu.

Madaktari walisema kwamba huyu mtoto ni lazima atiwe damu, kwa sababu ile ilikuwa ni kesi ya uzazi, alizaa kipindi kirefu lakini kutokana na ku-*bleed* sana, ali-*bleed* miaka yote, kuanzia 2,000 mpaka 2014 ndio yamemtokezea haya baada ya kulazwa hospitali. Maana yake kila nikienda naye hospitali ilikuwa tatizo ni damu, lakini asitiwe damu isipokuwa ale vyakula. Lakini vile vyakula ikawa anakula lakini bado hali haikuwa nzuri na baadae siku ile iliamuliwa kwamba atiwe damu.

Lakini ile damu ikawa ndio tatizo la kifo chake ingawaje *convention* huwa inatokea ukitiwa damu au ukitiwa maji inatokea, lakini baadae akapigwa sindano karibuni mara mbili alipigwa sindano na tokea siku ile yule mtoto kuanzia Jumatano, Alhamis, Ijumaa, Jumamosi, Jumapili mpaka Jumatatu alfajiri alipofariki hakuamka yule mtoto.

Kwa hivyo, nilitoa historia hiyo kwamba niwaweke *attention* madaktari au labda wafanye utafiti ni kitu gani kilitokea, lakini majibu yake yalikuwa ni hayo na nilieleza hapa, lakini baadae nikapata maelezo ya kuwa sipatiwi tena msaada mwingine wowote ambao tunaona humu ndani ni mawaziri na manaibu mawaziri na sote ni wawakilishi. Kwa hivyo, likija jambo kama hilo ni vizuri mkasaidiana.

Vile vile juzi nilipata jengine kuna mjukuu wangu mtoto wa mwanangu. Alikuwa anaharisha kwa bahati akalazwa hospitali kama siku tatu, lakini baada ya siku tatu zile akatolewa tukarudi naye nyumbani. Kwa bahati kwenda kuchukuliwa dawa dirishani baba yake akaambiwa hivi vidonge apewe mtoto yule vitatu. Kwanza yeye mwenyewe mtoaji wa dawa pale kauliza vidonge vitatu, yule baba mtu kwanza akashtuka vidonge vitatu kwa mtoto, kweli atachukua vidonge vitatu. Lakini baadae kurudi tena kwa daktari ikaonekana kwamba ni *over doze* na mtoto keshapewa.

Lakini yote hayo sio kitu, tukarudi tena nyumbani, tukamuona yule mtoto sasa anavimba miguu, mimi nikawa na wasi wasi, nikawaambia sasa huyu mtoto mpelekeni kwa Dkt. Ali Amour aende akaangaliwe zaidi, kwa sababu ilinitia hofu zaidi ile kuvimba miguu, nikasema kutakuwa na *another case*. Lakini baada ya kufika kule akaangaliwa mtoto na akam *check* kila kitu akasema mrudisheni hospitali mwendenae juu. Kwa bahati akapelekwa tena juu akalazwa yule mtoto, lakini baadae wao wenyewe sijui kwa nini inatokezea, tumekwenda pale ndio kama hivyo wanasema dawa hizi ni *over doze* na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, sasa huwa najiuliza kwa nini wao wenyewe pale hospitali wanakuwa hawaaminiani kwamba daktari huyu tuseme kutakuwa na gamba lake ambalo litakuwa linaonesha kila kitu tatizo la huyu mtoto, kwa kweli imenitia hofu kwa hivi namna tunavyokwenda. Madaktari wenyewe hawaaminiani, akiandikiwa hivi anakuambia, kwa nini kaandikiwa hivi, kwa nini kaandikiwa sindano. Sasa kwa nini wao wenyewe hawakubaliani pale hospitali, hivi kuna tatizo gani. Maana yake mtoto kaandikiwa sindano, anakuuliza huyu kaandikiwa na nani sindano. Kwa hivyo, hili ni tatizo katika hospitali yetu.

Lakini vile vile niende kwenye wodi ya mama wajawazito. Mimi nasema kama walivyosema wenzangu, ninapokwenda pahala mimi huwa sipendi sana kujitambulisha na kwa sababu najua kwamba kila mtu ana haki pale. Nikienda kwenye wodi ya wazazi pale na hususan saa za kukagua wagonjwa. Mimi namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri na yule mama ambaye katoa namba zake za simu, kwanza nimpongeze kwa jambo kama hilo. Kwa sababu tukienda pale tunaweza kuomba msaada kwake na akatusaidia. Kwa kweli ukifika kwenye wodi ya wazazi kwa sababu mtu anapokuwa na mzazi ile roho yake yote inakuwa haiko hadhiri, kwa sababu mojawapo hapa linaweza kutokea, ama kuzaa salama au kutokuzaa salama, na hayo ni mwenyewe Mwenyezi Mungu, tunasema au kupata mtoto lakini kuna mambo mengine yanakuwa ya uzembe.

Kwa kweli unapofika hospitali ikiwa una mgonjwa wako wa uzazi huku unakuwa akili zako zote hazifanyi kazi, sasa unakuwa na hamu kwamba ukamjue mgonjwa wako. Sasa hapa naomba uandaliwe utaratibu mzuri wa makusudi. Kwa sababu

unaweza kukaa pale saa saba imeshafika ukaambiwa huruhusiwi kwenda ndani utakaa nje kwa muda wote mpaka muda unakuishia hapa hapa.

Kwa hivyo lazima uandaliwe utaratibu mzazi akifika tu basi wale wahusika wa yule mgonjwa basi wapewe angalau kitambulisho na wakifika wasisimame, maana yake kunakuwa na zogo pale mlangoni, zogo linakuwa kubwa wakati wa kuangalia wagonjwa. Umeshafika saa saba kwa nini hakuandaliwi utaratibu, lazima uandaliwe utaratibu kila mtu yupo mlangoni pale unakwenda mkururo wa watu umekaa pale.

Kwa kweli inakuwa ni tatizo, kwa hivyo lazima uandaliwe utaratibu kila mtu anapokwenda pale anakuwa na hofu sijui itakuwaje; kama mtoto kapatikana, mtoto hakupatikana, mama mtu yuko vipi, kila mtu anakuwa na *tension* yake, lazima kuandaliwe utaratibu kwa upande ule pale.

Si tatizo wanaume wasiingie kama kuna tatizo mle ndani, wanawake ndio waingie kama hayo ndio yanatokezea kule chumbani kule na hasa kule kulikokuwa watu bado hawajajifungua, kule tusiwekewe vipingamizi sisi wanawake. Mimi nimeshakwenda kama anavyosema Mhe. Mohammed Mbwana; unakwenda kumkuta mwenyewe mkunga hayupo kabisa pale na wanazaa tukifika pale haya haya tunasaidia. Mimi sijui lakini nimeshaikuta hiyo kesi. Kwamba madaktari wanakuwa hawapo wanastiriwa na wanawake wenziwao, kwa hivyo hilo ni jambo vile vile la kuliona.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kitabu; Mhe. Naibu Spika, kuna kitengo cha lishe Mheshimiwa Waziri alipokuja amesema kwamba Wizara ilifanya utafiti wa hali ya lishe ya watoto chini ya umri wa miaka mitano, matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa hali ya udumavu wa watoto ni asilimia 24.4, uzito pungufu asilimia 13.9 na ukondefu asilimia 7.2.

Mikakati inayoendelea katika kuhakikisha hali halisi ya watoto inaimarika ni pamoja na kutoa elimu juu ya unyonyeshaji bora, kutoa matone ya *vitamin* (a) pamoja na kushajihisha matumizi ya chunvi madinijoto. Hili ni jambo zuri kabisa na nipende tu kumuuliza Mhe. Waziri kulikuwa na uji ule wa lishe ambao watoto walikuwa wanapewa kupitia masheha imefikia wapi, kwa sababu mara nyingi huwa tunaanzisha mambo mazuri lakini baadae tunaacha. Siku nyengine tulikuwa tunaalikwa sisi Wawakilishi tunakwenda lakini hivi sasa tunaona ni kinyaa, hakuna chochote.

Halafu wanasema kwamba kutoa matone *vitamin* (a) sio kama watoto wote sijui wanafanya utafiti gani hasa kuwapa watoto wote *vitamin* (a) na kitu chochote kikizidi mwilini basi kinakuwa kina athari zake. Kwa nini watoto wote wanapewa

*vitamin* (a), mimi kama ni lishe kwa sababu nimesoma mimi *Biology,* sikubahatika tu kwenda mbele na ningekwenda mbele basi ningekuwa Daktari Mkuu, najua *vitamin* (a) ina tatizo gani, na hii *kwashiorkor* au *pleco vitamin* nafikiri ni *vitamin* (d), najua kwamba *kwashiorkor* na *marasmus* ni maradhi ambayo yanaletwa kwa ukosefu wa *vitamin.* Najua si *vitamin* (a) kama huna uoni, sasa hili nauliza utafiti umefanywa na kwa nini wanawapa watoto wote *vitamin* (a) na ndio pale watu wanaposema huko maneno ya pembeni pembeni kwamba watoto wa siku hizi ni watoto wa sindano.

Vitendo vyao vyote vimekuwa vimoja kwa sababu kila kitu wanapewa pamoja. Kwa hivyo ufanywe utafiti kuhusu hili kwamba hii *vitamin* (a) anapewa kila mtoto hatizamwi mwenye *kwashiorkor,* mwenye *marasmus* na *kwashiorkor* hata nywele zake yule mtoto wa kipilipili, lakini hana asili ya uarabu lakini zinakuja zinakuwa hivo, kwa hivyo nasema lazima kufanywe utafiti Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, najua kuna mambo mengine hapa tunafanya wenzetu wanatusikia, siwezi kusema kumwambia Waziri kakurupuka kwa sababu hafanyi peke yake na wala hafanyi yeye, kwa hivyo sisemi kwamba kakurupuka, niseme wazidi kuongeza utaalam na kufanya utafiti zaidi kwa sababu jambo lolote ili lifanikiwe basi ni utafiti zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa wa nane Mhe. Waziri amesema "Kwa mwaka wa fedha 2014/15 kitengo kiliendelea na kazi ya ukaguzi wa wageni wanaoingia nchini, jumla ya wageni waliokaguliwa ni 70,601 kati yao 38,674 hawakuwa na kadi ya chanjo ya Homa ya manjano, ambapo wasafiri 31,718 walitokea maeneo yasiyo hatarishi na 168 walikuwa na sababu za kiafya, wageni 41 walichanjwa hapa hapa nchini".

Mhe. Naibu Spika, hili tatizo kwamba watu mnatathmini nyie tu kwamba hawakutoka kwenye eneo lililokuwa hatarishi, wenzetu ukienda pale Oman, ukienda pale pale *airport* unatolewa damu kutizamwa UKIMWI, Malaria na ukiwa una UKIMWI wala hutoki tena pale wenyewe walivyokuwa *strict* na mambo yao, na ikiwa Malaria utakuja kugongewa mlango kushaingia utakuja kupewa madawa.

Kwa hivyo hili kwa kweli mtu anatoka huko hata ile kadi ya kuchanja hana je, Serikali inachukua hatu gani kwa wageni kama hao ambao wanakuja hawana chanjo, isiwe tu wanapewa pale pale wananunua hilo ni tatizo Mhe. Waziri.

Kuna kitengo hiki cha kupambana na maradhi yasiyoambukizwa na Mhe. Waziri amesema kitengo hiki kilifanya utafiti uliolenga kupima uelewa na mitazamo ya wafanyakazi pamoja na jamii juu ya magonjwa yasiyoambukizwa. Matokeo ya awali ya utafiti huo yanaonesha ni asilimia 26.5 ya wafanyakazi waliohojiwa

hawakuwahi kupata mafunzo yoyote yanayohusiana na magonjwa yasiyoambukizwa. Kati ya watu waliowahi kupata mafunzo asilimia 30.8 waliwahi kufundishwa kuhusu saratani ya shingo ya kizazi, asilimia 34.6 walifundishwa juu ya saratani ya matiti. Aidha, ilibainika kwamba asilimia 50 ya wafanyakazi wanao uwezo wa kuhudumia wagonjwa wa kisukari na shindikizo la damu.

Mhe. Naibu Spika, utafiti ni mzuri na kwa sababu maradhi yapo na hasa haya maradhi mengine ni sugu na kwa kweli hayaambukizi. Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kuna ugonjwa wa miguu watu wengi umewashika kila unayemsikia, katika watu kumi utakaowauliza basi watu wanane watakuwa wanaumwa na miguu na wanaumwa na miguu hatari, hivyo Serikali au Wizara imefanya utafiti juu ya suala hili.

Ni tatizo gani hasa linalowafanya watu wote wanaumwa na miguu. Haiwi ng'ombe wanatizamwa na wanajulikana kama wana tatizo la miguu, sijui midomo sasa litafutwe hilo tatizo la miguu sasa hivi imekuwa tatizo watu wote wamekuwa hawatembei vizuri wanakuwa na matatizo haya ya miguu. Kwa kweli hili ni tatizo kwa sababu sio kwa wazee tu, hata vijana unakuta hilo hilo tatizo.

**Mhe. Naibu Spika:** Malizia.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo Mhe. Waziri amesema katika ukurasa 33 katika kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wanaoishi na VVU na UKIMWI, jumla ya *clinic* 11zinatoa huduma hii; 7 Unguja 4 Pemba. Kuanzia Julai 214 hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya wagonjwa 7,820 walikuwa tayari wameshasajiliwa kwenye *clinic* hizo miongoni mwao wagonjwa 5.375 sawa na asilimia 68.7 walianzishwa dawa za ARV, waliobaki kwenye dawa kufikia Machi, 2015 ni wagonjwa 3,587 na wagonjwa 1,788 asilimia 33.3 wamekimbia kuchukua dawa. Niiulize Serikali Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie Serikali imechukua hatua gani ya wagonjwa hawa waliokimbia dawa na ni athari gani zitatokea.

Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hoja mia kwa mia na nashukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Naibu Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu mdogo sana, alimradi na mimi nimetoa mawazo yangu.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu subuhanahu wataala aliyejinjaalia kuwa katika uzima na afya inaniruhusu ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Vile vile nichukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu Wizara hii Dkt. Jidawi, lakini nisiwe mwizi wa fadhila nimpongeze Mkurugenzi wa Wizara hii kwa kazi yao nzuri wanazozifanya. Tunawapongeza pamoja na watendaji wote kwa ujumla, wanafanya kazi nzuri.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia afya Wizara pia ina mambo mengi na Wizara ambayo ina mambo mengi na ni Wizara ambayo ni kubwa na ina mambo mengi wahudumu wetu wanajitahidi sana kadiri ya uwezo wao, wanafanyakazi kama *team work* na siri ya mafanikio yao ni umoja. Nazungumza hivyo kwa kuwaona kwa dhati kabisa. Mimi ni makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo na Wanawake tumewatembelea hawa, tumewaona jitihada zao wanavyozifanya, wanafanya kazi nzuri ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kama uko nje hujalazwa kule hospitali utasema hakuna wagonjwa na kama uko nje lakini ukienda huko utaona kama kweli kuna kazi. Wagonjwa ni wengi wa maradhi mbali mbali na wanapata huduma, Serikali yetu inajitahidi kadiri ya uwezo iliyowezeshwa na Mwenyezi Mungu.

Katika mchango wangu wa leo utakuwa mfupi sana lakini niende moja kwa moja katika Hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongo Chekundu katika ukurasa wa 18, hospitali ya Kodongo Chekundu imeambiwa ni hospitali ya rufaa ya wagonjwa wa akili, kwa bahati nzuri tumepata kulitembelea jengo lile kama kamati tumeona mengi na tumejifunza mengi.

Kwanza niseme Hospitali ya Kidongo Chekundu jengo lake ni chakavu na la zamani sana zamani, ilikuwa inaitwa jela ya wendawazimu basi ule mjengo wake ni wa kijela jela.

Tunaiomba serikali ifanye marekebisho makubwa sana kwa sababu wanaotibiwa pale ni wagonjwa wa akili na ukiwajengea mazingira mabaya wanazidi kudumaa akili hazifanyi kazi. Tunashukuru wameboresha boresha hata TV zipo pale *alhamdullillahi* kwa jambo hilo, lakini niwapongeze sana Serikali yetu hii jambo moja kubwa wamelifanya pale angalau wanapata mlo kwa siku mara tatu. Hili tunalipongeza. Mgonjwa inafika hadi kashatolewa katika hospitali lakini anarudi pale ikifika muda wa kula anarudi anakula ndio anarudi nyumbani, sasa mazingira kama hayo ndio unawajenga ki *psychology* wale. Hili ni jambo zuri na la faraja, jirani yangu hapa alikuwa anapiga kelele kuhusu na mlo Mhe. Jaku Serikali imeitikia wito wako na wagonjwa wa akili wanapata chakula mara tatu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizunguze hakuna zuri lisilokuwa na kasoro pale pale hali ya afya Kidongo Chekundu si nzuri, hali ya usafi hairidhishi hata kidogo,

ukipita unapita tu kwamba unafanya kazi lakini wale wanaokaa pale muda wote sisi tuliopita tunakwenda kuangalia tunajikamata pua, ni tatizo wale wagonjwa wa akili tunawazidisha akili kudumaa. Nazungumza tena lazima maeneo kama yale yawe safi sana.

Lakini utakuta sehemu kama ile hakuna detol, hakuna *glove* matatizo kabisa wanatwambia wenyewe, lakini kama kwamba haitoshi hata vitanda viliopo pale magodoro yao ni mabaya sana yameisha kabisa, mgonjwa anatwambia tunashukuru angalau vitanda tunavyo vizuri, lakini magodoro baba ni matatizo wale ni binaadamu kama sisi, wanataka waishi vizuri kama sisi haya matatizo aliyowapa Mwenyezi Mungu, wakati wowote Mwenyezi Mungu akitaka kutupa matatizo yale lakini atuepushie mbali, inshaallah tujitahidi kuwapa huduma zilizo nzuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nakuja katika ukurasa wa 17 Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ni hospitali ya rufaa au tunaelekea kuwa ya rufaa, lakini niseme tu ukiangalia hospitali ya rufaa lifti ya mnazi mmoja iko hoi inaweza kufanya kazi mara moja mwezi haifanyi kazi ni tatizo. Naweza kuipiga rangi yote ikapendeza kwa rangi, lakini ikawa mambo hayajakamilika kama haiwi, mgonjwa unabeba unataka kumpandisha juu unabeba kwa machera. Sawa mbebe kwa machera lakini ikifika sehemu mtue lifti ipandishe, bado lifti yetu iko mbaya tunaiomba serikali yetu ilione hilo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tunapozungumza afya kwanza tujali sana usafi, mgonjwa anaweza akenda akakosa dawa lakini akaona mazingira ni mazuri anafarajika kakosa dawa lakini mazingira mazuri, lakini unakwenda pale mahali pachafu na dawa umekosa ni tatizo. Kuna sehemu nyengine Jengo la Mnazi Mmoja lile linavujisha niliwahi kuzungumza hapa, hali sio nzuri hasa katika sehemu ya wagonjwa wa kisukari, kuna matatizo makubwa sana. Hebu angalieni wakati unapopata maradhi ya mripuko wa kipindupindu tunahimiza usafi katika ile kambi inayowekwa au karantini imewekwa. Kitu kikubwa kinachosomeshwa pale ni usafi na mkiyazingatia hayo yale maradhi yanaondoka na maambukizi yanatoka.

Lakini leo ukenda hospitali inakuwa tatizo la usafi halionekani kama muhimu. Nimetembea *Ocean Road* pale, pana wagonjwa wa aina nyingi hasa wagonjwa wa mambo ya kensa haya katika vidonda vyao, ni vidonda vichafu lakini ukenda pale unastarehe kwa usafi walionao, ni kitu ambacho nawapongeza. Wanatupeleka hawa hawa Wizara ya Afya kwenda kujifunza kule, jambo kubwa nililosoma ni hilo. Mheshimiwa usafi ni kutu muhimu sana hasa katika Mahospitali yetu.

Jambo jengine nimegundua ni kauli nzuri ya wahudumu, baadhi ya wahudumu wengine hawana kauli nzuri kwa wateja wao ambao ni wagonjwa, baada ya ugonjwa wanawatia ugonjwa tena kwa kuwapa kauli mbovu. Mhe. Muhammed Mbwana kazungumza sana hapa, kama huyo mama aliyejifungua hapo Mwembeladu anamwita huyo nasi kuja kumsaidia lakini kauli yake kama hiyo. Unamtia ugonjwa unaweza kuchangia mpaka kufikia kufa kwa kauli unazozitoa. Wewe umepelekwa pale, unalipwa mshahara kwa kazi ile , lakini Wallahi unafanya mambo hayaingii akilini.

Mhe. Naibu Spika, naiyomba serikali izingatie mambo haya sana, hakuna hata mtu mmoja anayetaka kwenda pale kulazwa katika sehemu zote hizo, lakini imeshafika Mwenyezi Mungu kakujaalia ni lazima uwende huna budi. Kauli zetu ziwe nzuri wahudumu.

Mimi nadhani wanaelekezwa kwa sababu wanakuwa wana vikao vyao hawa wa kuelimishana, lakini mtu anaweza kuwa mkaidi, mtu kama huyu achukuliwe hatua za kisheria si mtu mzuri huyu, anawaharibia hata wenzake, wenzake wana nia njema lakini yeye anafanya mambo kwa mkakati mchafu haipendezi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika mchango wangu katika vituo vyetu vya afya, Zanzibar tunamshukuru Mwenyezi Mungu tuna vituo vingi vya afya. Lakini katika vituo hivyo kuna changamoto nyingi.

Kwanza siku hizi unapata dawa kwa mujibu wa mahitaji unayotaka wewe mwenyewe katika kituo. Unataka mahitaji unaagiza kwa mahitaji yako unayoyataka katika kituo chako. Lakini pamoja unataka mahitaji ili upate dawa katika kituo chao kwa makisio hayo waliyokisia, lakini inafika kituo kinakuwa miezi mitatu hakipati hata dawa ya *aspirin* ni matatizo.

Mtu anasema mahitaji yangu ni haya, lakini unakuta kituo hakina dawa, kwa nini na mimi nimepeleka bajeti yangu ya matumizi ya dawa. Tujiulize hapa, hebu tuelekeze Waziri atakapokuja hapa atufafanulie vizuri Wajumbe wako wapate faida na wananchi wetu kwa ujumla wapate kulijua hili jambo.

Kama haitoshi Mhe. Naibu Spika, katika vituo vyetu hivi tuna zana nzuri za kufanyia kazi lakini hazina wataalamu kabisa, zana zile zinaweza zikaoza pale pale hazijafanya kazi hata siku moja. Kwa mfano kama Kituo cha Hospitali ya Kojani ni kizuri, tuna mashine ya kung'olea meno haina mtaalamu ingawa tunaambiwa wataalamu hawa ni kidogo sana. Lakini kwa nini hatuwasomeshi tukapata wataalamu. Hili ni tatizo, mashine ipo itaishia pale pale na mamilioni ya fedha yametumika. Tunaambiwa daktari mmoja ndio akang'oe meno huku, siku nyengine ndio anapelekwa huko mwezi sijui mara ngapi.

Kituo cha Wesha kule ipo mashine kama hiyo nacho hakina mtaalamu vile vile na vituo vyengine ni hivyo hivyo. Kwa hivyo kama wataalamu hawa ni kidogo basi tuwasomesheni ili tupate wataalamu wa kuzifanyia kazi mashine zetu zisiharike ovyo.

Mhe. Naibu wa Spika, kama nilivyosema sitokuwa na mengi lakini ujumbe umefika. Nimalizie kwa kusema kama kituo cha Kojani Kamati yetu hii ilifika ya Afya, kule nyumba ya madaktari ya kituo cha Afya Kojani haipo salama hata mlango haina na paa lote linavujisha. Karibuni watataka kugoma kuondoka pale kwamba na wao wenyewe hawana huduma nzuri. Tunaambiwa kama imakarabatiwa, lakini kilichokarabatiwa mimi sikioni, labda bawaba za mlango na huo mlango wenyewe haupo. Kwa hivyo tunaiyomba serikali izingatie kuwaweka katika mazingira mazuri hawa wahudumu wetu.

Mhe. Naibu Spika, sitaki unipigie kengele baada ya hayo niliyoyaeleza naunga mkono mia juu ya mia hoja za hotuba ya Waziri wetu. Asante sana nakushukuru. (*Makofi*)

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Asante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mchana huu nikawa na afya njema.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza mchango wangu nimpongeze Mhe. Rais kwa uwadilifu na uwongozi wake wenye busara na hekima ambayo imewezesha nchi yetu kuwa katika nchi ya amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Afya Mhe. Rashid Seif Suleiman kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2015/16.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza tena Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba hii, hotuba ambayo kaiwasilisha vizuri tena kaiwasilisha kwa wakati uliokuwa makini.

Pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa mashirikiano yao mazuri pamoja na Waziri wake na kitabu chao cha hotuba leo tumewasilishiwa hapa.

Pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa mashirikiano yao mazuri wanayowapa viongozi wao wa juu na kazi zao zikawa nzuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi kusema kweli nikiwa Mjumbe katika Kamati hii kwa vipindi viwili mfululizo. Kwa hivyo, mimi nimesoma sana kuhusu Wizara ya

Afya. Nikianza na mchango wangu kuhusu Hospitali ya Mnazimmoja, kusema kweli Hospitali hii wamejitahi sana tena sana. Kipindi kilichopita tulikuwa tunapiga kelele sana kuhusu *incinerator* lakini nashukuru Wizara ni sikivu, inasikia na ukiwambia wanafatilia na kazi wanafanya. *Incinerator* ipo na hapa wajumbe sijawasikia kuchangia mara hii kwa sababu ile kazi imetekelezwa.
Niipongeze Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kujiwekea malengo yao na malengo waliyokuwa wamejiwekea wameyatekeleza. Mhe. Naibu Spika, kuna majengo haya mapya, jengo la Mgongo na Ubongo, pia kuwepo na wodi ya wagonjwa mahatuti (ICU). Kusema kweli Hospitali ya Mnazi Mmoja imejitahidi sana kwa kazi hizo walizokuwa wamefanya. Si hayo tu na mengi mazuri wamefanya. Wizara ya Afya wanaoongoza ile Hospitali ni binaadamu, kwa hivyo mapungufu ni lazima hayatokosekana, mapungufu yatakuwepo, lakini wanajitahidi kwa uwezo wao sana kabisa.

Mimi nilivyoanza kuingia mwanzo katika Kamati kusema kweli yale matatizo niliyokuwa nimeyaona na tulivyoenda tena na kila tunapokwenda hatua baada ya hatua kusema kweli zile kazi wanazitekeleza vizuri sana. Lazima anayetenda asifiwe. Jamani Wazira ya Afya nikiwa mimi Mjumbe wa Kamati wanajitahidi.

Nije katika suala la kama alivyozungumza Makamu suala kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja suala la lifty. Mhe. Naibu Spika, ni kweli suala la *lift* ni tatizo, inatengenezwa inaharibika. Lakini tukizingatia ile Hospitali ni ya siku nyingi na lile *lift* linafanyiwa matengenezo lakini ndio *lift* halina uhakika kama litakuwa linafanya kazi zake kwa kila wakati.

Japokuwa kuna matatizo ya akina mama wanaolazwa juu na watoto wao wakiwepo katika wodi ya wazazi chini wanatumia *lift* ile. Lakini tukizingatia kama hospitali ya Mnazi Mmoja wanajitahidi kulifanyia matengenezo lakini ndio tukitizama halichukuwi muda mrefu linaharibika.

Pia Mhe. Naibu Spika, hapo hapo hospitali ya Mnazi Mmoja Katika wodi aliyokuwa anazungumza wanachanganyishwa wagonjwa wa sukari na wanaopata ajali. Kweli pana matatizo lakini kama tukiwa Kamati tayari tumezungumza na uwongozi na uwongozi wamesama watalifanyia kazi, kwa hivyo nawapa hogera sana.

Nikiondoka hapo niende katika hospitali ya Kidongochekundu ambao Wajumbe wenzangu wa Kamati walilizungumza sana. Kwanza hospitali hii niwape pongezi. Kipindi cha nyuma tulichokwenda kwenye Kamati, kweli kulikuwa kuna tatizo la chakula lakini sasa hivi *Alhamdulillahi* chakula kinapatikana kwa muda mzuri tena kinapatikana mara tatu.

Pia hospitali hii inasemwa kwamba haipo katika hali nzuri. Ni kweli lakini jamani wanajitahidi, tofauti nikilinganisha nilipokuwa nakwenda na kila kipindi tunapokuwa tunakwenda kutembelea Hospitali, sasa hivi mabadili yapo, wanastahiki pongezi.

Pia tukizingatia niwape pongezi kuhusu kitengo hichi cha watu wanaotumia madawa ya kulevya ambacho wanashughulikia wao pale. Mhe. Naibu Spika, wanafanya kazi nzuri sana, kama kitabu kilivyojieleza kwamba wamepata wagonjwa waliofika pale wanawake na wanaume na wanawashughukia kikamilifu. Na sisi tulivyokwenda kwenye Kamati tuliwaona wagonjwa wale na kweli mabadiliko yapo, kwa hivyo nawapa hongera sana.

Pia hapo Kidongochekundu pana changamoto ya wataalamu, muda tuliokuwa tumekwenda kipindi cha mwisho walitwambia pale pana wataalamu wawili, kwa hivyo wataalamu katika kitengo hichi hawatoshi. Kwa hivyo naiyomba wizara ijitahidi kuona kwamba wanapatikana wataalamu ili matatizo haya ya kuwa madaktari kidogo yanapungua.

Mhe. Naibu Spika, nikienda niende kwenye Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi. Kwanza nawapa hongera sana kwa kujitahidi kupata jengo lao zuri ambalo jengo hili wanajitosheleza sasa. Hapo nyuma walikuwa wameazimwa jengo sijui linaitwa Ofisi ya Panya, lakini pale wamehama, sasa hivi wapo katika jengo lao zuri, wanastahili sifa. Lakini sasa pana matatizo ya maji, pale maji wananunua. Kwa hivyo hii ni changamoto. Kwa hivyo namuomba Waziri aliangalie, ili kuona pale wanapata kisima ili waondokane na tatizo hili la maji.

Pia namuomba Mhe. Waziri wa Fedha basi na Idara hii waingize kwenye bajeti, kwa sababu hawapati bajeti. Namuomba Mhe. Waziri wa Fedha basi na suala hili aliangalie.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo pia na mimi nigusie kuhusu Hospitali ya Wete, Wizara ya Afya. Kusema kweli Wizara ya Afya Pemba hawana Ofisi, Ofisi yao imo katika Hospitali ya Wete. Kusema kweli pale hawawezi kufanya kazi vizuri wanabanana, yaani hawana nafasi nzuri ya kufanya kazi.

Sisi Kamati tumekwenda pale kama walivyozungumza wenzangu, wametueleza ile hali ya pale na kusema kweli tuliipeleka katika Wizara malalamiko yao na Wizara Katibu alitwambia kwamba ataifatilia. Lakini namuomba Mhe. Waziri atakapokuja basi atueleze wamefikia hatu gani kuhusu yale maombi yao ya kuombe lile eneo la kutaka kujenga Ofisi.

Mhe. Naibu Spika, pia katika changamoto za Wizara ya Afya kuhusu ufinyu wa fedha. Kusema kweli Wizara ya Afya fedha wanazoingiziwa hazitoshi. Kwa hivyo namuomba Waziri Fedha awaone kwa jicho la huruma Wizara ya Afya kwa kuwaongezea bajeti yao. Lakini pia hapo hapo pesa wanazowaingizia hawawaingizii kwa wakati. Kwa maana hiyo yale malengo waliyokuwa wamejipangia hawawezi kuyatekeleza. Kwa hivyo kwa muundo huu wa programu basi tunaomba kipindi hichi wanachoaanza baada ya kupitisha bajeti, pesa ziingizwe kwa wakati hizo walizowapangia ili na wao waweze kufanya kazi zao vizuri. Bila kuingizwa fedha kwa wakati ina maana wanashindwa kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo nawapa hongera sana Wizara ya Afya, kwa kazi zao nzuri wanazifanya, kwa mashirikiano yao mazuri. Kusema kweli kama binaadamu wanastahiki sifa. Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia. (*Makofi*)

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kuniwezesha kusimama hapa na kutoa mchango wangu mdogo tu katika Wizara hii ya Afya. Lakini pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Naomba Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri na Naibu Waziri aliyepita kwa jitihada zao kubwa walizozifanya na kwa kweli maendeleo ya Wizara hii tuliyaona. Lakini na vile vile naomba niwapongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri ambao wamekamata kijiti cha Wizara hii kutoka kwa Waziri aliyepita kwa jitihada wanazofanya. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, huko nyuma tulikotokea matibabu yalikuwa ni tatizo. Lakini hivi sasa japo kama hatujafikia lile lengo lakini kwa kweli wanastahiki sifa wamejitahidi sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu ambao utakuwa ni mdogo sana. Kwa sababu licha ya kuwa tunazungumzia Wizara ya Afya lakini mimi mwenyewe leo afya yangu sio nzuri. Kwa hivyo naomba nianze ukurasa wa 7 kwenye kifungu 4.24 na naomba nikinukuu. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa ametwambia:

"Mafunzo juu ya umuhimu wa kuuza chumvi iliyowekewa madini joto yalitolewa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo 200 kutoka Wilaya zote za kisiwa cha Pemba. Sambamba na hilo ugawaji wa madini joto kwa wakulima wa chumvi ulifanyika ambapo jumla ya kilo 200 zilikabishiwa kwa wakulima hao"

Mhe. Naibu Spika, nafikiri wewe ni shahidi, ni bajeti tatu za mwanzo zilizopita kuingia humu Barazani nilikuwa nikizungumzia suala chumvi, kuwa chumvi haina

wenyewe Wizara ya Afya hawashughuliki, Wizara ya Biashara hawashughuliki, Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanasema sio yao, Wizara ya Kilimo pia wanaicheza mpira.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, mimi nafurahi sana kuwa leo Wizara ya Afya imetia hili. Kwa sababu chumvi tunaona ni jambo dogo, lakini iwapo tutatumia chumvi iliyokuwa haina madini joto, kwanza watoto wetu wadogo akili zao huwa hazipo vizuri. Lakini la pili tunapata ugonjwa wa *goiter*, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ninafikiria pale nilipokuwa ninachangia watu wakiona ni mas-hara lakini bila shaka sasa Serikali imeona Wizara ya Afya wametoa elimu na hata kusaidia katika hayo madini joto. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba niipongeze Wizara ya Afya kwanza kwa hilo.

Pia niendelee kuchangia katika ukurasa wa 13 kifungu 4.93 pale Mhe. Waziri alipotwambia kama shughuli zilizofanyika lakini naomba niende hapa mbele katika kifungu hicho imeanza wakati huo matengenezo madogo madogo yaliyofanyika kwa nyumba za madaktari Kojani. Mhe. Naibu Spika, hapa namuomba Mhe. Waziri atueleze ni matengenezo gani yaliyofanyika. Kwa sababu nyumba ile mimi nimeishuhudia *hard board* yote mbovu inawezekana ni sababu kuvuja kwa nyumba ile ama ni kwa kuzeeka na pia mlango kama tulivyoeleza hapa na Mhe. Hassan ni mbovu madaktari wale wanaokaa mule wanawake wakitaka kulala mlango unaekewa kinu na waliomo ni wanawake watupu.

Kwa hivyo Mhe. Waziri hapa kutwambia kama matengenezo madogo madogo yamefanyika hatujui ni matengenezo gani ni huo mlango au ni ile *hard board* zinazonin'ginia. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri atueleze hasa nyumba ile imefanyiwa matengenezo gani na aone kama wale watu wamejitolea kukaa katika jumba bovu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi walioko Kisiwa cha Kojani. Kwa hivyo lazima Wizara au Serikali kwa ujumla nayo iwaone iwasaidie.

Mhe. Naibu Spika, na la kusikitisha zaidi wale madaktari wamehamia pale wakikutia limbikizo la deni kubwa la umeme ambalo pia ni tatizo linalowasumbua. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kidogo ufumbuzi wa hili tatizo la umeme wamewasaidia vipi wale madaktari na pia lile jengo wamelitengeza vipi.

Mhe. Naibu pia naomba niende ukurasa huo huo wa 14 kwenye kifungu 4.94. Hapa naomba pia niipongeze Wizara kuna huduma hapa wanaitoa ambayo wanasema ni huduma za mkoba katika vijiji vilivyo mbali na vituo vya afya. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi hapa ninaipongeza sana Wizara ya Afya kwa kutoa huduma hizi. Kwa sababu kweli kuna vijiji vingi ambavyo mbali na vituo vya afya, halafu pia na wananchi wapo waliokuwa hawajaelimika kwenda katika Vituo vya Afya.

Kwa hivyo hapa naomba niipongeze Wizara ya Afya na hasa pale ilipomalizia kwa kusema kama kuna wananchi ambao walipewa rufaa walionekana na dalili ya saratani za matiti na shingi ya kizazi. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ugonjwa huu sisi wanawake unatuathiri sana, saratani ya matiti na shingo ya kizazi sasa hivi imechukua nguvu na hasa ukizingatia wananchi pengine dalili hawazijui.
Kwa hivyo iwapo hii huduma itaendelea kutolewa bila shaka wananchi watapata kuelimika na watajulikana mapema wale ambao tayari washaanza kuwa na tatizo hili. Naomba hasa Mhe. Waziri watayarishe vipindi katika vyombo vya habari ili kuelezea tatizo hili wananchi wapate kujua zile dalili mapema na waweze kukimbilia hospitali.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo naomba niunganishe katika bajeti ya mwaka jana Mhe. Naibu Spika, niliipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuwa na *mobile clinic* ambayo inapelekwa katika kijiji cha Vikunguni, Mgenikage, Dutani ambapo watu hawa wako mbali na Kituo cha Afya.

Mhe. Naibu Spika, nililichangia hili kwa imani kubwa na kwa kutaka wale wananchi wa kule wafaidike na huduma hii ya afya hasa ukizingatia tayari wameshaanzisha kituo chao lakini hakijamalizika. Pia katika mchango nilijua kama watafaidika wananchi, lakini hata na wale watoa huduma watafaidika kwa sababu watakuwa na pahala pazuri pa kutolea ile huduma.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe masikitiko yangu katika Baraza hili baada ya kuchangia tu ile bajeti wajawazito wale walilolipata ni kuwa wale wahudumu wakenda waliwaambia sasa mtakwenda Gombani ama Chake, kwa sababu Mwakilishi wenu kasema maneno mabaya Barazani. Hivyo kweli Mhe. Naibu Spika, mimi kuna ubaya gani kuwatetea wanawake kuwa wasifanyiwe huduma ile nje waende Kituo cha Afya wapate huduma pahala pazuri. Hata kama ni mwanamme matibabu yanatakiwa yawe pahala siri, leo wale watoa huduma waliona vizuri kwenda kuomba upenu wakatoa huduma ile kama mimi kuwatetea humu Barazani wapate Kituo cha Afya. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, inasikitisha, wajawazito wa vijiji vile mpaka leo wanaenda Gombani au Chake. Kwa sababu eti nilichangia kuwatetea kuwa wapate Kituo cha Afya.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile hili kwa ile nilivyochangia hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliyekuwemo Barazani lilimuathiri sana na akanambia kwa vyovyote itabidi Jumamosi twende tukakiangalie hicho kituo kilichoanzishwa na pahala wanapopimiwa wajawazito. Mhe. Naibu Spika, tulikwenda na Makamu wa Pili wa Rais aliahidi kama kituo kile kitafunguliwa katika sherehe za Mapinduzi yaliyopita.

Mhe. Naibu Spika, nina masikitiko makubwa kituo kile hivi tunavyoelekea ni sherehe ya Mapinduzi nyengine lakini bado hakijafunguliwa. Lakini vile vile kwa kuwaonea huruma wanawake wale niliuliza swali la nyongeza humu Barazani, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri alinijibu kama ni kweli wananchi wengi wana tatizo hili lakini angalau wananchi hawa kuna daladala kuna wengine hakuna hata daladala. Naomba nimueleze Mhe. Naibu Waziri Vikunguni wacha daladala hakuna hata barabara, hivi sasa mvua hizi zote wajawazito wapite mabondeni kwenda kupata huduma hii Gombani. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri anieleze Kituo kile cha Afya cha Vikunguni kitafunguliwa lini.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika ukurasa wa 37 ambapo Mhe. Waziri katueleza kama kuna mradi wa kupandisha hadhi hospitali zetu. Hapa tumeelezwa kama katika hospitali ya Abdalla Mzee na ya Wete zimepandishwa hadhi na zitakuwa hospitali za Mkoa. Mhe. Naibu Spika, naomba hii hadhi inayopandishwa isipandishwe kwa maneno ipandishwe kwa vitendo, zile huduma ziwe zinalingana. Si kwa kuwa tuseme tu kama ni hospitali ya Mkoa lakini ukitizama huduma ziko vile vile lakini Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda naomba niende katika hospitali yangu ya Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, hospitali ya Chake Chake ni hospitali ya Wilaya lakini ni hospitali ambayo kwa Pemba inahudumia wagonjwa wengi. Takwimu zinazoonesha humu wagonjwa wa nje waliohudumiwa katika hospitali ya Chake ni wagonjwa 49,580. Wagonjwa wa Wete ni 45,207, wagonjwa wa Mkoani ni 25,891 na hata wagonjwa waliolazwa hospitali ya Chake ina wagonjwa wengi kuliko hizi hospitali nyengine. Kwa hivyo naomba Wizara iangalie hospitali ya Chake.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kidogo katika wodi ya ugonjwa wa sukari Mnazimmoja, wodi hii kwa kweli ina tatizo la vyoo. Pana vyoo viwili ambavyo vyoo vile vyote ni vya kukaa. Lakini tatizo zaidi liliopo ni kuwa kuna wodi ya *emergency* ya ugonjwa wa matumbo. Sasa tuwatizame wagonjwa wa sukari ambao huchukuliwa hawajiwezi wakawekwa pale kujisaidia na ugonjwa wa matumbo kutumia vyoo vimoja Mhe. Naibu Spika, hii si kuhatarisha afya wale wagonjwa wa sukari tokea hapo afya yao ishakuwa si nzuri halafu tena wanachanganywa kutumia vyoo na wagonjwa wa matumbo. Mhe. Waziri labda atueleze hapa kinga gani inayotokea pale hata wagonjwa wale wakachanganywa kutumia choo kimoja.

Mhe. Naibu Spika, ninamshauri hapa Mhe. Waziri angalau waweke utaratibu choo cha wagonjwa wa matumbo na choo cha wagonjwa wa sukari iwe tofauti au wodi zao ziwe mbali mbali kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sijamaliza lakini unaendelea kunitizama sana kwa hivyo naomba niunge mkono hoja hii nasubiri majibu kutoka kwa Waziri.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nishukuru kwa kupata nafasi hii fupi kwa kutanguliza kumpongeza Mhe. Waziri kwa kusoma kitabu chake vizuri na pengine ni kwa sababu huko nyuma alikuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Afya. Kwa sababu ya wakati mimi yote yale ambayo nichangie itabidi nibadilishe mfumo na ninamuomba Mhe. Waziri anisikilize kwa makini kwa sababu ninalotaka sasa ni maswali na nipate majibu tu.

Nianze na Kitengo cha Afya bandarini ambacho kitengo hiki cha afya bandarini, jukumu kubwa kilichonacho ni kuzuia uingizwaji na usafirishwaji wa maradhi pamoja na wadudu wanaosababisha maradhi kuingia na kutoka nje ya nchi. Hiki kitengo ni muhimu sana na hakuna jambo kubwa na muhimu kama kuona kuwa wote wale wanaoingia kwenye nchi wanachunguzwa kwa maslahi ya afya zao na kwa maslahi yetu. Lakini katika maelezo niliyoyapata katika kitengo, hii ni kuwa tuna jumla ya wagonjwa 70601 ambao hawa walichunguzwa na katika hao kuna wageni 38774 hawakuwa na chanjo ya homa ya manjano. Halafu kuna wageni 31718 walitokea maeneo yasiyo hatarishi. Wageni 168 walikuwa na sababu za kiafya na wageni 41 walichanjwa hapa hapa nchini.

Mimi Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ninavyojua mtu anaposafiri kutoka nje ya nchi kwenda nchi yoyote huwa anachanjwa na anakwenda kule hana maradhi ya kuambukiza na wanaokuja huku ninaamini wanafanyiwa utaratibu huo huo naomba nielewe kwa nini hawa wagonjwa 38,674 hawakuwa na chanjo ya homa ya manjano wakati homa ya manjano nayo ni miongoni ya maradhi ambayo ni mabaya sana.

Vile vile nielewe hawa wagonjwa 168 walikuwa na sababu za kiafya ni zipi sababu za afya hapa sikufahamu Mhe. Waziri alivyoeleza katika kitabu chake na ni sababu zipi zilizowafanya wagonjwa 41 kuchanjwa hapa hapa nchini. Kama nilivyozungumza kusema kuwa mtu anapotaka kusafiri huwa anachanjwa mwanzo kwa maslahi ya afya yake na wenzake kule anakokwenda.

Hapo hapo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya wakati niende katika Idara ya Tiba ambayo hii iko ukurasa wa 15 na ninachokusudia kuzungumza ni kifungu cha 5.13. Idara hii ya Tiba ilifanyiwa uhakiki watu 206 na katika wagonjwa hao 206 kuna wagonjwa ambao walipelekwa nje ya nchi na hawa ni wagonjwa 156. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri na Wizara yake kwa juhudi wanayoichukua kuona kwa yale maradhi ambayo hayawezi kutibika hapa wanafanya kila inavyowezekana ili wagonjwa wale wapelekwe nchi za nje watibiwe ili wawe salama katika afya yao.

Mhe. Naibu Spika, hapa wizara ilitengewa shilingi milioni 800 kwa kusafirisha wagonjwa nje lakini wizara hii ilitumia jumla ya shilingi bilioni 3,231,526,142/40

ni sawa sawa na kusema kuwa kuna jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 2,431,526,142/40 walizitafuta kwa njia yao wenyewe ninawapongeza sana kwa hili kuona kuwa kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa uhai wa mgonjwa unapatikana kuliko kumwachia akafa bure.
Sasa mimi ninavyojua wizara hii hasa katika kipindi hiki kilichopita haikuingiziwa fedha za kutosha na imetumia pesa kama nilivyozitaja hizo bilioni 2,431,526, 142/40 kwa kusafirisha wagonjwa katika njia zao wenyewe. Nikitaka nijuwe fedha hii waliikopa kutoka wapi, kulitokea wafadhili na kama ilitumika kama ni fedha katika bajeti yao athari iliyojitokeza katika mfumo mzima wa uendeshaji katika wizara kwa kuafu maisha ya watu hawa ulikuwa ni upi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuna bodi hii, kuna bodi ya chakula dawa na vipodozi. Bodi hii katika uchunguzi wa kimaabara imechunguza sampuli 888 na kati ya hizo zikiwemo 792 za chakula, 4 za dawa, 43 za vipodozi na 49 na dawa za miti shamba.

Mimi ningeliomba kujua hizi za chakula ni sampuli za chakula aina gani na aina gani kama itawezekana hivyo na vipodozi na hivyo hivyo dawa za miti shamba. Lakini kwa bahati nzuri jambo linalonitia moyo na ninapongeza na isingeliwezekana kama si kazi nzuri iliyofanywa huko nyuma ni kuona kuwa ni sampuli moja tu nayo ni ya chakula ndio iliyoonekana haifai na nyengine zote zilikuwa zinafaa.

Sasa katika kifungu cha 12.23 ukurasa wa 26 katika kufanya kazi zake jumla ya tani 88.9 zikiwemo 84.9 na bidhaa za chakula, 4 na bidhaa za dawa na vipodozi, hizi zilionekana zina matatizo. Kuna nyengine ziliteketezwa na kuna nyengine zilirejeshwa zinakotoka. Sasa ikiwa hali ni hii vifaa vinavyoingia au vitu vinavyoingia vinakuwa na matatizo kiasi hiki lakini kule kulipatikana sampuli moja tu naomba nichanganyishiwe mambo na kujua ilikuwaje ikawa hakuna lakini sasa ikawa kumbe wanaoingiza wanaingiza vitu ambavyo havimo katika kiwango.

Namalizia programu ya kumalizia malaria. Mhe. Naibu Spika, tumeona kuwa wizara inafanya kazi kuona kuwa hali ya malaria katika nchi inazidi kupungua lakini kwa bahati mbaya kutokana na mazingira yetu na kazi waliyoifanya moja ni kutia dawa kila palipo na maji ya kuulia vidudu vya malaria. Mimi Mheshimiwa naomba kuuliza mambo mawili tu kwa kumaliza wakati, wakati maji yanapotiwa dawa na wananchi wanatumia hasa watoto na ile dawa ni sumu huwa wanaathirika ningeliomba kujua dawa hii inatumika katika kima gani ili isiwe inaleta dhara kwa wale watumizi. Pia kwa sababu nchi yetu ina vidimbwi na maziwa kama Kwerekwe ilivyo na kwa sababu mvua, siku zote zinanyesha na dawa inayotiwa inachujuuka, hivyo kuna sababu zipi hasa za kimsingi kuona kuwa malaria inapungua kutokana na kuwa katika maelezo yaliyofatia huko mbele walipofanya

utafiti kuna maeneo maalum malaria inazidi kujitokeza mara kwa mara. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya wakati nashukuru.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwanza kwa kunipa hii fursa ya kuweza kutoa mchango wangu na mimi, lakini Mhe. Naibu Spika, masikitiko yetu hii bajeti iliwasilishwa jana na jana wamechangia watu wawili tu, sasa leo kama tunapewa dakika kumi kumi kitu ambacho hapa sisi tumekuja kuwakilisha wananchi wetu katika bajeti hii ya serikali. Sasa mimi kama ni dakika kumi Mhe. Naibu Spika, basi nazisamehe nampa huyo mwenzangu, wala asirudi nyuma. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa unaweza ukapeleka kwa maandishi bado muda upo.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii mchana huu. Kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kuwa sote tukiwa katika afya njema mchana huu katika Baraza lako tukufu.

Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri na maelezo yake mazuri, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa mashirikiano yake makubwa na yuko makini kabisa katika Wizara hii ya Afya. Lakini pongezi za Wajumbe wote wa Kamati na Mwenyekiti wa Kamati kwa juhudi zao kubwa waliotuonesha katika ripoti yao waliyotuletea.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile muda ni mdogo nianze haraka haraka katika ukurasa wa 15, kifungu Nam.5.1.3. Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, jumla ya wagonjwa 156 waliothibitishwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi kwa matatibabu zaidi ya bilioni tatu na ushee.

Mhe. Naibu Spika, hizi fedha ni nyingi sana na kwa kweli tuna hali nyingi sana ya kuokoa katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja vifaa na baadhi ya mambo mengi, lakini mimi niseme fedha hizi zinapotea bila ya kiwango kilichokusudiwa. Mhe. Naibu Spika, kiwango kilichokusudiwa ilikuwa ni milioni mia nane, lakini imezidi mpaka bilioni tatu.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hii ni kazi kubwa sana na upotevu mwingi wa fedha kuwapeleka wananchi wetu nje ya nchi ni kitu ambacho hatukiwezi kukifanya hivyo, lakini tunatumia fursa hii kwa kujilazimisha. Mimi nitoe mfano mzuri Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni kumefunguliwa hospitali pale Mjini *Vegor Hospital* iliyofunguliwa na Mhe. Rais juzi juzi. Hospitali ile kweli ina ma-*specialists* ina mambo mengi ya uhodari katika kujua matatizo ya wananchi wetu na wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa wananchi wetu hali zao hospitali ile hawaiwezi kumudu hata kidogo. Mimi juzi juzi nimekwenda kutembelea hospitali ile kwenda kuona niliuliza bei tu nikaambiwa chumba cha *VIP* kulala ni 300,000 kwa siku mbali matibabu. Sasa *ordinary room* ukienda pale ni 120,000 kwa kweli ni fedha nyingi sana, lakini naomba sana Mhe. Naibu Spika tuangalie serikali na wizara tuanze kutoa hii huduma ambayo inaweza kufikia watu wengi, huduma ya bima ili iweze ku-*cover* na nimeenda pale nikaona hali ilivyo na nikauliza wakaniambia bima ya *jubilee* ina-*cover* pale inaweza kusaidia kwa kutibiwa.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, tuangalie suala la bima kwa ajili ya wananchi wetu, ili waweze kukimu yale mahitaji yao, fedha ni nyingi sana unaweza kutumia pale na wananchi wetu ni masikini sana.

Mhe. Naibu Spika, niendelee tena katika ukurasa wa 17, nipongeze sana jitihada za serikali kwa kujitahidi sana na nia yake nzuri kwa kuwasaidia wananchi wake kila siku inazidi kuboresha hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya wananchi wetu wanyonge.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa wa 17, kifungu Nam.6.1 kukidhi mahitaji ya wataalamu mbali mbali katika hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa. Mhe. Naibu Spika, wizara imewapeleka masomoni madaktari wawili kwa shahada ya tatu na madaktari saba kwa shahada ya *socialization*, ili wawe madaktari bingwa katika mionzi, *radiology* na matibabu ya macho, mifupa, meno, pua, masikio na koo, maradhi ya akili na upasuaji wa matatizo ya watoto.

Mhe. Naibu Spika, mategemeo ya serikali kuweza kufikia malengo ili hawa wataalamu wetu waweze kutusaidia kwa ajili ya kuwaponesha wananchi wetu kwa maradhi mbali mbali, wanaweza kuwasomesha waweze kuja hapa wafanye kazi. Mhe. Naibu Spika, fedha nyingi inatumia serikali kuwasomesha hawa madaktari mabingwa ili waje hapa wajitolee kwa ajili ya kufanya kazi za nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 38, kifungu Nam. 13.7.1 mafunzo ya udaktari ukiangalia kwenye kitabu inasema nchini Cuba jumla ya madaktari 38 tayari wamehitimu masomo yao na Septemba 2014 wameanza kazi rasmi, na wanafunzi 12 wanaendelea na masomo kwa muda wa miaka sita.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema serikali ina nia njema kabisa kwa kujitahidi kusomesha wananchi wetu ili wawe madaktari wazuri. Mimi niseme Mhe. Naibu Spika, hawa madaktari tutapoenda kuwasomesha nje fedha tutapoteza za walipa kodi, lakini madaktari hawa wakija Zanzibar kufanya kazi ni kwamba hawawezi kufanya kazi pale. Mimi niseme kwa nini hawawezi?

Kwanza ukitizama maslahi yao ni madogo, mishahara yao ni midogo hawawezi kukidhi mahitaji yao, ukitizama daktari bingwa hana gari, ukitizama daktari bingwa huyo nyumba ya kukaa sio makaazi mazuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme na tuliwahi kuzungumza na Waziri wa Fedha tulikuwa *Beijing* tukazungumza suala hili hili kuhusu hawa madaktari wetu mabigwa, mimi nikamwambia Waziri wa Fedha hebu tuangalie serikali iweze kuwakopesha nyumba hawa madaktari, iweze kuwakopesha usafiri kwa mkopo halafu wakatwe kidogo kidogo kupitia Benki yetu ya PBZ. Hawa madaktari bingwa hawatokuwa tena na fursa ya kuondoka kwenda nchi nyengine, watajitolea hapa hapa kwa ajili wana mkopo na maisha yao yatakuwa mazuri wataweza kutusaidia kwa mambo mengi ya maradhi yetu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitoe mfano mmoja mzuri kuna madaktari wengi wamesomeshwa na serikali hii na sasa hivi hawapo wengine wako Dar es Salaam na wako nchi tofauti. Kuna daktari mmoja Dkt. Idrisa hapa siku moja nilimkuta *Aga khan Hospital* pale anafanya kazi, nikamuuliza wewe vipi upo hapa dokta, akaniambia ah Unguja bwana maslahi madogo nimekuja huku kutafuta maslahi.

Ukitizama *private sector* inalipa pesa nzuri kwa madaktari hawa mabigwa wanawachukua na pesa zao nzuri wanawapa nyumba, gari na mshahara. Kwa hivyo, na sisi tuangalie bila ya hivyo tutakosa wataalamu kila siku. Mimi nimpongeze sana, sana Dkt. Ali Amour daktari bingwa wa watoto aliyekuwa yupo mpaka leo pale Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, tuombe Mungu daktari yule asije akaondoka pale, akija kuondoka itakuwa tatizo kubwa kwa watoto wetu maana yake daktari yule mimi mwenyewe kanitibu namshukuru sana na mpaka leo anakwenda Mnazi Mmoja na akitoka pale anakwenda katika hospitali ipo Kilimani wakati jioni, kuanzia saa kumi na moja, anasaidia wananchi wengi, mzalendo, na ana imani na nchi yake hawezi kuondoka naamini. Sasa madaktari kama hawa ni wazalendo lakini hawa vijana wa sasa hivi Mhe. Naibu Spika, hawawezi kufanya kazi kwa mshahara huu kama hawana maslahi mazuri wataondoka tu. Kwa hiyo tutawasomesha kila siku watakuja hapa, watafanya kazi muda wa mwaka mmoja wataenda sehemu nyengine. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie maslahi yao tuwakopeshe nyumba na gari na maslahi yao yawe mazuri ili waweze kutufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, inabidi nimpongeze Dkt. Jamali amesoma Urusi miaka mingi, dokta mzoefu, dokta mzuri lakini leo yupo Al-Rahma pale anafanya kazi na anatutibu kwa maslahi madogo lakini anasema yeye ameridhika hapa hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme suala jengine kuna hospitali moja ipo hapa inaitwa Mina Hospitali kuna dokta mmoja ni mzuri sana anaitwa Dkt. Ottah,

nafikiri kuna wajumbe wanamjua dokta huyu. Mimi nilikwenda Dar es Salaam kuna siku dokta mmoja anaitwa Shafii akaniambia kama una tatizo la uzazi au tatizo la wanawake muone dokta mmoja anaitwa Dkt. Ottah Zanzibar, huna haja ya kuja huku wewe Dar es Salaam kupoteza pesa usafiri na gharama kubwa, dokta huyu mimi namkubali na dokta mzuri.

Dokta huyu amefanya kazi Ulaya miaka mingi Mhe. Naibu Spika lakini kaja hapa na mimi niliongea nae kwa uzalendo wake amekodi lile jengo, ameweka vifaa lakini anasaidia wananchi na bei yake ni rahisi sio kubwa, lakini changamoto ni vifaa hawezi kununua kwa uzalendo wake mimi nampongeza sana.

Kwa hiyo, naiomba serikali sekta hii binafsi iwasaidie watu kama hawa Mhe. Naibu Spika, itatusaidia kupeleka watu nje kuokoa zile fedha lakini mtu kama huyu inakuwa tushaokoa fedha nyingi. Amesoma kwa fedha zake mwenyewe lakini amekuja mwenyewe kujitolea hapa, kwa kweli mimi nampongeza sana hivyo serikali imsaidie japo kwa vifaa na imuangalie kumuondoshea hata kodi daktari huyu ili aweze kuona zile changamoto zake na serikali inamsaidia na aweze kupewa mikopo au kusaidiwa katika sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitoe mfano mwengine mzuri kabisa, kuna siku nilikuwa Mnazi Mmoja *ICU* kuna mgonjwa wangu amelazwa pale, mtaalamu anatakiwa kuja kumpa ile dawa ya kulala kwa masaa ili afanyiwe *operation*, basi yule mtaalamu anakaa jimboni kwangu Bububu kule. Sasa nikaambiwa daktari huyu yupo kule kwa hivyo aje, yule daktari Mhe. Naibu Spika basi alipanda daladala mpaka pale hospitali akaja tumechukua karibu saa nzima tunamsubiri daktari yule aje ku-*mix* ile dawa tu ili yule mgonjwa alale na afanyiwe *operation*.

Sasa Mheshimiwa jambo hili kwa kweli linasikitisha sana, nikamuuliza daktari wewe unakaa jimboni kwangu, una usafiri akaniambia sina nimekuja kwa daladala Mheshimiwa, nikamwambia duh pole sana, ungeniambia mimi ninayo ambulance yangu pale KMKM hospitali ingekuleta mpaka hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme jambo jengine hili suala la *ambulance* ukitizama baadhi ya majimbo kama matatu, manne kwa Zanzibar, lakini nataka kumuuliza Mhe. Waziri kajipanga vipi kuwa ana *ambulance* ngapi pale Mnazi Mmoja maana yake pale akifika mgonjwa Mnazi Mmoja hatuoni *reaction* yake kama atarejeshwa au atakuja kuchukuliwa kwenye jimbo langu. Mimi sijawahi kuona *ambulance* ya serikali iliyokuja pale kumchukua mwananchi wa jimbo langu, hamna. Ile *ambulance* moja tu inafanya kazi usiku na mchana kupeleka wagonjwa.

Namshukuru sana mfanyabiashara mmoja anaitwa Jeff na nitamsema, kila siku Mhe. Naibu Spika ananisaidia pesa ya mafuta kila mwezi, anajitolea kusaidia ile

*ambulance* pesa ya mafuta. Mhe. Naibu Spika, namshukuru mfanyabiashara huyu kwa kuweza kuwasaidia wananchi masikini waliokuwa hawana uwezo hata kukodi gari wa kufika hospitali ya Mnazi Mmoja.
Kwa hiyo, namshukuru sana mfanyabiashara huyu na awe na moyo huo huo wa kusaidia na wafanyabiashara wengine naomba sana Mhe. Naibu Spika wajitolee kusaidia masuala kama haya muhimu kwa ajili ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kifungu Nam. 4, niipongeze sana serikali kwa juhudi zake kwa kuanza kazi kwa jengo jipya la utoaji huduma za upasuaji, maradhi ya uti wa mgogo na ubongo, na jana waheshimiwa wengi wamepongeza hapa na mimi naipongeza sana serikali kwani gharama hii ya matibabu kama utakwenda nchi nyengine kama huna dola elfu kumi basi huwezi kutibiwa maradhi haya. Kwa hiyo, mimi naipongeza serikali kwa juhudi zake kubwa hizo kwa kuona umuhimu huu.

Pia niipongeze kwa ile mashine pale *city scan MRI* kuna siku nilipeleka mgonjwa wangu pale mimi nikalipa laki moja thalathini. Mhe. Naibu Spika, mashine ile ukienda pale Dar es Salaam *Aga khan* unalipishwa laki sita. Kwa hiyo, mimi niipongeze serikali sana kwa juhudi zake hizo kwa ile mashine kwa ajili ya kusaidia wananchi wetu masikini na wanyonge kwa hiyo gharama ile ya laki moja thalathini kuchangia, sio pesa nyingi sana kwa mashine ile kwani ina umuhimu wake na uzuri wake.

Vile vile niendelee katika kifungu Nam.5 kukamilika kwa ujenzi wa wodi ya wagonjwa mahututi *ICU* katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Hilo jambo ni zuri sana na mimi naipongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi niipongeze sana serikali kwa juhudi zake kubwa na niwapongeze sana wafadhili wetu, lakini nimpongeze sana Rais wetu wa Zanzibar kwa juhudi zake kwa kudumisha amani na utulivu wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme bila ya amani hatutopata maendeleo katika nchi hii, na sisi wenyewe kwa vile uchumi wetu ni mdogo bila ya kupata wafadhili na washirika wa maendeleo tutashindwa kujikomboa katika matatizo yetu hasa katika sekta hii ya afya, elimu, barabara, maji safi na salama tutashindwa. Lakini niwapongeze sana hawa washiriki wa maendeleo. Niipongeze sana wizara pamoja na serikali kwa nia yake njema kabisa kwa kujitahidi kufanya mambo muhimu sana katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme wizara imetiliana saini na Kampuni ya *Rans* kwa kuanza ujenzi wa jengo la watoto chini ya ufadhili wa Serikali ya Norway. Mhe. Naibu Spika, mimi nipongeze sana wafadhili.

Mhe. Naibu Spika, jengo hilo litakuwa na wodi mbili, maabara ndogo kitengo cha kusafisha damu, matatizo ya figo, chumba cha watoto na wenye mahitaji maalum. Mhe. Naibu Spika, jengo hilo litagharimu karibu Euro milioni na jengo hili litakamilika mwisho mwa mwaka huu 2015, vifaa vya ujenzi gharama yake zaidi ya milioni moja za Marekani. Kwa hivyo, mimi nipongeze sana washirika wa maendeleo hawa kwa kutusaidia ufadhili wao huu kwa mambo haya muhimu kabisa katika hospitali yetu.

Pia niwapongeze na wafadhili hawa wengine katika ukurasa wa 36, kifungu Nam. 13 ujenzi wa jengo la kliniki wodi ya wazazi, chumba cha huduma za dharura, chumba cha upasuaji, wodi ya watoto wachanga, mtambo wa *oxygen* na umeme wa jua. Mhe. Naibu Spika, ujenzi huu utagharimu karibu Euro milioni 9.6. Mimi nipongeze sana wafadhili na serikali kwa ujumla, lakini pesa hizi nusu watatoa wafadhili wetu wa maendeleo watatoa Euro 4.8 na Serikali ya Zanzibar kwa jitihada yake kubwa itatoa Euro 4.8 vile vile. Kwa hivyo, mimi naipongeza sana serikali kwa ufadhili huu pia kwa kuona umuhimu wa kutusaidia katika kuendeleza mambo ya maendeleo hasa katika sekta ya afya.

Mhe. Naibu Spika, nisichukue muda wako mwingi mimi nashukuru sana naipongeza sana wizara, nampongeza sana Naibu Waziri kwa juhudi yake kubwa, nampongeza na Waziri pia kwa mashirikiano yao makubwa, kwa hiyo naomba waendelee ili waisimamie sekta ya afya kwa muda wa miaka mitano ijayo. Naamini tutafika mbali sana na Serikali yetu ya Mapinduzi kwa jitihada yake kubwa. Mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niwashukuru kwa ushirikiano wenu tangu asubuhi mpaka sasa hivi, ratiba yetu imetueleza kwamba tumebaki na wachangiaji watatu. Mchangiaji wa kwanza Mhe. Marina Joel Thomas, atafuatia Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa na tutamalizia na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na kuna mheshimiwa kataka dakika tano pia tutampa yeye Mhe. Abdalla Mohammed na baadae tutamwita Naibu Waziri na baadae Waziri mwenye.

Sasa ninachokiomba kwenu waheshimiwa jioni tunakuwa *quorum* ndogo sana tunaanza saa kumi na moja na watu watano, watu saba wananchi wanatuona si jambo zuri.

Kwa hiyo, tunaomba jioni tufike mapema tusikilize hoja tulizotoa zinavyojibiwa na baadae tupitishe vifungu. Baada ya hayo maelezo niliyotoa naahirisha kikao chetu hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 6:59 mchana Kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya. Pia, napenda kutoa pongezi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake wenye busara na hekima ambao umetuwezesha hata hii leo nchi yetu kuwa katika amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ya Afya, pamoja na *DHMT* za wilaya mbali mbali kwa utendaji wao mzuri na pia kwa kumsaidia Mhe. Waziri katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza katika miradi ya maendeleo kwenye programu ya kumaliza malaria. Maradhi ya malaria tunakumbuka siku za nyuma ilikuwa ni tatizo sugu miaka kama mitano iliyopita, lakini hivi sasa kwa jitihada ya serikali kupitia Wizara ya Afya hivi sasa tatizo la malaria limepungua kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa serikali na Wizara ya Afya kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kupunguza malaria kwa kiasi kikubwa, jambo ambalo limewafanya wananchi wetu kufanya shughuli zao bila ya matatizo yoyote ya kusumbuliwa na malaria.

Mhe. Naibu Spika, pia, napongeza kwa utaratibu mzima ambao Wizara ya Afya inatoa kwa kutoa vyandarua kwa wananchi wetu ili kuzuia maradhi ya malaria. Hii ni hatua nzuri inastahiki pongezi.

Mhe. Naibu Spika, kuna mradi wa shirikishi wa maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma. Hii nitasoma katika *page* ya 33, kifungu cha 13.3.2. Hapa katika ripoti yao wameeleza jumla ya watu 91 wamepatiwa ushauri nasaha wakiwemo Unguja 58 na Pemba 33. Watu 60,638 walichunguzwa wakiwemo 29,896 ni wanaume, kati ya hao waliogunduliwa *VVU* ni watu 330 sawa na asilimia 44.6.

## UTARATIBU

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunachangia Bajeti ya Wizara ya Afya na mara nyingi sana tunapokuwa sisi Wajumbe hatupo tunapokuja kuuliza maswali tunaambiwa wewe ulikuwa hupo ulikuwa nje

unasikiliza majibu majibu yashatolewa. Sasa hayupo waziri, hayupo naibu. Je, Mheshimiwa, naomba utaratibu hali halisi ilivyo, tuna uwezo wa kuendelea na hii bajeti yao au tukae tuwasubiri mpaka waje. Naomba utaratibu.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, Kaimu Waziri wa Afya ni mimi hapa niliyesimama, nadhani nitachukua hoja zote za Wajumbe.

**Mhe. Naibu Spika:** Kaimu waziri yupo tuendelee Mhe. Marina Joel.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika ukurasa wa 33, kifungu cha 13.3.4. Katika ripoti ya Mhe. Waziri, ameeleza jumla ya watu 91 wamepatiwa ushauri nasaha wakiwemo 58 Unguja na 33 kwa Pemba. Watu 60,638 walichunguzwa wakiwemo 29,896 ni wanaume na kati ya hao waliogundulika na virusi vya UKIMWI ni 330 sawa na asilimia 44.6.

Mhe. Naibu Spika, suala la maradhi ya UKIMWI yapo na yanaendelea kukua siku hadi siku, lakini kutokana na jitihada ya serikali na Wizara ya Afya kwa kiasi fulani elimu imetolewa ya kutosha na hata mtu akienda kupima sasa hivi virusi vya UKIMWI atapata ushauri nasaha, akipewa majibu yake anakuwa anaondoka na furaha kabisa, tofauti na miaka mitano sita iliyopita mtu akipewa yale majibu tu wengine wanazimia hapo hapo au anaweza aka-*flat*, wengine majibu yao wanapewa watu wengine. Lakini sasa hivi kutokana na elimu iliyotolewa na Wizara ya Afya kupitia serikali kwa kweli watu wengi wameelimika vya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mjumbe mmoja alisema kuhusu madada poa na kaka poa kutokuingizwa katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Hao madada poa na kaka poa hawa ni wananchi wa nchi hii, wanahitaji kupata elimu na haya maradhi ni maradhi mabaya ambayo yanaambukiza. Kwa hiyo, kuwaacha hawa kutokupata elimu ina maana kunapelekea maambukizi kuzidi kuendelea, lakini wakipatiwa elimu hawa wanatoa elimu kwa wale wenzao ambao wako rika moja.

Mimi nilikuwa mratibu wa UKIMWI wa wilaya Mheshimiwa karibu miaka kumi na ninaielewa hali halisi ya UKIMWI, unam-*train* kaka poa ili aende kuwasomesha wale wenzake kwa sababu wale ndio ambao wanafanana na wanaweza kumsikiliza. Kwa hiyo, kupata elimu dada poa, kaka poa hili ni jambo la lazima kwa sababu tunawanusuru wananchi wetu na maradhi haya ya maambukizi ili wasiweze kuendeleza maambukizi kwa watu wengine. Hii ni haki yao kupata elimu na serikali yetu Mheshimiwa haibagui inatoa huduma sawa kwa wote.

Mhe. Naibu Spika, Huduma ya Tiba kwa Wagonjwa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI imeelezwa hapa wagonjwa 7,820 wamesajiliwa sawa na asilimia 67.7. Halafu walioanzishwa dawa za *ARV,s* ni 3,587; lakini kuna hawa 1,788 sawa na asilimia 33.3 hawa tumeambiwa katika hotuba ya Mhe. Waziri wamekimbia kuchukua dawa.

Mhe. Naibu Spika, elimu imetolewa lakini kukimbia kwa wagonjwa hawa sio sababu ya kusema labda tuilaumu serikali. Serikali imetoa elimu ya kutosha, watu wamejitokeza wakenda kupima, wamepata majibu, wamefahamishwa jinsi gani ya kuishi na matumaini watatumia dawa, lakini wameanza kutumia dawa baadae wakakimbia.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mjumbe mmoja alisema kwamba serikali inajipanga vipi. Hili suala jamani la UKIMWI ni suala la mtu mwenyewe binafsi kutaka mabadiliko, ukisema mimi sitaki UKIMWI basi huwezi kupata UKIMWI. Kwa hiyo, hili jambo la UKIMWI ni mtu mwenyewe kubadilika tabia, tusikae tukailaumu serikali, hii ni mtu mwenyewe kubadili tabia ukisema sitaki UKIMWI utatulia hupati UKIMWI, lakini serikali kwa kiasi fulani imejitahidi kuelimisha wananchi wake kuhusu suala zima la majanga ya UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo idadi hii si ndogo nayo serikali pia nizidi kuishauri izidi kutoa elimu ili watu wawe na uelewa zaidi na hao ambao hata kama wamekimbia waweze kuwafanyia utaratibu. Kwa sababu naamini takwimu zipo wawafuatilie ili waendelee kuishi na matumaini na kutumia dawa hizo.

Mhe. Naibu Spika, tuna huu mradi wa kupandishwa hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja ikawa ya rufaa na kumeelezwa hatua mbali mbali ambazo serikali imezichukua. Hatu ya kwanza ni ujenzi wa jengo la huduma za upasuaji maradhi ya mgongo na ubongo hili nimekamilika. Pia, serikali imetia mkataba na Kampuni *RANS* kwa ajili ya ujenzi wa jengo la watoto chini ya ufadhili wa Serikali ya Norway. Jengo hili litakuwa na wodi mbili za watoto, maabara ndogo, kitengo cha kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya mafigo na chumba cha watoto wenye uangalizi maalum. Vile vile, wametaja gharama za mradi huo utagharimu karibu dola za Kimarekani milioni mia moja.

Mhe. Naibu Spika, pia, hapa napenda kuipongeza serikali kwa hatua ambayo imefanya. Halkadhalika, katika kuimarisha Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa hospitali ya rufaa kuna ujenzi wa jengo la *clinic* ya maradhi maalum, wodi ya wazazi, chumba cha huduma ya dharura, chumba cha upasuaji, wodi ya watoto wachanga na wodi ya huduma za kangaroo kwa watoto tayari pia umeshaanza. Mitambo mbali mbali na vifaa vitawekwa na ujenzi huo utagharimu *Euro* 9.6 milioni ambapo Tanzania itachangia karibu *Euro* 4 *point something* hivi. Kwa

hiyo, pia na hilo napenda kuipongeza serikali kwa hatua hii nzuri ambayo imefanya. Kuna suala pia la ukarabati wa *ICU* jengo hilo limekamilika.

Mhe. Naibu Spika, haya ndio mambo ya kuyazungumza katika chombo hiki, wizara zimejitahidi kwa kiasi kikubwa ambacho tumetekeleza katika serikali hii. Mhe. Naibu Spika, sio kukaa hapa tukasema hakuna *Vim*, hakuna *Detol*, ikawa tena suala hilo tu, kuna mambo madogo madogo unakwenda *direct* kwa uongozi wa wizara kuyapeleka. Suala la *Vim*, suala la *Detol*, suala la sabuni nenda kwenye uongozi wa wizara ukaeleze matatizo hayo madogo madogo, lakini haya ndio masuala ambayo ya kuyazungumza katika Baraza hili, ambapo mambo yaliyotendeka ya miradi mbali mbali ya kusaidia jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna mradi wa taaluma na hii katika *page* 38 kifungu cha 13.7.1. Mhe. Naibu Spika, hapa tumeelezwa katika ripoti ya Mhe. Waziri anasema wizara ilianzisha mafunzo ya udaktari hapa nchini kwa mashirikiano ya Chuo Kikuu cha Cuba na jumla ya madaktari 38 tayari wamehitimu na madaktari 12 wanaendelea na masomo yao mwaka wa sita. Napenda kuipongeza tena Mhe. Naibu Spika, wizara pamoja na serikali kwa jitihada kubwa ambazo za kuwaletea huduma za afya wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, kuna Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi. Moja ya jukumu la bodi hii ni kufanya ukaguzi. Hivi karibuni nilikaa nyumbani nikaona televisheni imeeleza kama kuna hospitali moja jina nimelisahau ilikuwa ni Pemba, kumepelekwa vifaa na madawa ambayo yamepitwa na wakati. Sasa mimi nilikuwa najiuliza kweli vifaa mpaka vinafika hospitali havijapitia katika uchunguzi wowote.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naiomba hii bodi kupitia Wizara ya Afya wafanye ukaguzi kabla zile dawa hazijapelekwa kule ambako zimekusudiwa. Kupeleka dawa ambazo zimepitwa na wakati ni kuhatarisha maisha ya wananchi wetu, dawa hizi zinaweza zikaleta matatizo kwa wananchi. Kwa hiyo, uchunguzi au ukaguzi uzingatiwe katika uletaji wa madawa mbali mbali ambayo tunapatiwa na wafadhili mbali mbali kutoka katika vituo vyetu vya afya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala zima la nyumba za madaktari ni muhimu kwa sababu kuweko kwa nyumba za madaktari karibu na kituo cha afya kunasaidia hata ikitokea kesi yoyote kwa *time* yoyote hata kama usiku wa saa ngapi inaweza ikasaidia, kuwepo yule daktari karibu pale na kuweza kuihami ile hali ambayo imejitokeza. Kwa hiyo, niiombe wizara ichukue jitihada za makusudi kujenga nyumba za madaktari wetu katika vituo vyetu ambavyo vipo katika maeneo yetu.

Pia, niwaombe hapa viongozi wenzangu Mwenyezi Mungu akitujaalia kurudi madarakani na Mwenyezi Mungu atatujaalia itakuwa hivyo, moja ya ajenda yetu ambayo tutanadi kwa wananchi kuwafanyia iwe ni kujenga nyumba za madaktari. Kwa sababu vituo vya afya vipo vya kutosha nyumba za madaktari ndio changamoto.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba hapa nitoe shukurani za pekee kwa wizara kwa suala zima la kuwatunuku vyeti wauguzi wetu ambao wamestaafu, wametumikia serikalini miaka mingi. Katika kutunukiwa kwao mimi na mama yangu tulikuwemo kwa sababu mama yangu alifanya kazi miaka 40 katika Wizara hii ya Afya. Kwa hivyo, natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Wizara ya Afya, naomba mchakato huu uendelee kwa wengine, hii inawapa wale watu ambao wametumikia nchi hii na kuona kwamba inawathamini serikali yao. Nasema ahsante sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba nitoe ushauri kwa suala zima la madaktari au wauguzi wenye lugha iliyokuwa sio nzuri, baadhi ya wenzangu wamezungumza. Hii nasema si madaktari wote wala si wauguzi wote, kuna baadhi tu ambao wana tabia hii. Suala la wauguzi kwa suala la huduma za afya kwa kweli kama ni wito. Kwa hiyo, nawashauri madaktari, wauguzi na wale wote wanaofanya kazi hospitali kuwa waadilifu, kuwa na lugha nzuri, wawe na usiri, kwa sababu hii kazi ni ya wito, tunahudumia watu mbali mbali wenye magonjwa mbali mbali, wenye matatizo mbali mbali wanahitaji faraja. Kwa sababu pale mtu anakuwa yupo katika hali nyengine, kwa hiyo, anahitaji lugha nzuri, anahitaji kusikilizwa. Kwa hivyo, ninawashauri wafanyakazi wa Wizara ya Afya wanaohudumia wananchi wetu wauguzi, ma-*nurse,* wote kwa ujumla watumie lugha nzuri kwa sababu kufanya hivyo hata Mwenyezi Mungu naye atakuzidishia baraka katika maisha yako.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia wizara imejitahidi kutekeleza mambo mengi mbali mbali ambayo ni mazuri. Kwa hiyo, ninachoshauri kusiwe na baya dogo au moja, mawili tukaifanya Wizara ya Afya yote haijafanya kazi. Kwa kweli imejitahidi na mambo yanaonekana. Changamoto sikatai kama zipo, changamoto zipo lakini ni moja ya kazi, huwezi kufanya kazi bila ya kupata changamoto. Changamoto katika kazi ni kuendelea mbele, kwa sababu ukipata changamoto ina maana unajipangia mikakati ya kuweza kutatua zile changamoto na kuweza kuendelea katika kazi zako.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho katika *page* 38 kuna changamoto ambazo zimeainishwa katika ripoti hii. Kuna changamoto ya ufinyu wa upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa kazi za wizara. Upatikanaji wa fedha ni finyu pengine fedha inayoainishwa katika bajeti wanapata asilimia ndogo kuliko, tuangalie hizi huduma kuna taasisi Mhe. Naibu Spika, kwa kweli si za kuzipa fedha ndogo kwa

sababu ni taasisi ambazo zinatoa huduma kwa wananchi wetu, zinatoa huduma kwa kunusuru maisha ya wananchi wetu. Kwa hivyo, naiomba serikali bajeti ya Wizara ya Afya ikiwezekana iongezwe na hata kama imepangwa kupata hiyo asilimia basi ipatiwe asilimia yote Mheshimiwa tena kwa wakati muwafaka.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la upungufu wa wafanyakazi wenye taaluma ya juu ya uhandisi na vifaa vya tiba inayokwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia. Hii nimuombe waziri changamoto hii ina maana kwa sababu suala la upungufu wa wataalamu ina maana kunaweza kukadhorotesha ufanisi katika wizara yake.

Kuna changamoto nyengine uwepo uingiaji wa bidhaa zilizopitwa na muda kwa matumizi hatarishi ya wananchi. Nalo hili limeandikwa changamoto katika ripoti hii, naiomba hiyo Bodi ya Ukaguzi ifanye kazi yake vizuri kwa sababu kuna watu wanauza bidhaa pengine wanabadilisha *date,* wanaandika tarehe pengine ya mbele, lakini athari hapati yeye, yeye anaangalia faida tu, lakini athari wanaopata ni wananchi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, suala hili la bidhaa kupitwa na wakati naomba walifanyie mikakati ya makusudi kwa sababu wataoathirika ni sisi pamoja na watoto wetu na vijukuu vyetu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho utegemezi wa wahisani katika ununuzi wa dawa na vifaa vya tiba. Tunajua serikali yetu inategemea misaada mbali mbali kwa wafadhili mbali mbali, naiomba kwa suala la dawa serikali ijidhatiti itumie fedha zake ili tusingoje ufadhili kutoka nje ndio ulete dawa, ikiwa dawa hakuna serikali ichukuwe hatua hapo hapo kuliko kutegemea nje. Mimi nathamini michango ya wafadhili kwa sababu inatusaidia sana katika sekta mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia mia moja. (*Makofi*)

**Mhe. Abdalla Moh'd Ali:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kupata fursa kama nilivyokuomba japo dakika tano ya kuzungumzia machahe kwenye hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, nafanya hivi kwa sababu sina uhakika huenda pengine ikawa mara yangu ya mwisho katika Baraza lako tukufu kuchangia hotuba ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu. Hii Wizara ya Afya ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.
Lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba zile neema alizoniazima hajazichukuwa mwenyewe leo hii, nashukuru kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wezangu hasa wanaotoka katika Wilaya ya Mkoani wamezungumzia Hospitali ya Abdalla Mzee. Tunawashukuru sana Makomredi wenzetu wa Kichina ambao toka mwaka 1969 wako bega kwa bega na sisi kutusaidia katika huduma hii na hivi sasa katika mpango wa serikali wa kuboresha Mahospitali, Hospitali ya Abdalla Mzee imeonekana upo umuhimu nayo hospitali ile kuiboresha.

Kusema kweli ujenzi unaendelea na hivi sasa unaendelea kwa haraka sana. Lakini mimi ninachotaka nikumbushe ni kwamba Mhe. Naibu Spika, kabla ya ujenzi huu jengo lilikuwepo pale Abdalla Mzee na lilikuwa zuri sana, lakini limebomolewa na hivi sasa linaendelea kuwa ni jengo na natarajia serikali kwamba jengo lile ilibadilishe sasa ilipe jina jengine lile jina la jengo kwamba ni nyumba liondoke na liwe ni hospitali na linapokuwa hospitali Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ambayo yanatafautisha na nyumba ya kawaida, mambo hayo yakiwemo ni madaktari pamoja na vifaa na madawa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hapo nyumba tulizoea kwamba pale Abdalla Mzee tunaweza tukaa miezi mitatu hata ile *X-ray* basi tukaitafute Vitongoji kule kunakoambiwa kuna *Mortuary* na hivi sasa tunatarajia jengo kwa sura litakuwa ni jengo la kisasa kabisa. Lakini hili jengo ni jengo la tiba na tiba uwe na madaktari, vifaa na madawa. Sasa sijui serikali kwa hili najua kwamba madaktari wenzetu Makomredi wa China mara nyingi huwa wanatusaidia kwa madaktari na wanatuletea wanakuwa wapo pale wanakuja kwa zamu miaka miwili wanaondoka wanakuja wengine.

Lakini katika sehemu ya vifaa inakuwa ni jukumu la serikali pamoja na madawa, wachina wanajitahidi lakini bado serikali inalo jukumu la kuendeleza upatikanaji wa madawa pamoja na madaktari ambao wachina hawakutuletea. Sasa sijui serikali imejiandaa vipi, kwa sababu kama tunasema tunataka kuboresha ile huduma sio jengo ni madaktari bingwa. Sasa je, kuna mpango wowote ule ambao serikali umeundaa wa kuona kwamba baada ya kukamilika kwa jengo hili tunalibadilisha jengo hili na kuwa ni hospitali kwa maana ya tiba kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, madaktari wenzetu au hawa Makomredi wenzetu wa China wanajitahidi, lakini inafikia wakati tunavunjika moyo kidogo kwa sababu wakati wa kufika likizo huwa wanaondoka siku nyengine miezi miwili mpaka mitatu na tunakuwa hatuna mzalendo pale ambaye yeye anaweza aka-*cover* ile huduma wanayoitoa hawa wataalamu wenzetu kutoka china.

Sasa sijui serikali imejiandaa vipi kwa hili kwamba je, wenzetu wanakwenda zao mpaka China muda wa mwezi hawapo, tutakuwa na mabingwa ambao wanaweza ku-*cover* ile sehemu ambayo wameondoka na kuondokana na ule utaratibu wa

wagonjwa wetu wanaotoka Mkoani labda kutafuta tiba sehemu nyengine za Chake Chake, Vitongoji na Wete. Kwa hiyo, naomba serikali hili ilione kwamba hivi sasa tunatarajia kupata jengo lakini je, tiba itapatikana ili kumuondelea mwananchi usumbufu. Kwa sababu hivi sasa ukitaka kufanya *beriameal* na vipimo vyengine hizo zilizopo zimechoka, unatakiwa sijui wengine wanafanya safari ya kwenda Chake Chake. Lakini Chake Chake huko inabidi ukodi *ambulance*.

Sasa jengine ninalotala kuuliza hapa hivi sasa kuna Waheshimiwa ambao wameeka katika Majimbo yao magari ya kuchukulia wagonjwa. Sasa je, kutokana na kwamba hivi sasa huduma hiyo inatolewa na baadhi ya Wabunge na Wawakilishi katika Majimbo yao, serikali imeliachia mkono imeondosha mkono wake katika huduma hii. Haitoi tena huduma ya kuchukuwa wagonjwa hasa wake wanaohitaji matitabu ya haraka. Kwa sababu naomba ma-*ambulance* yalipo yanatumika kwa huduma nyengine tu. Lakini hayatoi huduma za kutosha kwa ajili ya kuchukulia wagonjwa maeneo ya ndani ambayo hizo *ambulance* zilizowekwa na Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi nyengine haziwezi kufika kutokana na ubovu wa barabara.

Sasa je, tumeboresha huduma nyengine lakini huduma hii serikali imeiacha mkono, sijui huu utaratibu tumewawachia Wabunge moja kwa moja na Wawakilishi kwamba wao watoe ma-*ambulance* serikali tena basi au bado inaendelea na utaratibu huu na imejipanga vipi katika suala hili la upatikanaji wa magari ya kuchukulia wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, umenipa dakika chache. Lakini kuna suala ambalo nataka nilizungumze kidogo kuhusu Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya. Chuo hichi hivi sasa kinajitahidi sana kutoa wanafunzi au kutoa wataalamu ambao wanatusaidia katika Mahospitali yetu. Tunashukuru kwa hilo ingawa ajira zao zinasua sua, wizara hii mimi sitaki niseme kwa sababu hawahusiki na mambo ya ajira.

Katika Programu zao wanazokusudia kuzifanya wamesema wanaandaa *business plan* ambayo itasaidia katika kuboresha mapato yao. Ni imani yangu Mhe. Naibu Spika, kwamba *business plan* hii itakapofanyakazi malipo ya wanafunzi wanaoingia chuoni pale yataongezeka. Sasa yakiongezeka malipo imani yangu kwamba watakaoingia kujifunza pale pia watapungua na chuo hichi mpaka hivi sasa kinatoa ngazi ya Diploma na utaratibu wetu katika serikali ni kwamba wanaosoma ngazi ya Diploma wao bado hawajaingia katika Mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Serikali.

Sasa je, kufanya jambo hili ambalo litatunguza kwa imani yangu wanafunzi kuingia katika chuo kile, imani yangu kwamba wanafunzi au wataalamu wa tiba

watapungua jambo ambalo ni hatari katika nchi yetu. Sasa sijui wakifanya suala hili kuna utaratibu gani labda mwengine wa serikali wa kuwasaidia hawa ambao labda malipo yao yataongezeka katika chuo kile na huku kutasababisha kupungua kwa wanafunzi ambao tunawahitaji au madaktari ambao tunawahitaji katika chuo kile.

Lakini pia katika chuo hichi niulize tena Mhe. Naibu Spika, utakutia ukienda mahospitali unakutia baadhi ya madaktari huwa hatuna,yaani wataalamu na ukiangalia utakutia fani moja ina wanafunzi wakunga pengine *general nursing* wasiopungua 50. Lakini fani yengine zinakosa wanafunzi. Sijui hichi chuo hivi sasa kinapokea ushauri kutoka serikalini kwamba sisi hivi sasa tunataka watu wenye fani fulani ili wakashike nafasi fulani katika mahospitali yetu au chuo kinachukuwa tu wanafunzi na kusema sisi tunasomesha. Naomba Mhe. Naibu Spika, umewesha taa nakuheshumu.

Lakini la mwisho, naomba uniruhusu Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu huu UKIMWI. Takwimu Mhe. Naibu Spika, zinatuwashia taa kwamba kila leo naona takwimu hazipungui na wafadhili wanaingiza pesa nyingi sana na serikali inaingiza pesa nyingi sana kutokomeza tatizo hili. Lakini bado lipo na *ethic* za ukimwi haziruhusu mtu yule ambaye ana matatizo yale kumtangaza mawazo yangu ni kwamba hili ni moja katika matatizo na sisi maadili haya tumeyachukuwa moja kwa moja kutoka kwa wenzetu ambao wanatufadhili zaidi katika kutokomeza maradhi haya. Labda serikali haijaona kwamba sasa kwa upande wetu sisi Zanzibar kwamba hili tatizo linaenea kwa sababu ya kutambulika, ukijua kwamba njia ile ina nyoka Mhe. Naibu Spika, utachelea kuipita.

Lakini ukiwa hujui wewe utakuwa unapita siku zote. Sasa walio na matatizo haya hatuwafahamu na tumekewa miko kwamba, aaah, tusiwatangaze na miko hii inatokana na wenzetu ambao wameshaendelea zaidi kuliko sisi. Labda serikali haioni kwamba hivi sasa iko haja ya miko hii kuiondoa na kutengeneza utaratibu wetu wenyewe hapa Zanzibar utakaoturuhusu wale watu ambao wana matatizo haya kuwatambua ili kuepukana nao. Mhe. Naibu Spika, taa umeshaiwasha muda mrefu nakushukuru. (*Makofi*)

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sina budi kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kwa mara nyengine tena kufika hapa na kuendelea kwa yale tunajipangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na sura ya kitabu chetu hichi ambacho ni cha Wizara ya Afya. Mhe. Waziri, hapa ametupatia.

Hichi kitabu mbele kuna picha inamuomesha Mhe. Rais pamoja na mwana mama wa kizungu na Mkurugenzi Mkuu naona wa Hospitali ya Mnazi Mmoja Dr. Jamala namuona yupo hapa. Lakini nikigeuza nyuma huku nakuta kuna jengo letu jipya jengo ambalo linashughulika na huduma za upasuaji wa uti wa mgongo na vichwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, haya ni mambo matamu mno. Lakini nikitizama chini nakuta kuna picha nyengine inamuonesha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akienda kukagua hospitali binafsi ya ndugu yetu Turky pamoja na watu wengine wengine.

Haya ni mafanikio makubwa sana kwa upande wa Zanzibar kwamba Zanzibar ya leo imeweza kufikia hadi ikawa sasa tuna upasuaji wa uti wa mgongo na kichwa ndani ya Zanzibar yetu. Hili ni jambo la faraja sana Mhe. Naibu Spika kwa Zanzibar kufikia hatua hii. Lakini haya yote yametekelezwa chini ya utekelezaji makini wa Ilani ya Chama cha Maapinduzi inayosimamiwa na Dr. Ali Moh'd Shein.

Mhe. Naibu Spika, leo sina mchango mkubwa sana katika wizara hii hususan nikitilia maani kwamba wezangu wameshachangia mambo mengi sana. Mimi nakuja katika ukurasa wa 36, kifungu cha 13.5 ambacho kinahusiana na mradi wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kwenda katika buku letu kubwa hili nikaangalia mambo ambayo wizara hii imeyapa kipaumbele. Mhe. Naibu Spika, pamoja na mambo tayari watendaji kwa kushirikiana na Waziri wao pamoja na Naibu Waziri wametoa kipaumbele katika wizara yao. Lakini huu utamu ambao umeoneshwa hapa katika picha za kitabu hichi hautoamilika ikiwa bado tutaendelea na tatizo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tatizo la kupandisha wagonjwa wetu kwa kutumia mikono pamoja na zile machera kuwapandisha kwa kutumia ngazi za kupanda kwa miguu.

Naomba sana Waziri pamoja na watendaji wake katika bajeti yake ambayo ameileta kwetu kuna mafungu matatu. Katika ukurasa wa tabu kubwa hili *Volume II*, ukurasa wa 467 kuna maeneo matatu nimeyaona. Kwa maeneo haya Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri, tupunguze fedha sasa katika kifungu aidha iwe mradi wa huduma za kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi mmoja au maeneo mengine matatu ambayo yapo katika P02 ukurasa wa 467, P02 ambayo vile vile, inaendelea mpaka ukurasa wa 468. Maeneo haya matatu SO1 na S02 idadi ya fedha kama hivi nitakavyozitamka.

Eneo la kwanza lina shilingi 21,313,144,000.
Eneo la pili lina HO4 16,297,627,000.
Eneo la tatu H06 ina shilingi bilioni 1,500,000.

Katika maeneo haya matatu kwa heshima na taadhima namuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Naibu Waziri wake na wataalamu watendaji wake tukasimu shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kuweza kununua ma-*lift* ili Hospitali ya Mnazi Mmoja iweze kuwa na *lifts* za kuweza kupandisha wagonjwa ambao kwa sasa wanapelekwa kwa kutumia mikono. Naomba sana maeneo haya niliyoyaangalia zikitoka shilingi mia moja hakuna athari ambayo itakuwa inatokea hususan nikiangalia muongozo wa *activities* ambapo ni mipango imara wizara imejipangia.

Mhe. Naibu Spika, katika wizara hii inahitaji kuidhinishiwa shilingi bilioni thamanini na nne, milioni mia tisa na thamanini na laki moja. Sasa fedha hizi ili na mimi miweze kuridhia kuvipitisha namtaka Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe uhakika kwamba suala zima la *lift* ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja litatengewa fedha maalum na kufanyiwa utaratibu ili katika mwaka huu wa fedha *lift* ile ipatikane iweze kwenda sambamba pamoja na uhalisia wa majengo haya mazuri ambayo tumeyaona hapa katika kitabu hichi lakini pia na sifa ambayo ipo katika hospitali yetu hii ya Mnazi Mmoja hospitali ambayo tunaitegemea kwamba ni hospitali ya rufaa.

Mhe. Waziri, atakapokuja hapa akinithibitishia kununuliwa kwa *lift* nitaikubali bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. La kama hakunithibitishia hilo hapa tutapunguza fedha hata kama katika fedha zake mwenyewe tuhakikishe kwamba tunazitumia kwa kuzichanga na kuona kwamba tunanunua *lift* kwa pesa ambazo zinatokana na huduma yake yeye mwenyewe.

Jambo la pili ambalo nataka kuchangia, nimesema leo mchango wangu ni mdogo sana. Naomba sasa wale wazee wetu na wale wakunga ambao wanawasaidia akina mama katika maeneo yetu ya mashamba katika kujifungua, naomba sana inapotokezea ule mshipa wa damu ukakatika katika suala zima la uzazi wa akinamama, wale wazee ambao wanashughulika na ukunga wao wa jadi katika maeneo ya mashamba, wawakimbize akinamama wale katika mahospitali ili waweze kusaidia kuokoa maisha ya mama na mtoto badala ya kukaa na kusema kwamba maji tayari yamejaa baharini. Naomba sana suala hili kwa wazee wangu ambao wapo mashamba waliangalie na tuweze kufanya utaratibu wa kuweza kunusuru hali za akinamama na watoto katika maeneo hayo.

Baada ya maelekezo hayo sasa Mhe. Naibu Spika, nimesema leo sina mchango mkubwa na baada ya kwisha Mhe. Waziri, kunithibitishia kwamba ile *lift* itanunuliwa, kwa kuanzia ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia 60, asilimia 40 ninasubiri Mhe. Waziri, akinipa uthibitisho wa kununulia *lift* ninamkamilishia ile asilimia 40 zilizobakia, laa hakunipa ninazuia kifungu kwenye bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia hizo. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mheshimiwa. Wa mwisho ni mchangiaji Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikukushukuru wewe kwa jinsi na jitihada na umakini wa hali unavyokiendesha kikao hichi.

Mhe. Naibu Spika, leo nimebadilisha utaratibu wa kuchangia. Mara nyingi kabla ya Mhe. Spika au Mwenyekiti kukaa hajafika huwa ninakuja hapa kuchangia mwanzo, wakati mwingi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, hapa haniwezi. Lakini maneno ya mwisho ninafikiri yanakuwa na nguvu kidogo, maana yake ukimwambia mtu mwanzo anaweza kusahau, mara ya mwisho anaweza kupata kumbukumbu nzuri kukumbuka. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu utakuwa katika sehemu tatu muhimu kwa siku hii leo:-

1. Kushukuru
2. Kuchangia hoja
3. Maombi

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake wa hali juu kupita kiasi kwa jitihada anazochukua hasa ukizingatia sekta ya afya ameipa kipaumbele kweli kweli. Ni ukweli usioficha na ninapomshauri kwa sekta hii Mhe. Rais wetu amekuwa msikivu na mtulivu kupita kiasi. (*Makofi*)

Mhe. Balozi Seif Iddi naomba umpelekee salamu zangu za dhati mimi Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kwa Mhe. Rais, tumeona jitihada anazozichukua ikiwemo tulipiga kelele sana suala la ada ya wazazi hapa, ikawa watu wakafikiria labda ninasema uwongo, ilifika wakati mtu akenda hospitali hana shilingi elfu arobaini za kununua vitu, anaweka rehani mwenye chombo cha dhahabu ili apate kujifungua. Mhe. Rais tunamshukuru sana na Mhe. Balozi tupelekee salamu hizo hasa zake anazozifanya. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, si hilo tu amefanya jitihada nyengine ya kuhakikisha *ICU* ya kimataifa ipo hapa hivi sasa. Aga Khan ninathubutu kusema hawana *ICU* ile tuliyokuwa nayo sisi Hospitali ya Mnazi Mmoja. (*Makofi*)

Ikiwemo vile vile kuongeza baadhi ya fedha katika Wizara hii ingawa hazijafikia asilimia 35, 45 mpaka 50, zimeongezeka kiasi fulani ni jambo la kushukuru. Ninashukuru sana Wizara ya Fedha kwa jitihada hii, hazikidhi kweli lakini mbuzi anakula majani kutokana na urefu wa kamba yake. Kwa hivyo, zimeongezeka kidogo fulani, ni jambo la kushukuru. (*Makofi*)

Vile vile, ikiwemo ada za wanafunzi Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais amekuwa msikivu kaziondoa, kanunua meli ambayo mwezi huu au tunafikiria mwisho unaokuja itafika kwa kuwajali wananchi wake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nichukue fursa hii ukizingatia kuwa hichi ndicho kipindi chetu cha mwisho, tusiwe tunatupa lawama tu kupita kiasi kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa jitihada anachochukua za hali juu na anavyomshauri Mhe. Rais. (*Makofi*)

Na vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais katika jitihada za kufungua ufunguzi uliofanyika katika *ICU* mpya alikuwa ni mgeni rasmi, pia, nimpongeze kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi vile vile tena kwa mara ya pili uchukue fursa hii kupeleka salamu zetu za dhati kabisa wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako hili kwa ndugu zetu wa damu kabisa Serikali ya Jamhuri ya China kwa mchango mkubwa sana waliotupa katika sekta ya afya, ambapo hauna mfano. Tupelekee salamu hizi kwa Balozi wa China kwa jitihada alizochukua za hali ya juu kwenye sekta ya afya, amejitahidi sana.

Mhe. Naibu Spika, niendelee tena kuwashukuru Mawaziri mawili katika kipindi hichi cha miaka mitano; Wizara ya Afya mwanzo iliongozwa na Mhe. Juma Duni Haji baadae ikaongozwa na rafiki yangu Mhe. Rashid Seif ambaye hivi sasa ninafikiria kaamua kutaka kupumzika ama kustaafu katika mambo ya shughuli za siasa. Lakini nimwambie tu pengine huja likajalikatokea neema nyengine kama akiachia jimbo. Itakuwa sijafanya haki vile vile Manaibu Waziri wawili waliokuwa wakiongoza kwa kipindi hicho hicho vile vile Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya na rafiki yangu ndugu yangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa jitihada anazozichukua. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, usione hapa tunauliza maswali kwa kuwajengea hoja ni wajibu wetu na ukweli wenyewe Naibu Waziri pengine hawayaoni haya ili tukukumbushe sisi huku wapate kuyaona kuyajenga uwezo zaidi kuonekana hali ilivyo. Nikushukuru sana ukizingatia ni kipindi chetu hichi cha lala salama. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, itakuwa si mwingi wa fadhila kama sikumshukuru vile vile Katibu Mkuu Mohamed Saleh Jidawi kwa jitihada anazochukua na anapokuwa katika majukumu yake. Salamu nyengine za dhati zifike kwa rafiki Dkt. Jamala Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Huyu nimefanya naye kazi kwa muda mrefu na katika kipindi cha miaka miwili katika kamati tumekwenda naye vizuri sana, nimshukuru kuchangia vile vile ninapokuwa na matatizo yangu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nianze na mchango wangu sasa, ile ya mwanzo ilikuwa ni mambo ya shukurani. Sasa nianze mchangu hasa katika hospitali tatu ambazo ni muhimu sana Mhe. Spika, hapa Unguja, ikiwemo Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini ninataka kumwambia Naibu Waziri haijafika Hospitali ya Rufaa kama anavyojibu yeye humu. Hata kitabu kimeandikwa ukiangalia, mategemeo kufanya Hospitali ya Rufaa, unapokuja kujibu ukasema kwamba ni Hospitali ya Rufaa bado haijafika Hospitali ya Rufaa kwa maelezo ya kitabu hichi si maneno yangu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, jengo lile sasa hivi kubwa hali yake hairidhishi hata kidogo kwa baadhi ya sehemu. Ghorofa ya juu na ya tatu inavuja na *ceiling* yake ni mbovu. Ipo haja Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri mukaliangalia mukafanya ziara makusudi kutokana na hali ile. Isifike mpaka wakati tena, kuna msemo wa Kiswahili unaosema; "Usipoziba ufa utajenga ukuta".

Ngazi zile tunazopandia hivi sasa haziridhishi zishalika zote. Jengo lile ni muhimu haliridhishi kabisa. Kwa hivyo, nilikuwa ninawasihi sana muangalie mandhari ya jengo lile lilivyo na kama ikiwezekana ninafikiri panapojaaliwa mukalijengea bajeti yake mukafanya *renovation* kubwa sana ya jengo lile, hairidhishi kwa hali lilivyo; milango kuna sehemu hamna, kuna sehemu mumetia nikupongezeni kwa dhati kabisa, kuna madirisha wakati mwengine hayatizamiki.

Jengine nikunasihini sana kwa Wizara ya Afya na watendaji wake, hali ya uchafu kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja imekithiri mno. Hivi sasa ukenda asubuhi kwa hali nilivyoiona pana maji sijui kama ya mtaro yale ukiingia tu pale, maji machafu huwezi kupita, utafute pahali au ukunje suruali kupita. Hili liangalieni ninawasihi sana. Ni wajibu wetu kukumbushana.

Jengine katika sehemu ile ya *emergency* ya huduma ya dhurura pana milango miwili. Nishauri tu kuna mlango mmoja mungeweka *slope* ya kupandishia wale wagonjwa badala ya kupandisha ngazi ya kubebwa; kuna moja kungeekwa ngazi ya kawaida pale, inawezekana hichi kitu nimekiona mimi. Huu ni ushauri, kama mutauchukua ni wa bure ili kigari kile cha baiskeli kipate kupanda kwa urahisi. (*Makofi*)

Jengine mungeliangalia huduma zinazotozwa pale mgonjwa anapofika kibaiskeli kilichokuwepo ni kimoja tu kwa muda huu na ukikipeleka huku kinaelekea huku maringi yake. Kwa pale ipo haja ya kuongeza baiskeli.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije Kitengo cha Dharura ambacho ni kitengo muhimu sana, unapofika pale kuna baadhi ya huduma hazipatikani. Mhe. Waziri na Naibu Waziri ninafikiri mungeweza kusikiliza na watendaji wake kwa makini kabisa ili mukafuatilia kama ninayoyazungumza ni ya kweli.

Suala la *oxygen* ulijibu hapa Mhe. Naibu Waziri, sasa sijui kama imeshafika kweli. *Oxygen* katika kitengo kile ni huduma moja muhimu haipatikani, wodi ya watoto vile vile *oxygen* nayo haipo. Ni kitu muhimu katika maisha ya binadamu, mukakaa mukaliangalia suala hilo. Maana ya dharura ni kitu gani, akifika pale mgonjwa atamkuta daktari lakini vitendea kazi havipo, hiyo dharura sijui itakuwa ya kazi gani. Kuna dawa za kuokoa maisha zinaitwa *Adrenaline*, hizi zinasisitiza mambo ya wapiga moyo na hili mukakaa mukalifuatilia.

Halafu cha kusikitisha chengine pale Mhe. Naibu Spika, kama una mgonjwa unampeleka kama huna vifaa unakuwa mtihani wakati mwengine au unaambiwa unakopeshwa ukatafute pahali baadae uje ulipe. Kuna wengine hali zao haziridhishi kwa kusema ukweli na hili suala mungekaa mukaliangalia vile vile.

Kuna dawa za dege dege zinaitwa *carbamazepine* hizi nazo pia hutumika na pale hazipo. Kuna dawa ya haja kubwa za watoto inapokuwa homa kali nazo hazipo, *parection panadol* zinavyoitwa hazipo. Homa inapokuwa kali kwa mtoto kunakuwa na vidonge makusudi ambavyo hutumiwa kwa kutumia kwa haja kubwa, nazo hazipo.

Kuna dawa *magnesium sulphate* hazipatikani pale Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hizi dawa kwa waja wazito akinamama wenye kifafa. Mhe. Waziri, dawa hizi zifuatiliani, kile kitengo ni cha dharura. Dharura maana yake, ninafikiri munaelewa nini maana ya dharura, hizi hazipatikani. (*Makofi*)

Chengine Mhe. Naibu Spika, hichi kinahusu askari nacho ni *PF3*. Wanapopata mgonjwa pale kama kapata ajali kumpeleka pale ndiyo kazi yao imekwisha. Sasa wale madaktari kuna dawa pale zinataka kununuliwa, wakimuhudumia hawa madaktari inabidi hizi pesa watoe mifukoni. Hichi kitu mukae Wizara ya Afya na Kamishna wa Polisi mukaliangalia hili suala, wakamleta mgonjwa pale kazi yao askari ndiyo imekwisha wamemleta mgonjwa, kazi yote inayomkuta ni daktari. Atatoa wapi pesa za matibabu. Mhe. Waziri ninafikiri naomba uliangalie hili suala nalo, lakini naona Waziri kule anaandika andika hivi sasa.

Tuje katika wodi ya watoto. Hapa niipongeze Serikali ya Norway kwa jitihada kutokana na hali ya wodi ya watoto. Kwa kweli hali hairidhishi, kitanda kimoja Mheshimiwa mzee wangu yule wa Mtambile alizungumza maneno mazuri sana; kitanda kimoja wanaweka wagonjwa watatu; kuna mmoja wa moyo, kuna mmoja anaharisha, kuna mmoja pengine kaungua. Baada ya kutibu tunaongeza maradhi.

Mheshimiwa nikushukuru sana huu ndiyo ukweli ulivyo. Leo hii nilikwenda asubuhi pale, pana *giving set* inatafutwa ya damu ya kumuingizia mtoto hapana, kitu kidogo tu. Ingawa kuna baadhi ya Wajumbe wanasema tusilaumu mambo madogo madogo, kama hakuna madogo, makubwa tutapata wapi. Hesabu huanza na moja, baadae ndiyo unakwenda mbili, tatu na nne.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nije katika Hospitali hii ya Mnazi Mmoja katika Kitengo cha kufunga vidonga. Mazingira ya pale kwenye hali ya usafi hairidhishi. Hii hali muiangalie ili twende vizuri. Jengine zaidi niombe zile barabara za ndani mungezifanyia angalau kuziba yale mashimo, mgonjwa anabururwa kwa kibaiskeli anaumia, barabara za ndani zisafishwe njia ili kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Naibu Spika, nije katika sehemu ya uzazi kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hili nilipongeze kwa dhati kabisa, unajua tuzungumze ukweli ijapokuwa ni uchungu jitihada zinachukuliwa kwa hapa kwa wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja sehemu ya uzazi hakuna matatizo makubwa kiasi fulani.

Nije *ICU* Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hii iliyokuwepo hivi sasa hairidhishi hali yake ilivyo. Naomba mungekwenda mukaitazama, *AC* moja tu ndiyo inayofanya kazi na wakati mwengine haiwashwi, muna mafeni ya kwenda mbio tu mule ndani, joto tupu linazidi. Hayo maneno ya kubahatisha, huo ndiyo ukweli wa hali halisia ulivyo.

Mfanyakazi mmoja jengine atahudumia wagonjwa wale watu wangapi. Mhe. Naibu Spika, mfanyakazi ni mmoja tu, kuna wagonjwa kama karibu wanane au kumi atahudumia kwa wakati gani mfanyakazi huyo mmoja. Huku anahitajika na huku anahitajika, ipo haja ya kuongeza pale.

Kuna dawa za kushusha *pressure Hydralazine*. Hizi nazo hazipatikani, kuna *ceiling*, kuna mipira ile ya kuvutia maji nayo bado haipatikani katika *ICU. ICU* maana yake nini, ni kitengo muhimu ni *Intensive Care Unit.* Kama vitu kama hivi havipatikani Mhe. Waziri, maana yake nini *ICU*. Ndiyo yale nikarudia nikasema hatuna *ICU*, tulikuwa tuna *garage* kipindi hicho. Kuna taa mule ndani ya *bulb, bulb* bei gani. Haya mambo madogo madogo mungekaa mukayazingatia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo, Wizara hapa ije inieleze kuna sababu gani *ICU* iliyojengwa leo karibu nusu mwaka mpaka leo haijafunguliwa mpya, tatizo nini. Hakuna madaktari bingwa wa kuendesha ile *ICU* au vipi, imejengwa *ICU* imefungiwa tu ndani, sijui kuna umuhimu gani ili mukatuelimisha tukalifahamu suala hili. *ICU* mpya imejengwa ya kileo kabisa lakini mpaka leo haijafunguliwa.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kitengo chengine ambacho ni muhimu nacho kuna hali ya kusikitisha vile vile *X-ray department*. Katika Hospitali inayotaka kufanywa ya rufaa, haya yote ninazungumzia kadhia ya hospitali inayotaka kufanywa rufaa vitu hivyo havipatikani.

Mashine zote kubwa mbili zimekufanya Mhe. Naibu Spika, na alipelekwa fundi sijui kutoka Dar es Salaamu naye kashindwa kuitengeneza. Kuna vipimo pale vya *X-ray* havipatikani, kama *lens spin* ya mgongo ile huwezi kupigwa, kuna *scale* ya kichwa huwezi kufanyiwa, pana *mobile* tu iliyowekwa pale, kuna vipimo muhimu havipatikani. Waziri kama munalijua hilo sawa hamulijui lifuatilieni.

Hii *X-ray department* kwa kweli hali hairidhishi. Mashine zote mbili zimeharibika kwa kipindi kirefu, ipo *mobile* tu, kuna vipimo vya mgongo havipatikani vya kichwa havipatikani. *Otherwise*, uende *Al-Rahma Hospital*. Hii ndiyo hali ilivyo na ndiyo mziki wenyewe ulivyo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo patakuwa pana kazi sana katika kupitisha vifungu. Kuna aliyeanza na atakayekuja kesho. Kuhusu banda la wagonjwa nishadanganywa sana humu ndani, miezi sita, muda. Ramani imechorwa hapa utafikiri ni kitu gani. Hili kidogo nitakuwa mkaidi. Pale wale wagonjwa wanaokwenda pale hawapikwi pilau wala biriani wanakwenda kwa dhiki. Leo mvua ile inawanyeshea. Hapa Mhe. Naibu Spika, shughuli ipo leo hii, ukizingatia nimepiga kelele kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati mpaka pahali pale pakapatikana wakatoa hati miliki, leo zile kelele zangu ziwe bure, humu sitotoka Mhe. Naibu Spika, mpaka kieleweke. Wajumbe sijawahi kukuombeni kwa mara yangu ya kwanza, ninakuombeni hili munisaidie. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, banda lile kama halikuweza kujengwa nipewe ramani, mimi nitapitisha bakuli kwenda kuomba lakini pale pajengwe. Nimehangaika sana kugombana na Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban, kuhusiana na suala lile. Hapa linarudia tena na ninazungumza Kiswahili kinafahamika sitofahamu lolote kuhusu banda lolote. Wajumbe ninakunasihini sana, huu ni uongozi na dhamana tumepewa tutakwenda kuulizwa. Nisaidieni kwa hili ninakuombeni sana, ramani kama Wizara haiwezi kujenga itukabidhi tutafute njia nyengine ya kuweza kujenga pale. (*Makofi*)

Haiwezekani mfanyabiashara tu kajenga bandari pale anaitumia kwa maslahi, tunafika pahali pale pana sehemu anaweza kufanya biashara mtu pale. Ikiwa mfanyabiahara pale kajenga bandari inamsaidia na pahali pazuri, kama pale pashindikane kwa kuwasaidia wananchi wetu. Hili naona hapatoshi, nianze kusema kabisa sitofahamu lugha yoyote ukizingatia hichi kipindi changu cha mwisho. Ramani kama imeshindwa Wizara tukabidhini, banda lile limehangaika kwa muda mrefu humu ndani. Serikali niishukuru sana Waziri Ramadhani Abdalla Shaaban baada ya kuona umuhimu ule na akaridhia na Mji Mkongwe ukaridhia, leo tunadanganywa mwaka wa tatu. Hili haliwezekani "*kunfa ya kun". (Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije Hospitali ya Mwembeladu. Hii hospitali ni muhimu lakini cha kusikitisha kidogo ni kesi ya kibanadamu inaweza kutokea, huwezi kulaumu yote na mazuri tuyazungumze, pana ukosefu wa mipira ya uzazi pale. Hili suala mukae mukalifikiria, ikiwa Hospitali ya Mnazi Mmoja pengine hakuna kesi hii, Hospitali ya Mwembeladu kuna kesi ya mipira ya wazazi. Hili mukaliangalie.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo katika Hospitali ya Wazazi kuna gari ya *ambulance*, inapotokea *emergency case* gari inakuwa haina mafuta. Si maneno yangu haya, fuatilieni. Pale *ambulance* inapotokea *emergency case* haina mafuta, sijui kuna fungu gani. Haya ndiyo mambo ya wananchi muhimu.

**Mhe. Naibu Spika:** Umeshatumia dakika ishirini ninakuongeza na dakika tano.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, hapa uniongeze dakika ishirini nyengine, muda tunao kidogo.

**Mhe. Naibu Spika:** Tunakwenda kwa utaratibu, dakika ishirini, ishirini na tano.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Aah! Mhe. Naibu Spika, haya mambo mimi itabidi niende haraka haraka.

Pana maposho ya madaktari hapa kidogo yazingatiwe, mazingira wanayofanya kazi ni makubwa mno, pana taka taka pale bado zinachomwa pale kwenye tanuri liliopo kwenye hospitali hiyo. Kwa hivyo, liondoshwe.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu tena kuhusu *Mental Hospital*. Hospitali hii niliipigia kelele kwa muda mrefu, lakini bado kuna matatizo ya dawa, serikali izingatie, baadhi ya dawa nitazitaja.

Mhe. Spika, *haloperidon injection*, Waheshimiwa Wajumbe hii ni dawa muhimu sana ya kutuliza akili na *chlopromazine injection* hazipo kabisa. Kuna *tablets* zile

*haloperidon* hazipatikani, kuna mambo yameshaingizwa na lile jengo serikali angalau ilifikirie kulifanyia marekebisho, jengo haliridhishi.

Mhe. Naibu Spika, nije katika mchango wangu wa kuomba sana, niiombe wizara hii kwamba imefika wakati wa kuangalia, kuna baadhi ya maradhi kama *NCD*, yaani *Non-Communicable Disease.* Haya maradhi serikali itenge fungu kuangalia maradhi haya ya *pressure* na sukari, kwa nini maradhi yanazidi, hebu tafuteni utafiti wa mambo kama haya. Serikali iwekeze nguvu zake katika maradhi haya.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nije kwa daktari wangu Hamza wa Jambiani. Niiombe sana wizara, hii mara yangu ya mwisho, nafikiri imefika pahala wamekuja wazee kuomba wa kubwa daktari Fadhili nirejesheeni daktari wangu Hamza wa Jambiani, ni daktari ambaye amenisaidia kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, niombe sana na huu ndio mchango wangu wa mwisho, nilisema kuna kushukuru, kuchangia na kuomba. Katika kuomba niombe na nitataka jawabu hapa litoke, ili wananchi wa Jambiani wajuwe, nini msimamo wa serikali kuhusu daktari Hamza, huyu amefanya kazi katika mazingira mazuri sana na tumeshirikiana kwa hali na mali na daktari Hamza.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nije katika Kitengo cha Macho cha Hospitali ya Mikunguni, ili Hospitali ya Rufaa itimie ya Mnazi Mmoja iwe na huduma zote, kitengo kile kirudishwe Hospitali ya Mnazi Mmoja. Ili Hospitali ya Rufaa itimie basi vitu vyote vinatakiwa vipatikane katika hospitali kuu, hivyo, irudishwe huduma ile.

Mhe. Naibu Spika, haiwezekani mtu anakuja Hospitali ya Mnazi Mmoja anatoka pale anaambiwa aende zake Mikunguni. Sasa hiyo rufaa iko wapi. Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kuna huyu Mhe. Mjumbe wa Chambani aliyezungumza hapa, kitendo hiki ni cha kusikitisha sana. Yule mama, niiombe Kamati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, mwende mukaifanyie kazi tena ili muhakikishe mnampata mtu aliyefanya kitendo hiki, ndio maana ya kamati. Haiwezekani mtu mjamzito kesi ya kufa au kupona, yeye mwenyewe hajijui, kufika pale mtu anataka kuzaa, alaa! haya mambo namna gani. Wizara ichukuwe hatua za dharura kuhusu kesi hii. Mhe. Mohammed Mbwana, nyinyi ndio wenye kamati, hili suala lifuatilieni na hili ndio jukumu lenu, haiwezekani na ile iliyompeleka pale ni shida.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia, nichukuwe fursa hii kwa Wizara ya Afya kama kuna mtu niliyemkosea, niliyemuudhi na niliyemuonea anisamehe kwa dhati kabisa. Kama kuna mtu katika Kitengo cha Wizara ya Afya tumekoseana na tumeudhiana, binadamu hakuna mkamilifu, ni mmoja tu mkamilifu hakuna

mwengine. Kwa hivyo, niombe kwa dhati kabisa kipindi hiki bajeti hii ni ya mwisho, kama kuna mtu tumesuguana na tumefukuzana basi tusameheana. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sitounga mkono bajeti hii kama sijapata maelezo ya banda lile pale basi hapatoshi ndani. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub, sasa tunamwita Naibu Waziri wa Afya. Waheshimiwa Wajumbe, walioko nje waje ndani majumuisho yanaanza, tupate *quorum* ya kupitisha vifungu. Mnadhimu wa CCM na Mnadhimu wa CUF waiteni wajumbe. Kazi ya Baraza ni kushiriki kwenye Baraza. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, *Audhubillah Minasheytwan Rajiim, Bismillah Rahman Rahiim*. Mwenyezi Mungu atupe kauli thabiti hasa tunapokuwa tunafanya mambo haya ambayo yanagusa roho za wananchi moja kwa moja na afya za wananchi.

Ningependa sana ndugu yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, angekuwepo, kwa sababu baadhi ya hoja zinamgusa moja kwa moja yeye. Lakini kwa kuwa naelewa kuna Kitengo cha *Hansard* na kinachukua mambo mbali mbali, kwa hivyo, kokote aliko atakuwa anasikia, tofauti na vile ndugu yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alivyosema, alifikiri hatumsikii tulikuwa tunamsikia na waziri husika alikuwemo humu ndani na yale yote aliyosema yameandikwa na ninayo hapa mbele yangu. Sasa sijui kama ni kwa lengo la kuakhirishwa Baraza au jengine. Lakini yote aliyoyasema yapo hapa na mengi na mimi katika kuunga mkono hoja nitayachangia.

Kwanza kabisa naomba nitowe pongezi za dhati. Mimi pongezi zangu zinakwenda kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi leo wote, kwa sababu katika miezi hii minane niliyokuwepo mimi katika wizara hii, naweza kusema Baraza hili limenipa mafunzo makubwa sana, limenifungua macho, nimepata kuiona sasa hivi dunia kwa upeo au mwanga mwengine kabisa, maana Wizara ya Afya sio jambo la mchezo.

Mhe. Naibu Spika, mpaka leo mimi binafsi sijamaliza vituo vyote, kwa sababu vituo vyote ni 82, sijamaliza mpaka leo kuvitembelea vituo vyote. Sasa hivi niko kwenye *target* ya 58 au *maximum* 60 vilivyokuwa vimeshakwisha na vinafanyakazi na kadhalika. Kwa hivyo, bado kama zaidi ya 20 nimebakisha na sio rahisi. Nina amini na waziri naye hivyo hivyo hajavimaliza vituo vyote. Kwa hivyo, ni wizara kubwa, pana na ni wizara iliyokuwa na kijiji chake ambacho kina wafanyakazi zaidi ya 1,000 Hospitali ya Mnazi Mmoja peke yake. Ni wizara ambayo pana ina wafanyakazi ambao jumla yake ni karibu 3,000 ni 2,800.

Kwa hivyo, nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo tuliokuwa nao kwenda kwenye maeneo ambayo yameguswa na ndugu wajumbe. Kwanza kabisa nitaanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Naomba nimthibitishie kwa upande wangu mimi, kauli yake aliyoitoa ya kwamba kama amemkosea mtu au kama amemuudhi basi kwangu mimi niko safi. Natamani na Dk. Sira kama angekuwepo angeweza kuisikia kauli yake hiyo.

Kwa upande wetu sisi tuko safi kabisa na tunawashukuru yeye pamoja na wajumbe wengine, kila wakichangia masuala haya basi tunapata na sisi kutoa uelewa mkubwa, tunapata kujua na tunapata kufika sehemu za *store* ambazo nyengine zimegeuzwa zimekuwa za wagonjwa wa sukari. Hasa wale Waheshimiwa Wajumbe, waliochangia kwenye eneo la wagonjwa wa sukari, ile ilikuwa ni *store* hapo awali, kutokana na ufinyu wa nafasi ndio maana imegeuzwa kutoka *store* sasa imekuwa ni sehemu ya kuwashughulikia wagonjwa wa sukari na ndio maana hakuna nafasi ya vyoo vya kutosha, kuna choo kimoja tu eneo lile na hapo nadhani hilo litakuwa limejibika.

Pili, naomba nimuombe Mhe. Jaku, unajua serikali ina utaratibu wake. Ni kweli lile eneo la mbele pale la kupumzikia lilitolewa kauli hapo awali, ni kweli ramani yake iliwasilishwa upande wa Mnazi Mmoja hapa na Mhe. Juma Duni Haji wakati ule. Ni kweli kibali na Mamlaka ya Mji Mkongwe imefanyiwa kazi na kupatiwa kibali. Waheshimiwa Wajumbe, ningewaomba mkanisikiliza ili mpate faida kubwa zaidi, maana nina waraka hapa.

Kwa hvyo, yote hayo yamefanyika, lakini tulipofika kwenye taratibu za serikali tukajakuambiwa na nyie nyie Wawakilishi humu ndani tutakuja kugeukiana kama watu hawajafuata zile *procurement procedures*. Jana Mhe. Haji Omar Kheir, alijibu hapa, kuna vitu huwezi kuvunja sheria, lazima zile sheria zilizowekwa na kanuni lazima zifuatwe. Sasa tukaambiwa kuna sheria hii ya *tender board*. Kwa hivyo, hapa nina barua rasmi ambayo Katibu Mkuu wa Wizara ameshamuandikia Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Afya na barua hii nitaisoma mbele yenu, ili muelewe huo mchakato umefikia wapi na nitatumia *forum* hii hii kutangaza leo rasmi. Wale wananchi wote watakaokuwa wana hamu ya mradi huu, ama kwa kushirikiana ama kwa *PPP,* ama kwa njia yoyote nyengine, basi wanakaribishwa. Naomba nisome Mhe. Naibu Spika, hii barua.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mchakato wa ukarabati na kuendeleza bustani iliopo mbele ya Hospitali ya Mnazi Mmoja mkabala na kituo cha daladala. Napenda kukuarifu kwamba, hii anaandikiwa Mwenyekiti wa *Tender Board, ee.* Napenda kukuarifu kwamba tumeshapatiwa ruksa rasmi ya kuendelea na kuliendeleza eneo la bustani hiyo iliopo mbele ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kupitia Wizara ya Afya, tunatarajia zoezi hilo lianze mara moja. Hivyo, inabidi tuanze na kutangaza

kwa kupitia Bodi ya Zabuni, ili tuweze kumpata mdau. Mhe. Haroun nisamehe, hii imeandikwa mdau, ingawa mimi naelewa ni muhusika mkuu huyu, lakini hapa pameandikwa mdau na mimi itabidi nisome kama ilivyoandikwa. Atakayeshirikiana na sisi, yaani sisi Wizara ya Afya, katika ukarabati na ujenzi huo kama inavyoonesha katika kiambatanisho hiki. Kiambatanisho hiki kimeandikwa kwa Kiingereza, lakini nitasoma *heading* ambalo ni tangazo rasmi linalokwenda kwenye gazeti.

*Call for Partnership Propose Reabilitation of Mnazi Mmoja Hospital Pack and Bus Daladala Terminal. Mnazi Mmoja Hospital is situated in Stone Town of Zanzibar,* na kadhalika huko *mbele.* Kwa hivyo, hapa inasema*; The Ministery of Health Six to Emplement this Project Through a Transparent Public Proccess and Innovative Public Private Partnership* an Sheri yote imeshapitishwa hapa. *In order to implement to proposal Rehabilitation of the Mnazi Mmoja Hospital Park and the Bus Daladala Terminal Stand on the other Side. The assailment will also included development of the Visitors waiting shade, together with expansion of Bus Terminal and Associated Structure, Pharmacy, Kiosk, Public Toilet, Chafee and Restaurant Services, That will serve the daily Population Attending the Mnazi Mmoja Hospital.*

Mhe. Naibu Spika, naomba nisimalizie, kipande hicho ni muhimu sana. Sasa tunawaombeni Waheshimiwa Wawakilishi wote. Hili suala tayari limeshapitishwa na sasa hivi linaelekea kwenye tangazo. Tangazo la mwanzo ndio tunalitoa hapa leo. Kwamba Makampuni, watu binafsi, wawekezaji, hao waliojenga bandari, hao waliojenga majengo mengine, hao waliojenga *Restaurent,* hao waliojenga vibanda vya *Beaure de Change* Darajani na kwengineko. Wote wanakaribishwa kuleta *Proposal* yao kwa ajili ya kujenga eneo lile, kwa sababu serikali imeamua kwamba inataka kufanya *Public Private Partnership.*

Mhe. Naibu Spika, hakuna fedha iliyotengwa moja kwa moja kwa kuliendeleza eneo lile, badala yake tunawaalika kwa sababu pale patakuwa na mambo, kama *Pharmacy, Restaurent,* Kiosk na vitu vyengine, kama ilivyoandikwa kwenye waraka huu ambao unatarajiwa kuendeshwa na watu binafsi.

Naomba sana nimuomba Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, baada ya kulileta hili suala, tumefanya mawasiliano na watendaji wetu, tunakuomba sana. Kwa kuwa sisi Wizara ya Afya tuna bahati moja, tuna bahati kubwa ya kuonewa huruma, hususan na hawa *DONAZ* wenzetu wafadhili wa maendeleo. Kama utakuwa umeona bajeti yetu hii imetengwa ipo kipande cha serikali na ipo kipande cha wafadhili wa maendeleo. Naomba nikuthibitishie kwamba hivi karibuni kwa wale waliouliza swali lile, Mhe. Mshimba, nakumbuka alipiga chafya alipokwenda

kwenye mavumbi pale kwenye mafaili yale na akapiga chafya tena nyengine humu ndani kwa kukumbuka kule tu.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba wale Waheshimiwa Wajumbe wote waliozungumza habari ya ile *medical record system*, tunaondokana na yale mafaili, tunaondokana na yale mavumbi, tunaondokana na chumba kile, kitabadilika na patakuja *system* ya kisasa. Tuombeane kwa Mwenyezi Mungu turudi humu ndani ya Baraza na yale mambo yaliyoanzishwa yaweze kuendelea. Mimi nawaombea dua Mwenyezi Mungu awajaalie wote warudi *Inshaallah* katika kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pale palikuwa na tatizo tulikuwa hatuna bajeti. Lakini tunawashukuru sana ndugu zetu wa *WHO, World Health Organization*, tumewaomba juzi tu wametuletea jibu kwamba tumepata msaada wa karibu shilingi milioni 100 za kuweka *Computerization* ya *Medical Record* ya Hospitali nzima. Kwa hivyo, watatusaidia baadhi ya kompyuta za kuweka hospitali na kitengo kile sasa kitageuka badala ya kuwa na mafaili na mavumbi yale ya kupiga chafya, sasa itakuwa kila kitu *Automatic Computerized*.

Hata wale waliokuwa wanalalamika kina Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, waliokuwa wanalalamika kwamba ile filamu ya *CT Scan* hakuna. Siku hizi yale mambo ya ku-*print* yameshapitwa na wakati. Ndio. Nenda leo kwa wenzetu hawa *Global Hospital*, pale wanakuita kwa Turky maarufu, wao hawa- *print* tena *X-Ray*. Moja kwa moja unakwenda kwenye kompyuta. Kwa sababu kuna *staffs* wetu wengine wanafanya kazi *per time* pale jioni tunajua sisi. Hawa *staffs* wetu wamepata ujuzi mwengine mpya pale. Kwa hivyo, naamini na sisi tukileta huku wataweza kuja kutusaidia.

Kwa hivyo, pale unakwenda kwenye *screen* na inakwenda moja kwa moja mezani kwa daktari kwenye *screen* anafungua kwenye *screen*. Kama Maalim Haroun anatizamwa kichwa chake, kinaonekana kichwa chake chote pale kwenye *screen*. Hana haja tena ya yale mambo ya ku-*print slide*, kwa sababu na yale pia yana gharama, yale ma-*plastic*, ma-*chemical*, madawa yale ya kuchanganyia yana gharama yake nyengine.

Sasa kule Mhe. Mahmoud Muhammed, *WHO* wametusaidia kama shilingi milioni 100. Nakuomba sana hizi shilingi milioni 100 usizizuwie, kwa sababu tuna njia nyingi ya kuomba fedha kwa hawa wafadhili wetu na nina amini watatusaidia, wako wengi sana. Ikiwa hawa wametusaidia ndani ya kipindi cha miezi minne, mitano hii tumeweza kupata pesa hizi na ndani ya miezi mitatu mingine itakuja Kampuni maalum ambayo itachaguliwa kupitia Bodi ya Zabuni kuja kufanya

mambo yale, naamini na kwenye *lift* inawezekana. Mimi nilikuwa nina ombi hilo na ninatarajia utanikubalia.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, pia tunamshukuru sana kwa mchango wake aliochangia na mimi nitajikita zaidi kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Maeneo mengine yupo mwenyewe Mhe. Waziri, atakuja kuyaweka sawa pale popote nitakapokuwa nimeweka kasoro kidogo, yeye ataweka sawa. Lakini nitajikita zaidi kwenye eneo la Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *CT Scan* kwa nini haina filamu. Nimeshaeleza siku hizi tunakwenda kwenye *modern way,* wanaangalia kwenye *computer*. Tatizo letu kubwa ni lazima nilikubali ni *rediologist* yule wa kusoma ile, hilo ndio tatizo letu. Ehee! jambo la ukweli ni lazima tuseme, tatizo letu *rediologist* na waliokuwepo sasa hivi wengine wanasoma, pale tunamtegemea mtaalamu mmoja wa Kichina, akiondoka au akipiga chafya yeye basi tunaumia. Ndio.

Kwa hivyo, tunachotaka kufanya sasa hivi ni kwamba yule *rediologist* tupate vijana wetu wa Kizalendo waweze kusoma na kutafsiri. Bado tunawategemea pia wenzetu wa vitengo vya *Newro Surgical Unit*. Inabidi kama Ustadh Mohammed au mwengine kule atoke aje huku kuja kusoma kwenye *CT Scan,* wakati mwengine inakuwa shida hiyo. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akitujaalia, mtandao mpya ukishaunganishwa, basi wale watu wa *Newro* wataweza kuona picha kutoka pale moja kwa moja. Wewe unapigwa picha huku kule kwa daktari imeshafika unaonekana. Kwa hivyo, kama mgonjwa akiingia huku kule tayari atakuwa ameshaonekana. Kwa hivyo, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, naomba hilo utuchukulie kwa muda kidogo mpaka wagonjwa na wananchi wazowee na sisi *system* zetu zitanuke na zizowee pia hayo yatatatuliwa.

Vile vile, ulizungumzia mashine ile ya *full blood picture*. Naomba tena nirudie Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na wewe kwamba mashine ile ya pale ndani *laboratory* haifanyi kazi, mashine inayofanyakazi ni ya kule *Firstrack* Mapinduzi Kongwe, nilikwenda tena leo kuiangalia inafanyakazi. Huko ulikokwenda wewe ukatolewa damu ikafanyiwa *full blood picture* ukalipa na fedha ukapewa na risiti, maana nimeambiwa na risiti umepewa. Mashine ya huku yule aliye-*supply* hakufanya kosa lolote na hapa ipo. Niliambiwa ni Kampuni inayoitwa *Bwire Surgical Limited,* ndio walio-*supply* na wanafanya *services* hawa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tatizo lililokuwepo ni umeme wetu huu wa kupanda na kushuka, imeunguza *Power Suppy Unit*. Kwa hivyo, *Power Supply Unit* ya mashine hii imeungua kwa hivi sasa na ripoti zipo hapa, hizi ripoti za mafundi. (Mjumbe Kakohoa hapa),Naomba apewe maji Mhe. Mjumbe asije akaanguka, ingawa *oxygen* ipo ya kutosha hospitali.

Kwa hivyo, hapa pana ripoti kamili ya mafundi na Mwenyezi Mungu akitujaalia mashine hii iliyokuwa haifanyikazi, imetengenezwa tena mara ya mwisho. Tarehe 28/04/2015 katika *comment* yake fundi amesema; "*Not successfull until the machine is replaced with power supply unit*". Hii hapa, kwa hivyo, hilo linaendelea kushughulikiwa wakati huo tunatumia mashine yetu ile iliyokuwepo pale Mapinduzi Kongwe.

Vile vile, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, aliuliza swali la *oxygen*. Nimepata tena takwimu sahihi, nilitoa takwimu leo asubuhi katika swali kwamba tunatumia pale karibu chupa 240 kwa mwezi, lakini nimerekebishwa ni chupa 400 kwenda juu kwa mwezi. Chupa 100 zinakuja kwa wiki, zinaagizishiwa kwa kila wiki na kama nilivyosema hapo awali *solution* ni kujenga *tank* la *oxygen* ambalo litaweza ku-*supply oxygen*. Kwa hivyo, kwa hivi sasa tunaendelea kushirikiana na wenzetu wanaotu-*supply*, wakati mwengine tatizo linakuwa kwa upande wa usafiri wa kufikisha zile chupa, wakati mwengine zile chupa zilizokuweko hapa inabidi zirudishwe, ili chupa nyengine zifike hapa, lakini kwa hivi sasa *oxygen* ipo *oxygen*, ya *emergence* ipo, *oxygen ya ICU* ipo, hakuna *oxygen* kila wodi kwa muda huu, hakuna oxygen ile ya kufungua *pipe* ikatoka ikamwagika hakuna.

Kwa hivyo, tutakapoweza kupata *supplier* ya kutosha haya yatapatikana, lakini kwa *emergencies* za hapa na pale *oxygen* hiyo ipo na inaweza kuhamishwa wodi yoyote ambapo itahitajika kwa *emergency* ya aina yoyote. Mheshimiwa, nimesha eleze kuhusu chumba cha kumbukumbu mazingira hayaridhishi mambo yetu ya *computers* haya mapya yanayokuja.

**JENGO LA MACHO**

Mhe. Naibu Spika, jengo la macho katika bajeti hii limetengewa kama milioni mia saba *Development Budget* na jengo lile lina masharti maalum na magumu kweli kweli kwa sahabu liko chini ya *heritage*, yaani urithi wa kitaifa hawa *UNESCO* pamoja na Mamlaka ya Mji Mkongwe, kwa hivyo, tukifanya *repair* baadhi ya mbazo zilizokuwemo mule ndani lazima tuzirudishe kama walivyofanya *repair* wenzetu wa Serena na hii Hayate Hotel hizi za kisasa utaona zile mbao za zamani nyengine zimeweza kurudishwa. Kwa hivyo, na jengo hili lina masharti kama hayo.

Kwa hivyo, inakuwa vigumu wakati mwengine kupata fedha ya kutosha kuweza kulirudisha katika hadhi yake ile ile iliyokuwepo, kwa hivyo, tunachofanya sasa hivi tumepata hizi milioni mia saba naamini itapelekwa kwenye mambo ya *tendering process* kama lilivyofanyika Jengo la Manispaa pale *Horis Road* leo linafanyiwa *repair* ya kisasa kabisa, lakini bila ya kubadilisha mfumo wake wa kale basi na hili pia litafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, *ICU* ya Wenzetu wa China Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ameisifu sana, amesema ni ya kisasa na ni nzuri sana, kwa nini haifanyi kazi mpaka sasa hivi, *ICU* tunaitafutia wafanyakazi wake maalum hapa kunatakiwa wale *seniors* wanaita "*Intensive Care Nurse*" pamoja na "*Intensive Care Specialist*" wanaotakiwa kuwekwa hapa.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa mnaokwenda kuswali mrudi kwa sababu mkishamaliza msizungumze tuje tupitishe vifungu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kwa mujibu naomba hapa nisome kidogo. Kwa mujibu wa miongozo iliyopo ya wodi hii ya *ICU*, yaani hii ya kisasa ili iweze kufanya kazi kunahitajika kuwepo kwa wafanyakazi wafuatao hao ndio muhimu wawepo.

Wa kwanza kabisa *Anesthesiologist* yule wa kutoa fahamu, mmoja *Medical Officer, General Nurse, Nurse in charge, Diploma Nurse 12, Critical Care Nurse 14* wanahitajika. Kwa sasa wafanyakazi waliokuwepo tulionao wote jumla yake ni 12 tu, na hawa hawakidhi haja. Kwa hiyo, katika hatua zinazofuata wizara imefanya usaili hivi karibuni na jana tu imepata kibali cha kuwachukua *staffs* wa kitengo hiki, kwa hivyo, tuombe Mungu *Inshaallah* hivi karibuni mambo yote yatakuwa sawa kwenye *ICU* hii mpya, wakati huo huo wengine wale kutoka ile *ICU* ya zamanai wakihamia kuja huku *ICU* mpya.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea Mnazi Mmoja lugha za watendaji, lugha za wale wauguzi, lugha za ma-*nurses*, lugha za askari wa mlangoni, lugha za wengine wote waliokuwepo pale. Hapa ni *two sides of the coin*, yaani kuna pande mbili za shilingi, wengi wamesema wengine wajuba, wajeuri, wakorofi, Waheshimiwa mbali mbali wameshawahi kwenda pale, mimi mwenyewe nimeshawahi kwenda, wengine ndio waligaragara wakapiga na ma-*camera* yakatoka kwenye *TV*.

Sasa ninachotaka kusema pana mambo mawili kwanza tuangalie *natural character* ya watu afya, watu wa afya sio watu kama sisi wanasiasa, unaweza kujipinda huku, leo ukazungumza huku, leo ukacheka, leo ukamuudhi huyu, lakini baadae ukaomba samahani, Mhe. Jaku, anakupiga halafu anakuja kukwambia, aah, kama nimekukosa nisamehe, wao hawako hivyo, watu wa afya kidogo wako tofauti. Wao wako kwa ajili ya ile kazi yao na wakati mwengine wanapofika wagonjwa pale unakuta yule mfanyakazi ameshafanya *overtime* na hajatoka amefanya kazi siku nzima.

Kwa hiyo, hata ile *mood* yake inakuwa si nzuri, lakini wakati huo tuangalie upande wa pili wa shilingi, mgonjwa au muuguzi wake anapokuja na yeye anakuja kwa

kishindo, kwa kifua, lazima tuambizane ukweli, anaanza huyu kwanza ujuba ndio anampa nafasi ya yule na yeye kujibu ujuba. Kwa hiyo, mimi nasema hivi sisi tunaendelea kuzungumza na wafanyakazi wetu, kwa bahati nzuri wafanyakazi hawa wauguzi pamoja na kada nyengine zote pale hospitali ya Mnazi Mmoja na vituo vyengine vya afya wao wanapata masomo maalum ya *ethics* ambayo wanasoma hata hapa Mbweni katika Chuo cha Afya Mbweni yanasomeshwa masomo hayo na leo nilikuwa nazungumza na Bi. Amina Abdulkadir Kaimu Mkuu wa Chuo amenambia katika miongoni mwa masomo vijana wanaofaulu pale wanaofanya vizuri sana kwa upande wa kupata maksi ni masomo haya ya *ethics*, yaani namna ya kumnyenyekea mgonjwa, namna ya kumbembeleza, namna ya kutoa mambo huduma nyengine mbali mbali, ndio *nursing* yenyewe, *nursing* maana yake *nurse* hasa kauli hii "*nurse"* maana yake kunyonyesha.

Maana yake hasa ni kunyonyesha, mnyama akimnyonyesha mtoto wake anaambiwa *a cow is nursing the scarf,* kwa hiyo, na wao walikuwa wanatakiwa kutoa mapenzi kama hayo na tunajua mapenzi ya mama anaponyonyesha inavyokuwa.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema sisi tunaendelea kuzungumza na wafanyakazi wetu. Lakini nakuombeni Waheshimiwa wawakilishi, mnapozungumza na wananchi au mnapopata lawama kama hizi msiziweke tena kwa muda mrefu mpaka msubiri bajeti hadi bajeti au mwaka hadi mwaka ili ulete hapa kwa sababu tunashindwa kulitekeleza au kulitatua tatizo lile linapokuja, leo nadhani Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi, yeye alieleza suala la yule mtoto aliyepata taathira, sasa linapotokezea jambo kama lile kuna vitengo vya kupokea lawama, kuna vitengo vya kupokea malalamiko, kuna kitengo pale cha Mkurugenzi Mkuu Dk. Jamala ambaye yupo humu ndani sasa hivi. Kuna kitengo cha Muuguzi Mkuu *incharge*, kuna kitengo pale cha Katibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambavyo vyote hivyo vinashughulika na kupokea lawama na vyote vipo katika *Administration block* ghorofa ya kwanza.

Sasa mnapokaa mpaka mkapoteza na ushahidi mwisho tunashindwa kuchukua hatua, naomba panapotokezea matatizo kama haya, nakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe na kupitia kwenu tunawaomba wananchi wowote panapotokezea matatizo kama haya msimsubiri Mhe. Rashid Seif au Mahammoud Thabit au mwengine yeyote nenda moja kwa moja panapohusika ambapo ni jengo la utawala, Mnazi Mmoja *INT* iko chini pua na masikio wao wako ghorofa ya kwanza uwasilishe malalamiko yako.

Naomba Katibu wa Mnazi Mmoja asimame yupo huyo hapo, bahati nzuri yupo nataka wajumbe na wananchi wote wakuone, ma-*cameras* yote ya *TV* yakumurike wewe sasa hivi. Huyu ndio mhusika mkuu wa kupokea malalamiko, sasa leo

unapoleta malalamiko humu ndani moja kwa moja, kwanza umemnyima haki yake ya kufanya kazi, Ahsante sana katibu. Naomba sana panapotokezea matatizo kama hayo basi yaweze kufikishwa kwa katibu ili tuweze kutatua na kwa baadhi ya lugha tutaendelea.

Kitengo cha *Neuro Surgery* pale Mnazi Mmoja ni kweli sasa hivi tunawategemea wataalam wetu kutoka Spain na tuna mtaalam mmoja tu ambaye ni *Junior assistant medical officer* yule anayeitwa Mohammed Ustadh, lakini kwa kweli tunampongeza sana anafanya kazi nzuri sana, wanapokuwa wa Spain hawapo anafanya kazi nzuri sana, tunaye mtaalam wetu mmoja ambae sasa hivi anasoma China *Neurosurgical Unit* yuko China anasoma na jina nimepewa hapa lakini sitaki kumtaja nataka amalize masomo yake kwa salama, akija tunatarajia yeye ndio atashika kitengo kile yuko China. Kwa hivyo, tukishamaliza hapo atakuja yeye na ataendelea kushirikiana na ndugu zetu wa Spain.

Nimeeleza nadhani yote nimeyakamilisha, sasa labda kwa kumalizia upande wa *lift* nimezungumza na nimemuomba Mheshimiwa. Kuhusu hali ya usafi leo, jana, juzi nimeligusa sana suala hili hali ya usafi Mnazi Mmoja, nilikuwa leo nazungumza na *Staff* mmoja na ilikuwa ni wodi ya wazazi nikamwambia nyie mnasemwa sana na bahati mbaya kule Baraza la Wawakilishi nyie hamuwezi kuja kujibu ninayekwenda mimi pale kwenda kujibu hamuwezi nyie kuja huku chini kuteremka kujibu ni mimi ninayejibu.

Hebu niambieni suala la usafi liko vipi, wakanambia hivi: matatizo ya usafi ni pande mbili; kwanza ni upande wa kusafisha kwa wakati ambao wao wanafanya wanasafisha kwa wakati, lakini la pili upande wa pili wa shilingi ni utamaduni wetu wa usafi, panapotokezea mfanyakazi keshapita pale kasafisha halafu akatokezea mgonjwa hana utamaduni wa kutumia choo cha kukaa, narudia tena hana utamaduni wa kutumia choo cha kukaa, akenda pembeni kama sisi tungekuwa wasafishaji tungejihisi vipi, tufikirie hapo tu kama sisi tungekuwa wasafishaji tungejihishi vipi, ndio kwanza umemaliza kusafisha wewe anakuja mtu paaa pembeni pale, anakuchia kila kitu tena, ehee, nashukuru Mhe. Maalim Haroun kasema kauli hiyo.

Kwa hiyo, hili tatizo lipo na mara nyingi linatokezea wanasafisha na nimeuliza wana *scorches* za kusafisha, wodi ya *matenity* wanasafisha zaidi ya mara kumi na mbili kwa siku na bahati nzuri kuna vijana wa kiume shababi ambao mimi mwenyewe nimeona wapo wana nguvu za kusafisha pale wodi ile ambayo mara nyingi huwa wanakuwa wafanyakazi wa kike, kwa hivyo, naomba sana kupitia Baraza lako Mhe. Naibu Spika, kwamba na sisi utamaduni wetu wa usafi uwepo pia, pale sisi tutaendelea kujitahidi, vifaa vya usafi vitaongezwa, tunashukuru ndugu zetu *JAPAIGO*, kila Jumapili tutafanyakazi nao tena kwa ajili ya kampeni

ya za usafi na sisi wenywe tutakwenda tumeshajihishana na Mhe. Mgeni Hassan Juma, pamoja na Kamati yake ya Ustawi wa Jamii, tukasema kila baada ya muda tutakuwa tunatembelea pamoja pale tunajitolea kwa ajili ya kufanya usafi. Na wao watapata kuona, lakini panapotokezea tatizo hilo kwa kweli inaumza.

Lakini jengine nafikiri Mhe. Marina, alilitaja hili kuhusu msongamano wa watu, nadhani ulikuwa wewe kama sijakosea au mjumbe wowote mwengine kwenda *maternity* pale mchana, kuna msongamano mkubwa sana, na ni kweli tatizo kubwa sana mpaka sasa hivi tume-*fall* hapo sisi, kwa sababu pale tunatakiwa sisi tutoe *system* ya *identity,* yaani kila mgonjwa aweze kuwa na *identity* yake moja, wawe wanapokezana mtu mmoja mmoja kwenda kuangalia mgonjwa, hawawezi wala hatuwezi kuwaruhusu wote wale.

Na wakati mwengine mgonjwa mmoja anakuja na kijiji kizima kutoka Makunduchi wanakodi gari zima wanakuja kumtazama mjukuu wao, basi Kizimkazi ndio huko huko jimbo hilo hilo, wanakodi gari zima wanakuja pale, kwa hivyo, inakuwa tabu hawawezi kuingia wote kwa pamoja, kwa hivyo, tunatakiwa sasa hivi tuwe na *system* ya *identity,* tunaendelea kujadiliana na Mkurugenzi wa Mnazi Mmoja Hospitali, kuanzia mlangoni tuwe na *identity,* Waheshimiwa, wanasafiri kila siku wanaona India kulivyo wenzetu India ukifika tu wanakutia bandi siku ya kwanza wewe mgonjwa, pili wanakupa kitambulisho yeyote atakayekuja kutembelea mpe hichi, bila ya hichi hawezi kuingia kukuona wewe mgonjwa wake.

Kwa hivyo, hilo ni kweli msongamano unakuwa mkubwa sana hasa wakati wa mchana na jioni na hasa katika *maternity wod* na la pili pale Hospitali wanakuja watu wengi kwa siku wanakuja watu zaidi ya 2,800 mpaka 3,000 wakati mwengine, na kila mmoja anakuja na nia yake, huwezi kujua nia gani, kila mmoja anakuwa na nia yake; kuna vitu vimeshapotea pale, kuna mambo yamepotea, kuna nyaraka na kadhalika. Kwa hivyo, lazima sisi tuchukue indhari za kuweza kuweka *control,* kwa hivyo, hilo lazima lifanyike, mtatusamehe kwa muda huu, lakini tutaendelea kutoa mashirikiano ya karibu na nyie kwa lugha nzuri kwa watu kwenda kwa zamu kwenda kuwaona wagonjwa wao, kwa sababu na wagonjwa nao wanahitaji utulivu, hawahitaji hali ya kuwa-*disturb.*

Mwisho kabisa kwa uachache, suala la hizi *allowance, allowance* hizi ziko nyingi; kuna *risk allowance* na *disturbance allowance* ambazo zinawahusu wafanyakazi wa Mnazi Mmoja na wafanyakazi wa sehemu nyengine mbali mbali ndani ya kada ya Wizara ya Afya, kada zote za Wizara ya Afya, *responsibility, disturbance* na kadhalika, hizi kuna baadhi ambazo zimetolewa kibali na utumishi na Wizara ya Fedha wanalipa na kuna baadhi bado hazijatolewa ruksa, kwa hivyo, hizi tunakwenda kuzifanyia kazi na zikishakamilika tu na hususan hii *risk allowance* basi itaweza kufanyiwa kazi.

Upungufu wa wafanyakazi upo, tuna *deficit* kubwa sana kwa wafanyakazi, tuna *deficit* sisi zaidi ya wafanyakazi 200 sasa hivi, lakini kila tunapopata kibali cha utumishi na kibali cha Wizara ya Fedha kwa ajili ya mishahara kufanyiwa *allocation* tunaendelea kuajiri na ndio maana ata wiki hii mtaona watoto kama 30 wataajiriwa kwa ajili ya kuingia katika kada mbali mbali. Kwa hiviyo, tunaomba sana tuvumilie sio juu yetu sisi tu lakini ni *system,* kwa hivyo, tunapopata kibali basi hatutoacha kuchukua wafanyakazi hao ili tuweze kufanyakazi nao kwa pamoja katika kuliendeleza Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nimalize mimi naunga mkono hoja kwa asilimia moja. Mhe. Saleh Nassor Juma, simuoni leo lakini alikuwa kanichokoza sana pale kwenye *Predator - Prey Relationship,* aliwahi kuniambia ana nyaraka tena Mhe. Waziri na hili narudia tena aliwahi kunambia ana nyaraka nzuri sana ya kutusaidia sisi mawazo, nashangaa leo amezungumza na nyaraka hiyo hajawahi kutupa na mimi nimeshawahi kumkumbusha zaidi ya mara tatu, nne kwamba tunaomba nyaraka hiyo utupatie ili tuweze kufanya kazi. Basi naomba sana nimkumbushe ili atupatie nyaraka hizo.

Kwa hayo machache Mheshimiwa, tutakuwa tayari kutoa maelezo yatakapohitajika zaidi ili tuweze kupata, kuna suala la bodi ya vyakula na vipodozi nalo hili limeshashughulikiwa na juzi nilitolea ufafanuzi katika jibu la nyongeza kwamba wao wameshapatiwa ruzuku zao katika bajeti hii na ruzuku hiyo itakamilika.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo nakushukuru sana kwa muda ulionipa na naunga mkono bajeti hii kwa *hundred percent,* yaani asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima kwa taufiki yakukutana hapa kwa leo *Inshaallah* kumaliza ngwe yetu ambayo imebakia, na naamini kwamba tutapata mwelekeo wa kupitishwa bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii baada ya kukushukuru wewe kuwashukuru wale wote ambao wamechangia katika mjadala wa bajeti yetu hii wa kwanza akiwa ni Mhe. Farida Amour Mohammed, kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ripoti yao ambayo walitukabidhi na kuisoma. Wapili Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Mwajuma Faki Mdachi, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Mwanaid Kassim Mussa, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Abdalla Mohammed

Ali, Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa, Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Naibu Waziri wa Afya Mhe. Mahamod Thabit Kombo na mmoja amechangia kwa maandishi namshukuru Mhe. Salma Mussa Bilali.

Mhe. Naibu Spika, katika baadhi ya masuali ambayo tumeulizwa kabla sijayaeleza kwakumalizia namshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa kuendeleza majibu karibu yote ya Hospitali ya Mnazi Mmoja tuliyoulizwa, lakini mimi nina nyongeza ndogo *lift* katika Mnazi Mmoja ziko mbili moja inafanya kazi na iliwekwa mpya kabisa kabila ya *OTUS,* hii moja ndio bado imebaki kongwe ile ile, kwa hivyo, lile ombi la Naibu waziri, kukuomba sio Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa tu, lakini tunawaomba radhi watu wote kwamba tumo katika utayarishaji wa uhakika wa kupata *lift* nyengine mpya na sio kutengeneza ile. Kwa sababu ile ni kongwe sana na kwa mujibu wa *technology* ya sasa ni afadhali kupata *lift* mpya kuliko kutengeneza ile ambayo ipo tokea miaka 50. Kwa hivyo, Mheshimiwa hilo linashughulikiwa.

Lakini la mwisho ninalotaka kusema kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja kweli hospitali ile tukitaka tusitake ni hospitali ya Rufaa. Kwa sababu Hospitali ya Rufaa ni pale ambapo hospitali nyengine zote zimeshindwa anapelekwa mgonjwa pale. Sasa bahati nzuri sisi tunao ushahidi sasa hivi, ambapo mpaka Hospitali ya Al-Rahma bado kuna *time* wanawaleta wagonjwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kutoka Al-Rahma mbali ya hospitali zetu.

Lakini kweli kazi kubwa inahitajika kuweza kukamilisha utaratibu wa kuifanya kwamba ni Hospitali ya Mnazi Mmoja. Moja wapo ambayo tulizungumza sana ni kuipatia wataalamu yaani madaktari mabingwa ili wao ukishakupata yule daktari bingwa yeye ndiye atakayesema mimi nileteeni hichi, nileteeni hichi. Wao ndio chanzo kikubwa cha kuimarisha zile idara zao watakazokabidhiwa. Kwa hivyo, jambo la mwanzo ni kupata daktari bingwa ambaye ataweza kuijenga ile idara yake, tukimkabidhi kama ile *Neuro Surgical* iliyo pale wale madaktari ndio wanaoijenga ile idara. Ikiwa tunafungua *Urologist department* wale ndio watakaonini. Kwa hivyo, jambo la mwanzo ni kupata wale madaktari mabingwa kwa kuwatumia wale ndio watakaojenga ile idara.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya maswali mengine yaliyokuwa sio ya Mnazi Mmoja yaliyoulizwa ni kuhusiana na ruzuku lakini ameshaitaja Mhe. Naibu Waziri wa Afya kuhusu ruzuku ya vipodozi. Tayari kuanzia bajeti ya mwaka huu tayari imeshaanza Bodi ya Madawa, vyakula na vipodozi, imeshaanza kupata ruzuku zake.

Mhe. Naibu Spika, lilikulizwa swali kuhusu kupewa watoto *vitamin* A. Je, *vitamin* A zimefanyiwa utafiti. Jibu lake Mheshimiwa utafiti ulifanyika hapa Zanzibar kwa

watoto chini ya miaka 5 na mama wanaonyonyesha na kugundulika kuwa tatizo la ukosefu wa *vitamin* A kwa watoto na kwenye maziwa ya mama. Kufuatia utafiti huo mkakati wa kuwapatia *vitamin* A watoto kuanzia miezi sita na mama mara baada ya kujifungua ili kuweza kuongeza kiwango hicho kwa mahitaji ya watoto. Mafaniko hayo yaliweza kuthibitishwa hata na kitengo cha macho kwa kuweza kupunguza zaidi tatizo la ugonjwa wa macho, yaani kiza cha macho, kinachoitwa kwa kitaalamu *Zero Trachoma.*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ufafanuzi wa Kwashakoo na Marasma, kuhusiana na Kwashakoo na Marasma, hili ni tatizo la upungufu wa *protein* na uwanga (*starch*) na matibabu yake yanafanyika katika hospitali zote za Unguja na Pemba kwa kupatiwa *therapeutic food*.

Suala la kwamba je, ni wagonjwa wangapi kati ya 1232 walitibiwa kisukari na shindikizo la damu kati ya siku ya Afya ya Kijiji. Ni kweli kuwa huduma zinatolewa katika siku ya Afya ya Kijiji zinasaidia sana kusogeza huduma kwa wananchi kwa vijiji. Kati ya watu 1232 waliochunguzwa watu 42 waligundulika na maradhi hayo.

Je, ni lini huduma za kuzalisha zitatolewa katika kituo cha Afya Ukutini. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kituo cha Afya cha Ukutini kilijengwa kwa kutoa huduma za Daraja la pili ikiwa ni pamoja na huduma za kujifungua kwa awali. Kituo hicho miundombinu ya chumba cha kujifungulia ilikuwa haijakamilika. Lakini kwa sasa kituo hicho kimepatiwa vifaa na miundombinu imefanyiwa matengenezo kupitia timu ya Afya ya Wilaya ya Mkoani. Kuanzi mwezi Julai 2015, huduma za kujifungua zitaanza kutolewa.

Ufafanuzi wa nyumba ya wafanyakazi wa kituo cha Afya Kojani. Ni kweli nyumba ya wafanyakazi katika kituo cha Afya ya Kojani ilikuwa na matatizo na ujenzi wa nyumbe hii umesimamiwa na *TASAF* awamu ya II. Matengenezo ya awali yamefanyika kama vile milango, madirisha, umeme na maji. Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti ya mwaka 2014/15 ya matengenezo, ujezi huo haukuweza kukamika na unatarajiwa kukamilika kwa kipindi cha mwaka 2015/16.

Kituo cha Afya ya Kangani ni kidogo na kibovu, je, ni lini kituo hicho kitajengwa. Kituo hicho ni kweli kama ilivyotajwa Mhe. Naibu Spika, lakini kuna miradi miwili mikubwa sasa hivi katika Wizara ya Afya ya Ujenzi wa vituo. Bahati nzuri Kangani imo katika ujenzi wa vituo kwa mradi wa *Orio*. Vituo vyenyewe vitakavyojengwa kwa mradi wa *Orio* na vyengine ni Bambi, Chaani Kubwa, Chaani Masingini, Chambani, Chonga, Dunga, Fujoni, Kangani na Kiboje, mitaa mengine ni Kijini, Kisiwani, Kipangani, Kizimkazi Dimbani, Makongeni, Shumbaviamboni, Tunguu, Umbuji, Urowa na Wambaa.

Sasa nimeyataja haya kuonesha kwamba sio peke yake, aone kwamba labda nimetaja tu lakini kuna vituo vingi vilivyoorodheshwa. Kwa hivyo, vinajengwa kutokana na awamu mbali mbali. Mimi binafsi nilikwenda Kangani hivi karibuni kukitembelea kituo hicho na nikawaeleza kwamba tayari wajitayarishe na eneo ili mradi ukifika isiwe tena kunatafutwa eneo la kujengwa. Bahari nzuri eneo lipo karibu hapo hapo kilipokituo, kwa hivyo, ujenzi utakuwa ni mwepesi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililoulizwa ilikuwa, je, dawa zinazowekwa kwenye madimbwi ya maji hazina madhara. Jibu ni kwamba dawa hizi sio za kemikali. Haina sumu kwa viumbe vinavyoishi kwenye maji bali ina lengo la kudumaza ukuaji wa vimelea vya mbu vilivyomo kwenye maji, pindi wanapokula hiyo dawa. Dawa hizi kwa *hormones* na sio inatengeneza kemikali, imependekezwa na *WHO*. Dawa hizi zinawekwa kwenye maji kila baada ya wiki tatu baada ya mvua kupita. Wananchi wasiwe na wasiwasi kwa matumizi ya dawa hizi ni salama kwa mazingira ya wanyama na viumbe vyenginevyo.

Kulikuwa na suala la Benki ya damu. Kwa nini benki ya damu kwa upande wa Pemba ipo Wete na sio Chake Chake ambapo ni katikati ni urahisi wa kupeleka. Mhe. Naibu Spika, suala hili lilianzia pale 2009 ilipoanzishwa Benki ya damu. Na kwa Mazingira ya wakati huo basi hali ilikuwa ni hivyo. Kwa sababu tunafahamu kuwa hospitali zote zinatoa tiba ya damu, zina Benki ya damu hii ni Pamoja na Chake Chake, Wete, Mkoani na Micheweni.

Kwa upande wa Pemba ambacho kituo kipo Wete, kituo kinachoitwa *Satellite Site* ya kukusanya damu kutoka kwa wachangiaji wa hiyari na kusambaza damu Benki zote za Hospitali za Pemba, ziwepo tayari kutumika. Hata hivyo azma ya Wizara kupitia kitengo chake ilikuwa ianzishe kituo hicho katika hospitali ya Chake Chake. Lakini kutokana na sababu za kimiundombinu, kituo cha Damu salama ilibidi kianzishwe Wete kwa sababu:

1) Ili uanzishe kituo cha kukusanya na kusambaza damu kwenda Benki za damu za hospitali inabidi kuwe na umeme wa uhakika masaa 24. Wakati tunataka kupeleka huduma Pemba ni Hospitali ya Wete tu ndiyo ilikuwa na umeme wakati kutokana na kuwepo kwa umeme wa *solar*.

2) Wafanyakazi walio na utaalamu wa *hematology* na masuala mengine ya damu walikuwepo Wete. Cha msingi benki za damu za mahospitali zijue mahitaji yao na kuzifuata damu Wete kwa wakati ili wawe nazo tayari kwa kutumika. Vile vile, tunawaomba Wawakilishi mtusaidie kushajihisha jamii kupitia majimbo yetu ili tupate damu za kusha kusambaza katika mahospitali.

Kuhusu suala la lini Hospitali ya Chake Chake itapatiwa daktari wa upasuaji. Hii inatokana na kumaliza muda *surgeon* ambaye yupo sasa hivi alikwenda kwa *contract*, kwa hivyo, Wizara inaendelea kufanya mchakato wa kupata *surgeon* kutoka hapa Unguja, wakati huo huo tuna taratibu ya kupokea *surgeon* kila mwezi kutoka Unguja kwa ajili ya *outreach programme.*

Hivi sasa kuna ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee ya Mkoani. Suala lilikuja, je, itakapokamilika kutakuwa na wafanyakazi wa kutosha? Jibu ni kwamba Mpango wa Rasilimali Watu utaingizwa katika mwaka wa fedha ambao majengo yanatarajiwa kukamilika kupitia utaratibu na *nominal role* itapimiwa nguvu zaidi iliyopo ili kuelewa nafasi iliyopo. Kwa hivyo, utaratibu unapangwa ili wakati utakapojiri wafanyakazi watakuwa tayari. Tayari wengine wapo wanaofanyakazi katika ile hospitali ya muda ambayo ina majengo mbali mbali.

Kuhusu suala la maradhi ya Ukimwi na mambo mbali mbali yaliyojitokeza. Suala la mwanzo lilikuwa ni hatua gani zinazochukuliwa ili kuwarejesha wagonjwa wanaoacha kutumia dawa za kupunguza makali ya virusi vya Ukimwi (*ARV*). Jawabu mara nyingi wagonjwa wanaoacha kutumia dawa za *ARV*, huacha kutumia dawa hizo kwa sababu ya kukata tamaa na kuogopa unyanyapaa. Wakati mwengine wagonja hawa huwacha kutumia dawa za *ARV* na kwenda kutafuta matibabu kwa wataalamu wa tiba asilia.

Hatua zinazochukuliwa ni:

1) Wagonjwa wanaoacha kuhudhuria *clinic* ya dawa hupigiwa simu na kukumbushwa na wanapokosekana hufuatwa majumbani mwao na kupewa ushauri nasaha na dawa. Wagonjwa hawa wanapokuwa katika hali mbaya huchukuliwa na kupelekwa hospitali kwa matibabu zaidi.

2) Hatua nyengine inayochukuliwa kupambana na tatizo hili ni utolewaji wa elimu juu ya umuhimu wa kutumia dawa za *ARV* kitengo cha Shirikishi Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma kimekuwa kikitoa matangazo kuelimisha kupitia vyombo vya habari kama vile *ZBC*, *Zanzibar Cable* na redio mbali mbali.

Suala jengine lilikuwa juu ya bandari, sababu zinazopelekea baadhi ya safiri kutoka nje wasipatiwe chanjo, huko wanakotoka. Jibu ni kwamba Kitengo cha Afya cha Bandari kimekuwa kikitoa huduma za chanjo ya homa ya manjano kwa wageni wanaoingia nchini ili kuepusha uingiaji wa maradhi hayo nchini kwetu. Hata hivyo, sio wageni wote wanaopatiwa chanjo hizo kwa sababu zifuatazo.

1) Wageni waliona tatizo la uzio (*allergy)* zinazowadhuru zile dawa kwa chanjo ya hoja ya manjano huwa hawachanjwi ili kuepusha matatizo ya kiafya.

2) Nchi wanayotoka wageni ambazo hazijaathirika matatizo ya maradhi ya homa ya manjano nao pia huwa hawajanjwi kwani mara nyingi wageni huwa wanaaminika kuwa hawana ugonjwa huo. Wageni waliochanjwa katika nchi nyengine na watoto wachanga waliokuwa na umri wa chini ya mwaka mmoja.

Suala jengine ilikuwa kati ya watu 6499 walifanyiwa uchunguzi, ni watu wangapi waliokuwa wana matatizo ya kiafya. Jawabu, watu waliogunduliwa na matatizo ni 197 na matatizo yenyewe yalikuwa ni *pressure* ya kushuka, homa ya ini, minyoo, uwoni hafifu, matatizo ya moyo, masikio, sukari na pumu.

Mwisho kabisa Mheshimiwa napenda nitoe ufafanuzi kidogo kuhusiana na suala la maradhi yasiyoambukiza yanaitwa *NCD*, haya ni maradhi ya kisukari, moyo, *pressure* na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo. Magonjwa hayo zaidi huchangiwa na uwepo wa vichochezi hatarishi, yaani *respecters* ambavyo vimegawika katika makundi mawili.

Vichochezi hatarishi vinavyoweza kuepukika vya namna hii vipo vinne; matumizi ya tumbaku, matumizi ya pombe, kutofanya mazoezi na kula mlo usiozingatia afya kwa mujibu wa utafiti uliofanyika visiwani Zanzibar mnamo mwaka 2001, viwango vya magonjwa pamoja na vihatarishi hivyo vilikuwa kama ifuatavyo. Shindikizo la damu lilikuwa asilimia 33, kisukari asilimia 3.7, ulaji wa matunda na mbogo kama inavyoshauriwa kitaalamu ilikuwa asilimia 2.

Kwa takwimu hizo inatuonesha wazi kuwa bado muamko wa kutumia vyakula vya asili ikiwa ni pamoja na matunda na mboga mboga bado ni mdogo miongoni mwa jamii zetu. Aidha, ugonjwa wa shindikizo la damu iko katika kiwango cha kutisha kwani tafsiri yake ni kwamba katika kila watu watatu basi mmoja ana shindikizo la damu hapa Zanzibar. Hii inajumuisha kama vile umri, jinsi au urithi.

Waheshimiwa, mtu yeyote anapofika umri wa miaka 40 basi tayari mtu huyo yupo hatarini kuweza kupata magonjwa haya. Hivyo, jitihada za makusudi za kujinga ni lazima vichukuliwe ikiwa ni pamoja na kujiepusha na mambo manne niliyoyaeleza hapo juu. Aidha, ni vyema kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara kwani mara nyingi unapopata dalili za magonjwa haya inamaanisha tayari huleta athari mwilini ila yanapogunduliwa mapema hata matibabu yake yanakuwa yana nafuu.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana Wajumbe ila naomba nitoe sentensi mbili tatu kuhusiana na hoduma za afya. Mhe. Naibu Spika, huduma za afya zimegawika makundi mawili.

Kwanza kinga na pili tiba, ni jambo muhimu sana sisi kukimbilia kwenye kinga kabla ya tiba na rasilimali zetu nyingi tukazielekeza kwenye kinga kwa sababu tukiweza kutoa msukumo katika kinga tutaepukana na gharama kubwa ya tiba. Kinga imegawika katika maeneo mengi; maeneo ya kwanza ni tabia za watu wanavyoishi katika maeneo za usafi, namna gani wanavyoweza kutumia utaratibu wa kula, taratibu za kutumia wakati wa kupumzika na wakati wa kufanya kazi. Namna gani kiwiliwili chetu tunachikitumia.

Lakini vile vile kuna taratibu za zilizokwisha kupasishwa na ulimwengu chini ya shirika la *WHO* za kupata chanjo. Yapo maradhi yaliyokwisha kugundulika kwa hivyo tunahitaji kupata chanjo wa wakati. Hasa mama wajawazito, watoto wadogo na wote ambao wanaohusika. Tunahitaji kupata chanjo kwa wakati kabla hatujenda kwenye matibabu.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, napenda kulisisitiza ni kwamba sekta ya afya ili kuweza kutoa huduma bora zaidi inachangiwa na sekta nyingi sana. Moja wapo ni Wizara inayoita Maji, Nishati. Huduma ya maji safi ikiwafikiwa wananchi kunapunguza kwa kiwango kikubwa uwezekano wa kupata maradhi ya kuambukiza.

Utaratibu wa kuwa na barabara nzuri ili wale wanaoumwa waweze kufika katika vituo au wale wanaotaka chanjo waweze kufika katika vituo. Kwa hivyo, sekta hii inachangiwa na utaratibu mzima wa namna gani mipango ya sekta nyengine inavyofika. Kwa hivyo, nawaomba sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuiyone kwamba sekta hii inategemeana na sekta nyengine katika kufikisha huduma zake.

Kwa haya machache nawaomba sana Waheshimiwa muipitishe bajeti yetu ili hao wagonjwa waliyokuwepo tayari mahospitali na hao watoto wetu wanaongojea chanjo na mama wajawazito wanaongoja kujifungua tuweze kuwahudumia ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Habari na Utamaduni:** Naafiki.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*
*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. waziri, hoja imeungwa mkono, sasa niwahoji Wajumbe waliokubali hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2015/16 Wizara ya Afya wanyooshe mikono.

**UTARATIBU**

**Mhe. Mshimba Makame Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, umeona hapa Wajumbe wamesita kunyanyua mikono ili kukamilisha kuwa wamekubali au wamekataa hasa kutokana na akidi kidogo naona ipo pungufu. Kwa hiyo, ningeomba sana Mheshihimiwa kwa kuwa leo tunataka tuipitishe basi ningeomba kiti chako Mheshimiwa kihimize watu ili waweze kutimia tuweze kuendelea.

Kwa sababu hii ni Wizara kubwa sana, tunataka tuipe baraka kubwa Mheshimiwa. Kwa hivyo, ningeomba utaratibu kuhusu watu *quorum* kutimia Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Naomba makarani mnambie kuna Wajumbe wangapi humu ndani.

*(Hapa makarani walihesabu Wajumbe)*

**Mhe. Naibu Spika:** Sasa Waheshimiwa Wajumbe, *quorum* tumeipata. *(Makofi/ Kelele)*

Hebu hesabuni vizuri. Nimeambiwa kuna Wajumbe 31 na *quorum* inatakiwa Wajumbe 41 kwa maana hiyo *quorum* haijatimia. Mhe. Waziri wa Afya nitamwita kesho kumuuliza hoja. Baada ya hapo tutapitisha vifungu, kwa maana hiyo naahirisha kikao chetu hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 4/06/2015 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:04 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 04/06/2015 saa 3:00 asubuhi)*